# USAWIRI WA MANDHARI KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI: MFANO WA *KIU* NA *KIDAGAA KIMEMWOZEA*

**WYCKLIFFE COLLINS JAOKO**

**Tasnifu Iliyowasilishwa Katika Shule Kuu ya Mafuzu ili Kutosheleza Baadhi ya Mahitaji ya Shahada ya Uzamili (MA) katika Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Mount Kenya**

**CHUO KIKUU CHA MOUNT KENYA**

**MEI, 2025**

Mount Kenya University

## UNGAMO NA IDHINI

**Ungamo la Mwanafunzi**

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na wala haijawahi kuwasilishwa kwa mahitaji ya shahada yoyote katika chuo kikuu kingine chochote.

**Saini:** ............................. .............................. **Tarehe:** 21/5/2025

Wyckliffe Collins Jaoko

MAKI/2022/51252

**Idhini ya Msimamizi**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya Uzamili katika Kiswahili kwa idhini yangu kama msimamizi aliyeteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Mount Kenya.

**Saini:** ........................................... **Tarehe:** 23/05/2025......

Dkt. Stanley Adika Kevogo

Idara ya Lugha, Taaluma za Fasihi na Mawasiliano

Chuo Kikuu cha Jaramogi Oginga Odinga cha Sayansi na Teknolojia

Mount Kenya University

## TABARUKU

Ninaitabaruku kazi hii kwa mke wangu mpendwa Josephine Anyango Aremo, wanangu Gefallen Jaoko, Wilphine Jaoko na Blessing Jaoko kwa uvumilivu wenu na kunitia moyo wa kuendelea na kazi hii.

Mount Kenya University

## SHUKRANI

Shukrani za dhati nampa Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kuniwezesha kufikia hatua hii vile vile nampa msimamizi wangu Dkt. Stanley Adika Kevogo ambaye amekuwa wa manufaa kwangu katika safari hii ya kusaka elimu, amenielekeza kwa moyo wenye upendo na bidii za mchwa. Mwenyezi Mungu amfungulie milango ya baraka tele na afya njema ili wanafunzi wenzangu wajao baadaye waweze kufaidi kutoka kwake,shukrani nyingine ziende kwa wahadhiri wangu wote walioniongoza katika kozi mbalimbali pamoja na Chuo Kikuu cha Mount Kenya kwa kunipa fursa ya kunogesha makali yangu katika elimu humo. Bila kusahau familia yangu kwa kunipa motisha ya kuendelea na kazi hii. Mungu awatakrimu baraka tele.

Mount Kenya University

## IKISIRI

Mandhari hufasiliwa kuwa ni mahali na wakati ambapo kadhia, visa au matukio ya kifasihi hutendeka kwenye tungo zinazohusika. Madhari yanaweza kuwa halisi au hata ya kufikirika. Azma kuu ya huu utafiti ilikuwa kuchunguza usawiri wa mandhari katika riwaya ya Kiswahili tukiangazia riwaya ya Mohamed S. Mohamed, *Kiu* pamoja na ile ya Ken Walibora, *Kidagaa Kimwemwozea*. Utafiti ulinuiwa kuyaafikia malengo muhsusi yafuatayo: kubainisha aina za mandhari yaliyotumiwa kuwasilisha ujumbe katika riwaya ya *Kiu* na *Kidagaa Kimemwozea*, kutathmini mchango wa mandhari katika ujenzi wa sifa za wahusika katika riwaya ya *Kiu* na *Kidagaa Kimemwozea*, pamoja na kueleza mandhari yalivyochangia uendelezaji wa ploti ya hadithi katika *Kiu* na *Kidagaa kimemwozea*. Utafiti uliongozwa na mseto wa nadharia mbili – Uhalisia na Umuundo. Nadharia ya Uhalisia ilichangia katika kuangazia jamii jinsi ilivyo kwa ukamilifu wake nayo nadharia ya Umuundo ilichangia katika kusisitiza vipengele vya kazi ya sanaa kama vile msuko, uumbaji wa wahusika, mandhari na matumizi ya lugha. Aidha, ilibainisha uhusiano wa vipengele hivi katika kuikamilisha kazi ya kifasihi. Utafiti huu wa mkabala wa kithamano ulifanywa maktabani kwa kuzingatia muundo wa kiuchanganuzi. Eneo la utafiti huu lilikuwa ni fasihi andishi, hususan utanzu wa riwaya ya Kiswahili. Idadi lengwa ya utafiti ilikuwa ni riwaya 10 za kiuhalisia ambazo zinasawiri mandhari halisi. Sampuli ya riwaya mbili, *Kiu* na *Kidagaa Kimemwozea*, iliteuliwa kwa usampulishaji dhaminifu. Huu ni usampulishaji sinasibu ambapo sampuli huteuliwa kwa kuakisi sifa za kipekee zinazohitajika kwenye utafiti. Riwaya mbili zinazohusika ziliteuliwa kwa misingi ya wingi wa vifani vilivyochunguzwa, yaani usawiri wa mandhari. Pamoja na kuakisi malengo ya utafiti, utunzi wa riwaya teule uliambatana na mihimili ya mseto wa nadharia zilizoongoza utafiti. Data za utafiti zilikusanywa kwa njia ya usomaji makini. Huu ni usomaji wa kina wa matini kwa lengo la kupata uelewa wa ndani kuhusu matini inayosomwa na kuhakikiwa. Usomaji makini ulifanyika maktabani ambapo riwaya teule, vitabu, tasnifu na makala anuwai mkondoni zilihakikiwa. Data zilizokusanywa ziliainishwa kwa mujibu wa mihimili ya nadharia na malengo ya utafiti. Hatimaye, data ilichanganuliwa kwa mujibu wa yaliyomo na matokeo kuwasilishwa kimaelezo. Matokeo ya utafiti yanadhihirisha kwamba mandhari yana mchango wa moja kwa moja katika kuwasilisha ujumbe anuwai katika riwaya teule. Mandhari yana mchango katika kujenga sifa za wahusika na pia katika ukuzaji wa ploti za riwaya teule. Matokeo ya utafiti huu yana tija kwa taasisi za ukuzaji mitaala. Yatawasaidia kuweka mojawapo ya vigezo vitakavyoongoza uteuzi wa vitabu vya fasihi kwa ngazi mbalimbali. Mandhari yatatumika kama kigezo mojawapo katika maamuzi ya uteuzi. Vile vile, matokeo ya uchunguzi yatakuwa na faida kwa wanariwaya na waandishi wa kazi za kifasihi kwa jumla. Yatawasaidia kutunga visa vinavyosawiri na kuakisi mandhari kuntu. Isitoshe, wahakiki wa kazi za fasihi watawezeshwa kubaini, kutathmini na kuchanganua mandhari anuwai pamoja na dhima zao katika kazi za kifasihi.

# ABSTRACT

Setting is defined as the place and time where literary events take place in a particular text. The setting can be real or even imaginary. The main aim of this research was to examine the depiction of setting in the Kiswahili novel by focusing on Mohamed's *Kiu* as well as Ken Walibora's *Kidagaa Kimemwozea*. The study sought to achieve the following specific objectives: to identify the types of settings employed in conveying messages in *Kiu* and *Kidagaa Kimemwozea* novels, to evaluate the contribution of setting in developing the characters' traits in *Kiu* and *Kidagaa Kimemwozea* novels, as well as to explain the setting's contribution to the plot's development of the story in *Kiu* and *Kidagaa Kimemwozea*. This study was guided by a set of two theories – Realism and Structuralism. The Realism theory contributed to highlighting the society as it is in its entirety while Structuralism did so by stressing the artistic components of the work, namely: plot, the development of characters, setting and language use. Furthermore, it helped in determining the relationships of these elements in completing the literary work. The analytical research design was employed in the conduct of this library study. The area of this research was literature, particularly the genre of realist Kiswahili novel. The target population of the research were 10 novels that portray realistic settings. A sample of two novels, *Kiu* and *Kidagaa Kimemwozea*, was selected by the purposive sampling technique. This is a nonprobability sampling procedure where the sample is selected by reflecting on the unique characteristics required in the study. The two novels were selected based on the occurrence of research variables under investigation, that is, the depiction of realistic settings and their suitability to the objectives of the research. In addition, the composition of the selected novels is in line with the tenets of theories that guided the research. Data for the research were collected through close reading, which involved the selected novels, books, theses and various online sources. The collected data were sorted and classified in accordance with the theoretical framework and research objectives. Finally, it was analysed thematically and presented descriptively. The research findings confirmed that setting has direct contribution to the messages in the two novels, the development of characters' traits, as well as the development of plot in the two novels studied. These research findings will benefit curriculum development institutions in setting one of the criteria that can guide the selection of literature books at various levels. Setting can be used as one criterion in selection decisions. Correspondingly, the findings of this study will benefit novelists and literary artistes in general. It will help them compose works of art that depict and reflect suitable settings. Finally, literary critics will be empowered to identify, evaluate and analyse various settings together with their roles in literary works.

Mount Kenya University

## YALIYOMO


**UNGAMO NA IDHINI** .......... ii

**TABARUKU** .......... iii

**SHUKRANI** .......... iv

**IKISIRI** .......... v

**ABSTRACT** .......... vi

**SURA YA KWANZA** .......... 1

**MISINGI YA UTAFITI** .......... 1

**1.0 Utangulizi** .......... 1

**1.1 Usuli wa Utafiti** .......... 1

**1.2 Suala la Utafiti** .......... 6

**1.3 Malengo ya Utafiti** .......... 6

**1.4 Maswali ya Utafiti** .......... 7

**1.5 Misingi ya Uteuzi wa Mada** .......... 7

**1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti** .......... 8

**1.7 Umuhimu wa Utafiti** .......... 8

**1.8 Hitimisho** .......... 9

**SURA YA PILI** .......... 10

**MWAUO WA MAANDISHI** .......... 10

**2.0 Utangulizi** .......... 10

**2.1 Uainishaji wa Mandhari Yatumiwayo katika Fasihi** .......... 10

**2.2 Dhima ya Mandhari katika Ujenzi Sifa za Wahusika** .......... 13


Mount Kenya University

**2.3 Mchango wa Mandhari katika Ukuzaji wa Ploti** ........ 14

**2.4 Misingi ya Kinadharia** ........ 16

**2.4.1 Nadharia ya Uhalisia** ........ 16

**2.4.2 Nadharia ya Umuundo** ........ 17

**2.5 Hitimisho** ........ 19

SURA YA TATU ........ 20

MBINU ZA UTAFITI ........ 20

**3.0 Utangulizi** ........ 20

**3.1 Muundo wa Utafiti** ........ 20

**3.2 Eneo la Utafiti** ........ 20

**3.3 Idadi Lengwa** ........ 21

**3.4 Sampuli na Usampulishaji** ........ 22

**3.5 Njia za Ukusanyaji Data** ........ 22

**3.6 Uchanganuzi wa Data** ........ 23

**3.7 Uwasilishaji wa Matokeo** ........ 23

**3.8 Maadili ya Utafiti** ........ 24

**3.9 Hitimisho** ........ 24

SURA YA NNE ........ 25

UCHANGANUZI WA DATA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO ........ 25

**4.0 Utangulizi** ........ 25

**4.1 Matumizi ya Mandhari Kuwasilisha Ujumbe wa Riwaya** ........ 25

**4.1.1 Mandhari Yawasilishavyo Maudhui ya *Kidagaa Kimemwozea*** ........ 26

**4.1.1.1 Mto Kiberenge** ........ 26

Mount Kenya University

4.1.1.2 Sokomoko ... 29

4.1.1.3 Nyumbani kwa Mwalimu Majisifu ... 30

4.1.1.4 Kibanda cha Amani ... 32

4.1.1.5 Shuleni Ulitima ... 34

4.1.1.6 Kasri ya Mtemi Nasaba Bora ... 34

4.1.1.7 Uwanja wa Nasaba Bora ... 36

4.1.1.8 Barabara ... 37

4.1.1.9 Chumba Shuleni Nasaba Bora ... 38

4.1.1.10 Mandhari ya Seli ya Mtemi Nasaba Bora ... 39

4.1.1.11 Mandhari ya Ukumbi wa Mtemi Nasaba Bora ... 39

4.1.1.12 Mandhari ya Ukumbi Chuoni Mkokotoni ... 40

4.1.1.13 Chumba cha Kulala kwa Mtemi Nasaba Bora ... 41

4.1.1.14 Zahanati ya Nasaba Bora ... 42

4.1.1.15 Misitu ... 43

4.1.1.16 Barazani kwa Amani ... 43

4.1.1.17 Mandhari Kiwakati ... 44

4.1.2 Mandhari Yawasilishavyo Maudhui ya *Kiu* ... 45

4.1.2.1 Chumba cha Mwinyi ... 45

4.1.2.2 Benzi la Mwinyi ... 46

4.1.2.3 Makonde ... 46

4.1.2.4 Mtaa wa Selea ... 47

4.1.2.5 Nyumba ya Idi Vibyongoni ... 48

4.1.2.6 Mandhari ya Benki ... 49



Mount Kenya University

**4.1.2.7 Ukele** ... 50

**4.1.2.8 Mandhari Kiwakati** ... 50

**4.2 Mandhari Yajengavyo Sifa za Wahusika** ... 52

**4.2.1 Mandhari Yajengavyo Sifa za Wahusika kwenye *Kidagaa Kimemwozea*** ... 52

**4.2.1.1 Mtemi Nasaba Bora** ... 53

**4.2.1.2 Mwalimu Majisifu** ... 58

**4.2.1.3 Bi. Zuhura** ... 59

**4.2.1.4 DJ** ... 61

**4.2.1.5 Amani** ... 61

**4.2.1.6 Imani** ... 62

**4.2.1.7 Majununi** ... 63

**4.2.1.8 Wauguzi** ... 64

**4.2.1.9 Dora** ... 65

**4.2.1.10 Askari** ... 66

**4.2.1.11 Wafanyikazi wa Mtemi** ... 66

**4.2.1.12 Fao na Dadake** ... 67

**4.2.2 Mandhari Yajengavyo Sifa za Wahusika wa *Kiu*** ... 67

**4.2.2.1 Mzee Mwinyi** ... 68

**4.2.2.2 Idi** ... 69

**4.2.2.3 Bahati** ... 71

**4.2.2.4 Cheusi** ... 73

**4.2.2.5 Bi. Mvita** ... 74

**4.3 Mandhari Yanavyochangia Ukuzaji wa Ploti** ... 75



Mount Kenya University

4.3.1 Mandhari Yanavyochangia Ukuzaji wa Ploti ya *Kidagaa Kimemwozea*......... 75
4.3.1.1 Mto Kiberenge ........................................................................ 75
4.3.1.2 Sokomoko ............................................................................... 77
4.3.1.3 Kibanda cha Amani ................................................................ 78
4.3.1.4 Kwa Kina Fao .......................................................................... 81
4.3.1.5 Zahanati ya Nasaba Bora ........................................................ 81
4.3.1.6 Uwanja wa Nasaba Bora .......................................................... 82
4.3.1.7 Mandhari Kiwakati .................................................................. 83
4.3.2 Mandhari Yanavyochangia Ukuzaji wa Ploti ya *Kiu* ....................................... 83
4.3.2.1 Chumba cha Mzee Mwinyi ...................................................... 83
4.3.2.2 Chumbani kwa Kina Bahati ..................................................... 84
4.3.2.3 Vibyongoni ............................................................................. 86
4.3.2.4 Hospitalini .............................................................................. 87
4.3.2.5 Bahari ..................................................................................... 87
4.4 Hitimisho .............................................................................................. 88
SURA YA TANO ........................................................................................ 89
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ...................................... 89
5.0 Utangulizi ............................................................................................ 89
5.1 Muhtasari wa Tasnifu ............................................................................ 89
5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ......................................................... 91
5.2.1 Mandhari Yatumiwavyo Kuwasilisha Maudhui ya Riwaya ........................... 91
5.2.2 Mandhari Yachangiavyo Ujenzi wa Sifa za Wahusika katika Riwaya .......... 93
5.2.3 Mandhari Yachangiavyo Ukuzaji wa Ploti ya Riwaya .................................... 93



Mount Kenya University

**5.3 Hitimisho** ........ 94

**5.4 Mapendekezo** ........ 94

**5.4.1 Mapendekezo ya Utafiti** ........ 95

**5.4.2 Mapendekezo ya Tafiti za Baadaye** ........ 95

**MAREJELEO** ........ 96

**VIAMBATISHO** ........ 103

**KIAMBATISHO A: BARUA YA UTAMBULISHO** ........ 103

**KIAMBATISHO B: CHETI CHA IDHINI** ........ 104

**KIAMBATISHO C: IDHINI YA NACOSTI** ........ 105

**KIAMBATISHO D: KIZIO CHA MFANANO WA MATINI** ........ 107

Mount Kenya University

## SURA YA KWANZA

## MISINGI YA UTAFITI

### 1.0 Utangulizi.

Sura hii inajishughulisha na usuli wa utafiti, suala linalochunguzwa, malengo na maswali ya utafiti, misingi ya uteuzi wa mada, upeo na mipaka ya utafiti, pamoja na umuhimu wa kulitafitia suala lililochunguzwa.

### 1.1 Usuli wa Utafiti.

Fasihi hujengwa na vipengele mbalimbali vya fani, ikiwemo matumizi ya kipengele cha mandhari. Kipengele hiki ni muhimu katika uandishi wa fasihi na huwa kinachangia kwenye ujenzi na uwasilishaji wa ujumbe wa mwandishi. Kwa hivyo, mandhari ni kipengele cha sanaa ambacho mwanafasihi hukitumia kuwasilishia ujumbe wake kwa msomaji. Kipengele cha mandhari kimefafanuliwa na wataalamu mbalimbali. Mathalan, Wamitila (2008) anaeleza mandhari kuwa ni elementi inayomfichulia msomaji ni wapi na lini kadhia au matukio fulani yalitendeka. Mandhari yanaweza kuwa na uhalisia au yawe hayana uhalisia bali ni ya kidhahania. Mandhari ya uhalisia yanahusu mahali ambapo panapatikana katika ulimwengu halisi. Kwa mfano, mandhari ya msitu, chuoni, nyumbani, ofisini, mjini na maabadini. Mandhari ya kidhahania yanahusu mazingira yasiyo ya kawaida na mengi huonekana kupitia ruya. Mfano wa mandhari ya kidhahania ni peponi, kuzimu na jahanamu.

Kwa hivyo, kutokana na ufafanuzi wa Wamitila tunaweza fasili mandhari kuwa ni sehemu, mahali, eneo au hata hali ambapo kazi ya fasihi ilitendeka, inatendeka au itakapotendeka. Kazi ya fasihi yoyote ile, lazima iambatane na sehemu au mahali ambapo matukio hutendeka. Mandhari

yanahusishwa na wahusika, mbinu na maudhui inayowasilishwa kwenye tungo za kifasihi. Mandhari yana manufaa mengi katika tungo za kifasihi kwa sababu kupitia kwayo mivutano katika utungo wa kifasihi hujengeka. Mivutano hii hudhihirika miongoni mwa wahusika waliotumiwa kwenye masimulizi au riwaya katika mazingira fulani na wakati fulani. Mivutano hii ndiyo inayoibua maudhui ya kazi ya mwandishi anayehusika. Vilevile, mandhari humwezesha msomaji au mtazamaji kupata welewa, tajiriba, hisi pamoja na lengo analotazamia kuwasilisha mtunzi wa kazi ya kifasihi inayohusika. Kwa ujumla, mandhari huiwezesha hadhira kupata uzoefu wa yale anayotaka mtunzi kuwasilisha kwa wasomaji na jamii yake. Mtunzi aghalabu hutumia mandhari kuitoa hadhira yake kwenye ulimwengu wa kinjozi na kujaribu kuiweka kwenye ulimwengu halisi. Hadhira, kwa hali hiyo, huweza kupata taswira halisi inayohusiana na kazi ya mtunzi anayehusika.

Mandhari yamefafanuliwa pia kuwa ni mahali popote pale ambapo tendo la masimulizi hujiri (Mbatia, 2001). Eneo hili linaweza kuwa ni kiamboni, barabarani au mahali penginepo ambapo mtunzi aamuapo kupatumia kwa azma ya kuwasilisha ujumbe, kukuza sifa za wahusika wake na hata kuusuka utungo wake ili uakisi mantiki ya kifasihi inayofaa. Akiifasili istilahi mandhari, Wamitila (2003) anasema hili ni neno litumikalo kuelezea pahali pa matukio kwenye hadithi. Anaongezea kuwa mandhari huwa na dhima kubwa katika hadithi na hivyo basi msomaji anapaswa kubaini endapo kuna uhusiano wa mandhari na mbinu nyinginezo za utunzi, ikiwemo dhamira, maudhui, wahusika na hata lugha inavyotumiwa. Wamitila anasisitiza kwamba mandhari huweza kuwa ya kisiasa, kihistoria, kijamii, kijiografia na kadhalika. Katika tungo mbili zilizochunguzwa, aina mbili za mandhari zimebainika; nazo ni mandhari ya wakati na mandhari ya maeneo. Mandhari ya maeneo ndiyo yale Wamitila (2003) anayatambua kuwa ni mandhari ya kijiografia ilhali yale ya wakati ndiyo anayoyaeleza kuwa ni ya kihistoria.

Mandhari hujidhihirisha pia kama sehemu au kiambo mahsusi kilichojengwa na mtunzi panapotukia matendo mbalimbali ya fasihi (Njogu & Chimerah, 1999). Mandhari huwa ni mambo au hali inayozunguka wahusika na hivyo lazima pawe na matukio yanayohusu mahali hapo wanapokaa . Fasili hii inachimuza hali, maeneo na masaibu yanayowazingira wahusika mbalimbali katika kazi za kifasihi. Mathalan, mhusika Majununi katika *Kidagaa Kimemwozea*, anakataliwa na mchumba na hatimaye kuchukia wanawake wote duniani na kuishia kutooa maishani. Haya yanatendeka kwenye mandhari ya kasri lake baada ya kufanya juhudi nyingi za kujaribu kumfurahisha kwa kujenga hema, nyumba na hatimaye kasri.

Mandhari halisia hutoa udhuru kwa hadhira kugusia majira mbalimbali na maeneo tofauti ili kupata kuwaelewa vizuri wahusika, maeneo na hata nyakati nyingine (Erickson, 2018). Kwa hali hiyo, mandhari hufanikisha dhima aali kwenye kazi ya kifasihi; yaani huchochea. Uchochezi huu ndio hutoa suluhisho miongoni mwa wahusika wanaokumbwa na migogoro inayosababishwa na mandhari kwa kuhusisha mivutano hiyo na mandhari halisi. Mbali na hayo, mandhari hutekeleza dhima ya kitaashira kwa sababu wahusika, maeneo na matukio fulani huwasilisha maana fulani kwenye masimulizi. Hii ina maana kwamba mwandishi anaweza kutumia mandhari kuwasilisha ujumbe kwa njia iliyofichika ili msomaji aweze kuwa makini sana katika kung'amua anachowasilisha mtunzi kwa hadhira yake. Kwa mfano, mtunzi anaweza kutumia mandhari yenye jua linalochomoza kuwasilisha ujumbe wa mwamko mpya.

Mandhari aghalabu huwa tofauti baina ya hadithi moja na nyingine kwa sababu waandishi tofauti tofauti hutumia mandhari kwa dhamira mbalimbali kwenye kazi ya fasihi (Hunt, 2006). Watunzi husawiri mandhari kwa hisia, kuangalia, kusikiliza na milango mingine ya fahamu. Hata hivyo, mandhari yanaweza kutumiwa na watunzi kwa usanii mkubwa ili kuwasilisha ujumbe wao, kukuza sifa za wahusika na kuendeleza ploti zao kama inavyojadiliwa katika utafiti huu.



Mount Kenya University

Watunzi wa kazi za kifasihi wanapaswa kuwa waangalifu upande wa mavazi, makazi, vyakula na hata lugha kwa mujibu wa mila na desturi zinazoafiki (Bakize, 2014). Lengo hapa ni kufanikisha uwezo wa kueleza majira, hali na mahali ambamo masimulizi yanatukia. Ni kutokana na usuli huu ambapo wanariwaya kama vile Ken Walibora wanasawiri wahusika wao. Mathalan, mhusika DJ anadhihirishwa upenuni mwa Mto Kiberenge kama kijana anayetumia lugha ya mtaani, *Sheng*, ili kueleza kwamba katika jamii wapo vijana ambao hawamudu lugha rasmi ya Kiswahili bali wameibuka na lugha mbadala kwa lengo la kuwasiliana katika mazingira yao. Vilevile, mavazi yake mararu marau yanatumika kuibua suala la umaskini linalowasakama baadhi ya wanajamii kwenye jumuiya ya *Kidagaa Kimemwozea*.

Taswira na usimulizi huibuliwa na wanafasihi ili kumchorea msomaji picha ya mandhari ambayo humsaidia kuielewa kazi inayohusika vizuri (Fang, 1996). Msanii anao wajibu wa kuisawiri picha dhahiri ya mandhari akijitahidi kuhusisha uhalisia wake, hata kama mandhari yenyewe ni ya kidhahania. Mfano hapa ni mandhari ya mbinguni anayozungumzia Mtemi Nasaba Bora akiwa nyumbani kwa nduguye Mwalimu Majisifu. Kwa mujibu wa maelezo yake kuyahusu mandhari haya na wanaoenda huko, mwandishi anachora uhalisia fulani unaoelezwa kwenye madhehebu mbalimbali ya kidini. Kwamba wenye dhambi hawataingia huko ingawa haya mandhari ni dhahania.

Mtunzi wa kazi ya fasihi anapoteua mandhari, sharti masimulizi yake yafungamane na ukweli wa eneo na wakati unaohusika (Oyoo, 2003). Mandhari dhahiri kwa hadhira huchangia katika usawiri wa picha akilini. Udhihirishaji mzuri wa mandhari humsaidia mwanariwaya kuibua mitazamo chanya miongoni mwa hadhira yake na kuwafanya watake kuisoma kazi inayohusika. Mtunzi anavyosuka kazi yake huwa na athari kwa wasomaji kwa sababu ya vipengee mbalimbali vilivyotumika.



Mount Kenya University

Pamoja na kuangazia mandhari na usawiri wa vipengele kama vile maudhui, fani na matumizi ya lugha kwa ujumla wake, utafiti uliofanywa awali umekitwa kwenye tanzu tofauti za fasihi kama vile tamthilia, ushairi, hadithi fupi na novela. Hata hivyo, utafiti huu unaangazia riwaya teule za Kiswahili zisizohakikiwa kwa upande wa mandhari na jinsi yanavyokuza sifa za wahusika, ujumbe wa mwandishi pamoja na ujenzi wa ploti ya hadithi inayosimuliwa. Akiongozwa na mseto wa nadharia ya Umtindo pamoja na Finominolojia kuchunguza usawiri wa mandhari katika hadithi fupi teule, Mbithi (2021) anafafanua jinsi mandhari husawiri maudhui, wahusika na matumizi ya lugha. Pamoja na kujikikita kwenye misingi ya kinadharia na utunzi wa fasihi tofauti, wahusika wanaochunguzwa na Mbithi wanadokezwa tu pasipo kuviringwa kwa uketo na uchangamani utokanao na ufafanuzi wa mandhari katika riwaya ya kihalisia; jambo lililochunguzwa katika utafiti huu. Isitoshe, nafasi ya mandhari katika ujenzi wa ploti haishughulikiwi.

Kwa hivyo, utafiti huu ulichunguza usawiri wa mandhari katika riwaya za Kiswahili teule za *Kidagaa Kimemwozea* yake Ken Walibora na *Kiu* iliyotungwa na Mohamed S. Mohamed ili kubaini jinsi ambavyo aina mbalimbali za mandhari zilivyochangia katika uwasilishaji wa jumbe za hawa waandishi. Aidha, jaribio lilifanywa kubaini jinsi ambavyo mandhari mbalimbali yalichangia katika ujenzi wa sifa mbalimbali za wahusika katika riwaya hizi. Hatimaye, dhima ya mandhari katika ukuzaji wa ploti ya riwaya hizi mbili zilibainishwa. Uchunguzi wenyewe umeegemezwa kwenye fasihi andishi, hususan utanzu wa riwaya ya kihalisia ya Kiswahili bali si utanzu wowote mwingine wa fasihi.

### 1.2 Suala la Utafiti.

Mandhari anayochorewa msomaji husalia akilini mwake. Waandishi wengi wanapotunga kazi zao huziweka katika mandhari tofauti tofauti kwa sababu ya kutosheleza mambo mbalimbali kifasihi



Mount Kenya University

na kisanaa. Mandhari huathiri mtazamo wa msomaji kwa njia nyingi ikiwemo kumpa taswira anuwai ya yale ambayo mwandishi alikusudia kuyawasilisha. Taswira hizi zinaweza kuwa kama vile: taswira oni, inayompa uwezo wa ‘kuona’ kile ambacho mwandishi anamchorea kwa maneno, taswira mwendo ambayo itamsaidia kupata tukio ‘kimwendo’, kwa mujibu wa mandhari ambamo tukio linatokea, taswira hisi ambapo atapata hisia mbalimbali za wahusika katika eneo la tungo jinsi mwandishi alivyochimuza hisia hizo, taswira mwonjo, ambayo msomaji huipata katika mandhari ambamo kitendo au vitendo vinavyoibua hisia ya kutonesha mate huibuliwa na nyingine nyingi kama vile taswira sikivu. Kwa hali hiyo, mandhari kwa njia zozote zile hufanya kazi kubwa katika tungo za fasihi, ikiwemo riwaya. Inajuzu kusema kwamba mandhari ni mhimili mkuu katika tungo za kisanaa. Ni kutokana na sababu hizi ambapo utafiti huu ulipania kuchunguza uhusiano uliopo kati ya mandhari na ujenzi wa sifa za wahusika mbalimbali; jinsi ambavyo mandhari yalivyochangia katika uwasilishaji wa ujumbe katika tungo hizi na hatimaye kubaini jinsi mandhari yalivyochangia ukuzaji wa ploti kwenye tungo za *Kidagaa Kimemwozea* na *Kiu*.

## 1.3 Malengo ya Utafiti.

Azma ya huu utafiti ilikuwa ni kuchunguza usawiri wa mandhari kwenye riwaya ya *Kiu* na *Kidagaa Kimemwozea* ili kubainisha uhusiano uliopo kati ya mandhari na sifa za wahusika, mandhari na uwasilishaji wa ujumbe, pamoja na uhusiano uliopo kati ya mandhari na uendelezaji wa ploti. Utafiti wenyewe ulinuiwa kuyafikia malengo mahsusi yafuatayo:

i) Kubainisha aina za mandhari yaliyotumiwa kuwasilisha ujumbe katika riwaya ya *Kiu* na *Kidagaa Kimemwozea*.

ii) Kutathmini mchango wa mandhari katika ujenzi wa sifa za wahusika katika riwaya ya *Kiu* na *Kidagaa Kimemwozea*.

iii) Kueleza mandhari yanavyochangia ukuzaji wa ploti kwenye riwaya ya *Kiu* na *Kidagaa Kimemwozea.*

## 1.4 Maswali ya Utafiti.

Huu utafiti ulilenga kuyajibu haya maswali:

i) Aina zipi za mandhari zitumiwazo kuwasilisha ujumbe katika riwaya ya *Kiu* na *Kidagaa Kimemwozea*?

ii) Mandhari yanachangiaje ujenzi wa sifa za wahusika katika riwaya ya *Kiu* na *Kidagaa Kimemwozea*?

iii) Mandhari yanachangiaje ukuzaji wa ploti katika riwaya ya *Kiu* na *Kidagaa Kimemwozea*?

## 1.5 Misingi ya Uteuzi wa Mada.

Uteuzi wa mada hii ulifanywa kwa misingi kwamba mandhari aghalabu huwa na ushawishi mkubwa kwa mwitiko wa ujumbe unaowasilishwa kwa hadhira. Hii ni kwa sababu mandhari hufanya kazi nyingi katika utungo fulani. Mandhari huwa muhimu kwa sababu ndipo pahali ambapo msanii huwatengea wahusika wake kwenye utunzi ili hadhira yake iweze kutambua wako wapi, ni kina nani na mbona wako waliko (Msacky, 2015). Kwa hali hii mtunzi huwezeshwa kuyasawiri mandhari yake kwa njia fulani kwa lengo la kuwasilisha ujumbe fulani kwa hadhira lengwa.

Vilevile, hii mada iliteuliwa kwa ufahamu kwamba mageuzi katika jamii huathiri jinsi mandhari husawiriwa pamoja na jinsi yanavyoingiliana na wahusika, sifa zao pamoja na maudhui. mbali na kuwakilisha vipindi tofauti vya utunzi, riwaya teule - *Kiu* (Mohamed, 1972) na *Kidagaa Kimemwozea* (Walibora, 2012), zinasawiri mandhari mbalimbali kwa kina na uchangamani

Mount Kenya University

unaoafiki malengo ya utafiti. Isitoshe, mandhari yanathibitika kuwa ni nyenzo muhimu katika uendelezaji wa ploti katika kazi nyingi za fasihi andishi.

### 1.6 Upeo na Mipaka ya Utafiti.

Utafiti huu ulichunguza usawiri wa mandhari kwenye riwaya teule mbili ambazo ni: *Kidagaa Kimemwozea* na *Kiu*. Ulijikita katika kubaini mwingiliano wa mandhari na wahusika pamoja na sifa zao. Aidha, mchango wa mandhari katika uwasilishaji wa ujumbe katika hizi tungo mbili umefafanuliwa pamoja na jinsi ambavyo mandhari yayo hayo yachangiavyo ujenzi wa ploti za riwaya hizi mbili.

Utafiti huu ulikuwa wa muundo wa kiuchanganuzi ambao ulijikita katika fasihi andishi, hususan riwaya mbili teule, Idadi lengwa ilikuwa riwaya kumi ya riwaya za kiuhalisia, usampulishaji ulifanywa kupitia usampulishaji dhaminifu ambao ulifanywa kwa msingi wa sifa bainifu za kipekee ambazo sampuli hizo mbili (*Kiu na Kidagaa Kimemwozea*) zilikuwa nazo na zilifaa zaidi katika utafiti. Data zilikusanywa kwa njia ya usomaji makini wa kazi hizi mbili zote kikamilifu, uchanganuzi wa data ulifanywa kwa mujibu wa matokeo yaliyopatikana na matokeo kuwasilishwa kwa njia ya maelezo.

Mount Kenya University

### 1.7 Umuhimu wa Utafiti.

Matokeo ya huu utafiti yanatarajiwa kuwasaidia wahakiki na watunzi wa kazi za fasihi kutambua aina mbalimbali za mandhari na jinsi ambavyo zinavyochangia katika kukuza ploti za kazi za fasihi andishi. Inatarajiwa kwamba matokeo ya utafiti huu yatasaidia kubainisha uhusiano uliopo kati ya mandhari na ujenzi wa sifa mbalimbali za wahusika pamoja na jinsi ambavyo mandhari huchangia katika uwasilishaji wa ujumbe kwenye utanzu wa riwaya.

### 1.8 Hitimisho.

Sura hii imeangazia mambo muhimu yanayouwekea utafiti huu msingi wake. Imeangazia vipengele vinavyoufafanua usuli, suala lililochunguzwa, madhumuni na maswali ya utafiti, misingi iliyozingatiwa katika uteuzi wa mada pamoja na umuhimu wa uchunguzi wenyewe. Sura ifuatayo inahakiki maandishi yanayohusiana na uwakilishaji wa mandhari katika kazi za kifasihi.

Mount Kenya University

## SURA YA PILI

## MWAUO WA MAANDISHI

### 2.0 Utangulizi.

Sura hii inajishughulisha na uhakiki wa masuala mbalimbali yaliyochunguzwa na kuandikwa na watafiti wengine kuhusiana na usawiri wa mandhari katika kazi za fasihi. Nia ni kuuwekea msingi utafiti uliofanywa. Kwa hivyo, sura hii inahakiki maandishi yanayoangazia dhima ya mandhari katika ukuzaji wa ploti, ujenzi wa wahusika pamoja na uainishaji wa mandhari mbalimbali na michango yao katika fasihi, hususan katika kuibua jumbe mbalimbali katika tungo za kifasihi.

### 2.1 Uainishaji wa Mandhari Yatumiwayo katika Fasihi.

Wamitila (2003) anasema kuwa ikiwa mandhari fulani yana umuhimu mkubwa katika hadithi, basi yanaweza yakaelezwa kwa urefu kidogo. Hata hivyo, mwandishi yuko radhi kuyadokeza tu kwa maneno machache. Kwa hali hiyo, mandhari yanapochunguzwa, hutokana na utambuzi kwamba kila jambo au tukio hutendeka mahali fulani palipojengwa na msanii. Mahali penyewe ni pale panapotukia tukio au matukio kadhaa ya kazi ya utunzi wa kifasihi. Hii ina maana kwamba uanishaji wa mandhari aghalabu huangazia wakati na eneo au mahali panapojiri matukio yasimuliwayo. Ukweli huu unajitokeza pia katika kazi hizi zilizotafitiwa. Kwa mfano, kwenye *Kidagaa Kimemwozea*, mwandishi anatuakisia matukio yaliyotendeka enzi za Vita Vikuu Vya Dunia, enzi za kikoloni na harakati za mapambano kutaka uhuru katika nchi huru ya Tomoko.

Hoja hii pia ilishadidiwa na Njogu & Chimerah (2008) wanaoeleza kwamba mandhari huwa ni mambo au hali inayowazunguka wahusika. Kwa hivyo, lazima mahali panapohusika pahusishwe na matukio yanayosimuliwa. Mandhari ni mahali mahususi wanapokaa wahusika pamoja na

Mount Kenya University

mitagusano au migogoro baina yao. Matukio yanayojiri mahali na wakati fulani yanaweza yakawa ya kijamii, kiuchumi au hata kisiasa. Mandhari pia huakisi nafasi za wahusika kitabaka. Kwa mfano Mtemi Nasaba Bora alikuwa Mtemi wa Sokomoko. Maelezo ya wataalamu hawa yanachimuza umuhimu wa kuainisha mandhari kwa msingi wa wakati na mahali au mazingira; jambo lililoshughulikiwa katika uchunguzi huu kwa kurejelea riwaya teule zilizofanyiwa uchunguzi hapa. Ikadhihirika kwamba mandhari ya maeneo na wakati ndiyo yaliyotumika zaidi kwenye tungo hizi.

Haya maoni yanaafikiwa pia na Sengo (2009) ambaye anasema kuwa mandhari ni sehemu ambapo mtunzi ameteua katika kazi yake kwa minajili ya kufahamisha shughuli mbalimbali za kijamii kama vile uongozi na matendo hasi kama ukabila, utabaka, ubaguzi na mengine mengi. Kupangwa kwa njama ya mauaji ya babu yake Amani (Chichiri Hamadi) na Mtemi Nasaba Bora na hatimaye kuuliwa alipopokelewa katika uwanja wa ndege na mwanawe Yusuf Hamadi, ni thibitisho la dai lake Sengo (2009) kuhusu mandhari na wajibu wake kuhusu shughuli hasi katika jamii kwenye riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea.*

Naye Ntiba (2011) anasema kuwa, maana ya kifasihi inaweza kutazamwa kwa kuchunguza mazingira ya msomaji, mwandishi au andiko lenyewe na jinsi andiko hilo linavyofasiliwa na anayelisoma au kulisikiliza.

Omondi (2011) naye anaeleza kwamba mandhari ni eneo lililojaa ati ati nyingi na shughuli za kisiasa pamoja na uongozi. Ni kupitia maoni haya ndipo waandishi wengi huibuka na utunzi ambao unalenga maudhui zinazofungamana na siasa na utawala, mifumo ya ubepari, ukiritimba na usosholisti na mengine mengi. Wazo hili linajitokeza wazi kwenye *Kidagaa Kimemwozea* ambapo suala la utawala wa kikoloni linaangaziwa.

Joyce (2011) naye anaeleza mandhari kuwa ni mahali panapomrahisishia anayesoma kazi ya mtunzi na kumfanya kupata uelewa wa malengo ya mtunzi anayehusika, jumbe zake na hata kupata picha kamili ya anayodhamiria.

Mandhari vile vile yanaweza ainishwa kwa mujibu wa wakati, hiki ni kipindi ambacho tukio lilitendeka. Kwa mujibu wa Matei (2011) mandhari ni mahali na wakati ambapo sanaa ya fasihi hutendwa. Zipo nyakati nyingi ambazo zimetumika katika riwaya hizi mbili kama vile enzi za kikoloni, vita vikuu vya Dunia ya pili kwenye *Kidagaa Kimemwozea* na hata miaka ambayo mhusika Bahati walimaliza katika ndoa kisha mateso yakaanza kumwandama, kwa mujibu wa *kiu*. Mandhari haya yote yalichunguzwa na kuwekwa chini ya migao miwili mikuu; ya maeneo na wakati.

Mbithi (2013) anaeleza kuwa usawiri wa mandhari ni kigezo muhimu katika ukadiriaji wa ubora wa kazi yoyote ile ya fasihi. Kigezo hiki huweza kutumiwa na vingine katika tungo za fasihi ili kuwasilisha ujumbe wa mwandishi. Utunzi wa kazi zilizochunguzwa unashadidia wazo la Mbithi kwa sababu unatumia mandhari kuwasilisha jumbe mbalimbali. Kwa mfano, mhusika Mwinyi kwenye *Kiu* ameonyeshwa akiwa ametundika picha ya mwanamke aliyekuwa uchi kwenye moja ya kuta za nyumba yake. Baadaye, Mzee huyu anatumiwa na mwandishi kuendeleza maudhui ya mapenzi.

Kwa upande wake, Mpalanzi (2020) anaeleza kuwa mandhari ni kama pahali asilia ambapo masuala mengi katika jamii hufanywa au kutokea. Ni kupitia maoni haya ndipo waandishi wengi hujaribu kutunga kazi ambazo huakisi mazingira yanayofahamika na wasomaji huku wakijaribu pia kusuka matendo yao na mahali wanamoishi kwa nia ya kudhihirisha ukweli ulivyo katika jamii. Masuala kama vile,wahusika Bahati na Idi kwenye *Kiu* kuishi kwenye mitaa yanadhihirisha ukweli

kwani katika hali ya kawaida kuna mitaa mingi ambamo wanajamii huishi. Kuelezwa kwamba baba yake Imani (Mtembezi) alinunua shamba Baraka ni jambo la kihalisia kwa sababu ununuzi wa mashamba ni jambo la kawaida katika jamii zetu.

Utafiti huu ulichunguza mandhari kwa kuyashikilia maana kuwa ni mahali na wakati ambao tukio au matukio hutendeka katika tungo za sanaa. Mandhari haya ya mahali (kigiografia) na mandhari ya kiwakati (kihistoria) yaliteuliwa kwa vile waandishi wa riwaya hizi teule walitumia mandhari haya mawili kwa ustadi na ubunifu mkubwa, zaidi ya hayo, mawanda ya mandhari haya yalikuzwa kikamilifu kwa hivyo kuchangia pakubwa katika ukusanyaji wa data kwenye utafiti wenyewe.

## 2.2 Dhima ya Mandhari katika Ujenzi Sifa za Wahusika.

Wamitila (2002) anasema kwamba mandhari huwa na michango maridhawa katika kusawiri wahusika kisifa, anaeleza kwamba kwa kiasi kikubwa wahusika huathiriwa na mazingira ambamo wamo. Hili dai la Wamitila lilijitokeza katika huu utafiti. Tukichukulia mfano wa eneo la Selea ambalo liko kwenye riwaya ya *Kiu* tunaelezwa na mwandishi kwamba lilikuwa ni eneo (mandhari) ambalo lilikuwa na umaskini mwingi, shida nazo zilikuwa kemkem, wenyeji waliishi kwenye vibanda na wengine vyumba vilivyokandikwa kwa udongo, barabara yenyewe ya kufikia huko ilikuwa mbovu kiasi kwamba hata gari la Mwinyi halingefikia. Wahusika kama Bahati na Mamake Chausiku walioishi katika mtaa huu walikuwa maskini vilevile. Hii ina maana kuwa mazingira yale yalikuwa na athari ya moja kwa moja kwa hawa wahusika na sifa zao. Walikuwa maskini ndiyo maana wakaishi pale.

Wamitila (2002) anaendelea kueleza kuwa mandhari yanafahamisha kuhusu safari ya mhusika kuanzia mwanzo wake hadi mwisho kwenye hadithi. Kwa hivyo, msomaji hupata kumwelewa mhusika katika kila eneo kisifa katika kila hatua. Mfano mzuri ni wa mhusika Mwalimu Majisfu

kwenye riwaya *Kidagaa Kimemwozea* ambaye tunaambiwa kuhusu utoto wake, kusoma kwake hadi ng'ambo, kuingilia ulevi na kushindwa kuhudhuria vipindi vyake shuleni Nasaba Bora, kuachishwa kazi na kupata nyingine, kuingilia wizi wa miswada ya waandishi na kushindwa kutoa mihadhara alipoalikwa Wangwani. Hapa inatupatia sifa kadhaa za huyu mhusika kupitia mandhari mbalimbali kwamba alikuwa msomi, mlevi, mwizi wa taaluma na mtepetevu kazini.

Ili kusawiri mhusika kwa njia fulani jambo la msingi ni kuchunguza mandhari alimo (Wamitila, 2008). Dai hili liliafikiwa na huu utafiti pale ambapo mhusika kama Majununi aliangaziwa sifa zake kwenye riwaya *Kidagaa Kimemwozea,* tulipata kwamba mhusika huyu alitumiwa na mwandishi ili kutujuza kuhusu kipindi fulani cha kihistoria ambacho ni Vita Vikuu Vya Dunia vya Pili na kwamba Majununi alikuwa miongoni mwa wanajeshi wa Uingereza waliopigana katika vita hivi, watu wengi wakafa katika uwanja wa vita lakini yeye akaponea. Kwa kusawiriwa vile, moja kwa moja inatusaidia kubaini kwamba alikuwa jasiri kwa vile ujasiri ndicho kigezo cha kukubali kuingia vitani. Hivyo, basi asemavyo Wamitila (2008) kila mhusika hupata sifa zinazooana na mandhari alimo ni madai ya kweli na yalisaidia katika kupata jibu la swali la utafiti kwamba mandhari huchangia katika kukuza sifa za wahusika.

Kwa hivyo, tukichunguza baadhi ya fasiri za wataalamu hawa tunapata kwamba walijikita katika mandhari ya maeneo na wakati katika fasiri zao. Fasiri ambazo zilichangia pakubwa katika utafiti huu kwa maana utafiti wenyewe ulichunguza mandhari kwa kuegemea katika dhana kwamba mandhari ni wakati na mahali ambapo matukio ya kisanii hutendeka.

### 2.3 Mchango wa Mandhari katika Ukuzaji wa Ploti.

Rowe (1939) anasema kuwa ploti ni kufululizika kwa matukio yaliyopangwa kiasi kwamba yataweza kuteka nathari ya wasomaji kwa vile yanaibua taharuki. Msuko katika masimulizi



Mount Kenya University

hutusaidia kuanzisha ukurasa mpya wa masimulizi tukiwa na lengo la kutaka kujua yaliyotokea hatimaye. Baada ya misukosuko ya ndoa kati ya Bahati na mumewe na hatimaye Bahati kuamua kurudi kwao Selea, alipokea barua kutoka kwa mumewe Idi ili wakutane Kinarani, hadithi inamalizikia pale Cheusi akihangaika kumtafuta mwanawe Bahati ambaye alichelewa kurudi nyumbani. Kwa kweli tunabaki katika taharuki kuhusu hatima yake. Haya ni kwa mujibu wa *Kiu.*

Nao Symbo na Mazrui (1992) wanaeleza ploti kuwa ni kule kufuatana kwa matukio ili kujenga utunzi wa msani. Wanasema kuwa ususi huu wa vitushi katika masimulizi lazima ulenge uendelezaji wa hadithi ndipo upate kutambuliwa kama ploti. Kwa kutajiwa kuhusu mambo ambayo yalitendeka enzi za ukoloni licha ya kwamba mtunzi alikuwa akizungumzia Tomoko huru kwenye masimulizi yake, lengo lilikuwa kuendeleza ploti ya hadithi kwenye *Kidagaa Kimemwozea* (Wamitila, 2003; Symbo & Mazrui, 1992).

Wamitila (2003) anasema kwamba matukio yajengayo masimulizi ni ploti. Kwa kuegemea kwenye fasiri hizi za wasomi mbalimbali ni vyema kusema kwamba mandhari huwa na mchango mkubwa katika msuko wa hadithi kwa sababu, kwa mfano tukichukulia riwaya teule ya *Kidagaa Kimemwozea* tunapata wahusika kwa jina Amani na Imani ambao wanasafiri kutoka maeneo (mandhari) mbalimbali, Ulitima na Baraka mtawalia, kisha kujipata kando ya Ziwa Mawewa halafu kufunga safari pamoja mpaka Sokomoko. Malengo yao yakiwa kuwajua waliowapoka mali ya familia zao, waliamini kwamba aliyewafanyia haya alikuwa akitoka eneo hili. Safari hii ya wahusika hawa kupitia mandhari tofauti tofauti mpaka Sokomoko imechangia pakubwa katika kuendeleza ploti ya hadithi kupitia motifu ya safari.

Mount Kenya University

## 2.4 Misingi ya Kinadharia.

Utafiti huu uliongozwa na mseto wa nadharia mbili. Yaani, Nadharia ya Uhalisia na nadharia ya Umuundo.

### 2.4.1 Nadharia ya Uhalisia.

Nadharia ya Uhalisia ilichipuka kunako karne ya kumi na tisa (Ntaragwi, 2004). Istilahi 'uhalisia' ni tafsiri la neno la Kiingereza *'realism'* lililotumiwa awali kurejelea tawi la falsafa linalojihusisha na masuala yanayohusika na milango ya fahamu ya binadamu. Hivi sasa neno hili linatumiwa kurejelea fahiwa mbili, ya kwanza ikiwa ni ile inayotathmini hali ya maisha, yaani hali halisi ya fasihi inayoashiria kipawa cha utunzi na kuelezea matukio kwa mujibu wa ukweli; na fahiwa ya pili ikiwa hali halisi ya maisha ya binadamu.

Kwa mujibu wa Mbatia (2001) uhalisia ni neno linalorejelewa kama mbinu ya utunzi ambayo inajiegemeza sana sana na uibuaji wa picha kamili ya maisha ya binadamu au watu kwa njia fahamivu kwenye jamii wanamoishi. Naye Lukacs (1963) anasema kwamba katika uhalisia, mtunzi husukumwa zaidi ili atunge tungo ambazo zitaakisi ukweli kikamilifu na majira kamili tena maalumu. Matukio, wahusika na hata mazingira huchukuliwa kuwa ni ya kuakisi ukweli au hali halisi ikiwa kuna mfanano na hali halisi ya maisha ya binadamu. Hata hivyo, Wamitila (2003) anaitumia istilahi uhalisia kwa njia mahsusi zaidi kuzifafanua tungo za fasihi ambazo zinasawiri ulimwengu au mbari ambamo wanajamii wanatenda masuala yao jinsi wanavyochochewa na mazingira waliomo kwa uhalisia wake.

Ni kupitia fasiri mbalimbali za wataalamu hawa ndipo utafiti wetu uliongozwa na mitazamo yao katika riwaya hizi mbili nasi kushikilia kwamba uhalisia tunaouchunguza uwe ni jinsi ambavyo kila mtunzi alivyojaribu kusuka matukio yake kwa kuakisi ukweli uliopo katika jamii. Riwaya hizi

mbili ziliibuka kuwa ndizo zilitujengea taswira za kikweli au hali halisi zaidi kwa mapana na marefu na zilitufaa katika uchanganuzi wa data ambazo tulikuwa tukichunguza.

Kwa mujibu wa Ntaragwi (2004) nadharia ya Uhalisia ina mihimili ifuatayo:

a) Waandishi na wahakiki wa kiuhalisia wanachukulia kwamba jukumu la mtunzi liwe kusawiri ukweli unavyojitokeza katika jamii husika.

b) Wanauhalisia waliamini kuwa mwandishi alihitajika kutoa picha kamili ya jamii yake jinsi ilivyo bila kuidunisha wala kuipigia chuku.

c) Wahakiki walimtathmini mwandishi kwa namna ambavyo alijitahidi kusawiri matukio halisi katika kazi yake.

d) Wanauhalisia walitambua jukumu la mwandishi anayezingatia uhalisia kwa kuchagua, kuchanganua na kutenganisha mambo anayotaka kuyazungumzia ili kuonyesha ukweli jinsi ulivyo katika jamii.

Kupitia kwa mhimili wa pili wa nadharia ya uhalisia,utafiti huu ulichunguza jinsi waandishi wa vitabu hivi teule walivyosawiri hali halisi katika tungo zao kupitia mandhari mbalimbali walizotumia ili kutuwezesha kubaini baadhi ya jumbe zilizopaswa kupitishwa kwa hadhira lengwa hivyo basi kutusaidia katika kuafiki lengo la pili la huu utafiti.

### 2.4.2 Nadharia ya Umuundo.

Nadharia ya Umuundo aghalabu huhusishwa na wanaisimu wa Prague (Mwangi, 2005). Inasisitiza vipengele vya kazi ya sanaa kama vile msuko, ujumbe, wahusika, muktadha, lugha na jinsi ambavyo vinahusiana hadi kuikamilisha kazi inayohusika. Nadharia hii inachunguza uhusiano uliopo baina ya vipengee vingi vya tungo za fasihi kama vile uhakiki wa usimulizi kimuundo.



Mount Kenya University

Nadharia hii huzingatia usimulizi wa kazi ya sanaa. Kwa mfano, uhakiki wa riwaya kimuundo huzingatia riwaya kama kazi inayojitosheleza na iliyo na vipengele vya kimuundo kama vile msuko, wahusika na mbinu mbalimbali za usimulizi ambazo huingiliana na kutegemeana.

Waasisi wa nadharia hii kama vile Feinand De Saussure kwenye kitabu chake *A course in General linguistics* (1915). Anaamini kuwa lugha hutumiwa kama muundo wenye vipengele kadhaa ndani yake. De Saussure alitumia taratibu za kiisimu alizoziita *langage*, *langue* na *parole*, hizi alizieleza hivi: *parole* kurejelea ubinafsi wa kutumia lugha katika hali halisi, *langue* ikiwa ni lugha jinsi inavyotumika na wazawa na *langage* jumla ya ishara zinazotumika na wanadamu.

Ni kupitia ufahamu huu wa kiisimu ambao wanafasihi hutumia wanapotunga kazi zao ili kusuka ploti zao vilivyo na zenye mantiki kwa wasomaji wao. Ujuzi huo vile vile huwasaidia katika uteuzi wa fani zifaazo na wahusika katika tungo zao.

Mihimili ya nadharia ya Umuundo ni pamoja na:

a) Kazi yoyote ya fasihi ina muundo unaojitosheleza ulio na sehemu mbalimbali zinazohusiana na kuungana ili kuunda mfumo mmoja mkamilifu (ploti).

b) Wamamuundo wanaeleza kuwa kazi maalum za fasihi zizingatiwe kwa mfano, matumizi ya lugha yanayomlenga mtu binafsi na yanayotegemea sheria za mfumo wa lugha ya fasihi na lugha kwa jumla.

Kwa hivyo, mhimili wa kwanza wa nadharia ya Umuundo ulitusaidia kubaini jinsi mandhari yanavyochangia kuibua vipengele muhimu vya ploti pamoja na sifa za wahusika mbalimbali katika riwaya teule zilizochambuliwa.

Mount Kenya University

Kwa ujumla, mseto wa nadharia hizi mbili, Uhalisia na Umuundo, ulichangia katika uchambuzi wa riwaya teule: *Kidagaa Kimemwozea* na *Kiu.* na kusaidia kuyafikia malengo mahususi ya utafiti pamoja na kuyatafutia majibu maswali ya utafiti.

**2.5 Hitimisho.**

Kwa kifupi, sura hii ya pili ya utafiti ilibaini masuala mbalimbali katika utafiti huu ikiwemo uanishaji wa mandhari yatumiwayo katika fasihi, dhima ya mandhari katika ujenzi wa wahusika mbalimbali, michango ya mandhari katika ukuzaji wa ploti na msingi wa kinadharia ambao uliongoza utafiti wetu. Zaidi ya hayo ilibainika wazi kwamba baadhi ya tafiti za awali zilijikita katika tanzu nyingine za fasihi kama vile tamthilia, ushairi na hadithi fupi pengo likabaki upande wa riwaya ambalo huu utafiti ulijaza kikamilifu.

Mount Kenya University

## SURA YA TATU

## MBINU ZA UTAFITI

### 3.0 Utangulizi.

Sura hii inajihusisha na masuala yanayohusiana mbinu zilizofanikisha uchunguzi huu, yakiwemo: muundo, eneo pamoja na idadi inayolengwa katika utafiti huu. Mengine yanayoshughulikiwa ni sampuli na usampulishaji, njia za utafiti, vifaa vya kukusanyia data, uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa matokeo pamoja na maadili ya utafiti.

### 3.1 Muundo wa Utafiti.

Utafiti huu wenye mkabala wa kithamano ulijikita katika muundo wa utafiti wa kiuchanganuzi. Kwa mujibu wa Stephen na wenzie (1987) utafiti wa kiuchanganuzi huchunguza kwa undani vibadiliki ili kufikia uamuzi ufaao. Muundo huu ulituwezesha kukusanya, kuchambua na kueleza matokeo kwa mujibu wa yale yaliyotokana na utafiti huu hivyo basi kutusaidia kufikia uamuzi ufaao. Kwa hivyo, data ilikusanywa kwenye riwaya zilizoteuliwa, kuchambulia na kufafanuliwa ili kufanikisha malengo ya utafiti.

### 3.2 Eneo la Utafiti.

Huu ni utafiti wenye mwegemeo katika fasihi andishi, hususan utanzu wa riwaya ya kiuhalisia ya Kiswahili. Kwa mujibu wa Senkoro (2011) riwaya ni masimulizi ambayo yana urefu ambao unauruhusu utambe na zaidi ya hayo utambe jinsi mwandishi wa kazi hiyo anavyopenda akiangazia vizingiti kadhaa vinavyopatikana maishani. Senkoro anaongezea kwamba riwaya ni masimulizi marefu yenye kubuniwa na kwamba yana visa kadhaa. Murray (1978) pamoja na Wamitila (2003) wana maoni kwamba riwaya ni kazi ya fasihi andishi ambayo urefu wake

umeshinda ule wa hadithi fupi. Urefu hapa wakimaanisha ususi wa vitushi vyake umejengwa vizuri kwa kuweka wahusika zaidi, muda wa maenezi ni mrefu na hoja zake zikiwa pana na nzito vilevile.

Ni kwa sababu hii ndiyo maana utafiti huu uliegemea kwenye riwaya na wala sio tanzu nyingine za fasihi andishi mathalan: ushairi, tamthilia na hadithi fupi. Kwa kiasi kikubwa, tanzu za ushairi, tamthilia na hadithi fupi huwa na ubanifu mkubwa upande wa mandhari, wahusika, msuko, jumbe na vipengele vingine vya kimtindo, ubanifu hapa tunarejelea hali ya kutoa maelezo kwa uchache bila kukuzwa kikamilifu. Hivyo basi, utafiti huu ulifaa sana upande wa riwaya na siyo tanzu nyinginezo kwa vile mandhari katika riwaya ni mengi na yamekuzwa vyema.

Isitoshe, huu utafiti ulifanywa kwenye maktaba na mtandaoni ambapo usomaji wa riwaya teule za *Kiu* na *Kidagaa Kimwemwozea* ulifanyika kwa kina. Isitoshe, usomaji wa makala, majarida, tasnifu na marejeleo mengine mengi kuhusu mada ya utafiti pia ulifanywa. Usomaji huu ulisaidia kubainisha malengo ya utafiti vile vile ulichangia katika upatikanaji wa data za upili katika utafiti huu.

### 3.3 Idadi Lengwa.

Kimsingi, utafiti huu ulipaswa kuchunguza riwaya zote za kiuhalisia za Kiswahili ambazo zingeweza kuchanganuliwa mandhari. Hata hivyo, ni baadhi tu ya riwaya hizi ambazo zilisawiri mandhari halisi kwa uketo, kina na uchangamani uliofanikisha ujenzi na uviringaji wa wahusika wake na wakati huo huo yakichangia ukuzaji wa maudhui na ploti. Kwa hivyo, idadi lengwa ya utafiti huu zilikuwa ni riwaya kumi zifuatazo: *Kiu* (Mohamed, 1972), *Utengano* (Mohamed, 1980), *Mwisho wa Kosa* (Burhani, 1987), *Siku Njema* (Walibora, 1996), *Kufa Kuzikana* (Walibora, 2003),

*Ndoto ya Almasi* (Walibora, 2006), *Cheche za Moto* (Habwe, 2008), *Kidagaa Kimemwozea* (Walibora, 2012), *Chozi la Heri* (Matei, 2017) na *Nguu za Jadi* (Momanyi, 2021).

## 3.4 Sampuli na Usampulishaji.

Kwa mujibu wa TUKI (2019) sampuli ni kitu kimoja kati ya vingi vya aina moja, ni mojawapo ya idadi lengwa katika utafiti, ni kati ya ile hesabu ya vitu vya kutafitiwa ili kutafuta suluhu la suala linalofanyiwa uchunguzi. Kwa mujibu wa Kothari (2008) usampulishaji ni utaratibu anaoutumia mtafiti kupata idadi ya watoa taarifa (sampuli) kutoka katika idadi ya walengwa wa utafiti. Katika utafiti huu uteuzi wa sampuli ulikuwa wa kimaksudi, uteuzi huu ni ule uliohusisha hali ambapo mtafiti alichagua kundi fulani la watu, vitu au dhana alizoamini zingefaa utafiti wake.

Kombo & Tromp (2006) wanasema kwamba ni utafiti usiokuwa na shaka aghalabu hutoa majibu ya uhakika. Kwa hivyo, riwaya hizi mbili ziliafikiana na malengo pamoja na nadharia za utafiti huu na ndiyo maana ziliteuliwa kimaksudi. Kwa hivyo, uteuzi wa sampuli ya riwaya zilizochambuliwa uliongozwa na usampulishaji dhaminifu. Hii ni aina mojawapo ya mbinu za usampulishaji sinasibu ambapo sampuli huchaguliwa kwa sababu ina sifa za kipekee zinazohitajika kwenye utafiti. Mbinu hii ilitumika kwa vile ilifaa zaidi katika utafiti huu. Sampuli ya riwaya mbili zilizoteuliwa ilikuwa muhimu na ilifaa zaidi kwa utafiti wa aina hii.

## 3.5 Njia za Ukusanyaji Data.

Data ya utafiti huu ilikusanywa kwa kutumia njia ya usomaji makini. Kwa mujibu wa Rief (2012) hii ni njia ya usomaji ambayo ina mitindo mingi kama vile kupigia mistari maneno usiyoyajua maana (msamiati maalumu), kudondoa hoja muhimu, kuandika au kunakili mawazo kutokana na kile ulichosoma, kuandika maswali, kuchunguza uhusiano au uingiliano matini na mchango wa msimulizi.



Mount Kenya University

Fisher na Frey (2014) wanaeleza kwamba katika usomaji makini inatarajiwa kwamba msomaji azingatie zaidi lengo la mwandishi na hivyo basi kumruhusu msomaji kufahamu na kupata uelewa wa ujumbe unaowasilishwa kupitia matini ya mwandishi anayehusika. Wanaendelea kusema kwamba kwa kufanya hivyo msomaji ataweza kuielewa matini na kwa njia hiyo kumwezesha kuelewa kwa kiwango cha juu. Hinchman na Moore (2013) wanashadidia hoja hii kwa kusema kwamba kusoma kwa aina hii kunamwezesha msomaji kubaini maana na kwa uweledi kuichambua lugha na misuko mbalimbali jinsi inavyojitokeza kwenye tungo au matini.

Kwa hivyo, utafiti huu uliongozwa na usomaji makini ili kutuwezesha kudondoa hoja muhimu kwenye tungo hizi mbili ili kutuwezesha kuafikia malengo yetu. Ikumbukwe kwamba mbinu hii inakuza uelewa wa tungo au matini (Shanahan, 2014)

### 3.6 Uchanganuzi wa Data.

Buliba na wenzie (2014) wanaeleza kwamba uchanganuzi wa data hutegemea aina ya utafiti unaohusika. Uchanganuzi wa data za utafiti huu ulifanywa kwa mujibu wa yaliyomo ili kubaini aina mbalimbali za mandhari kwenye riwaya teule na michango yao katika ujenzi wa ploti ya hadithi pamoja na ukuzaji wa sifa za wahusika mbalimbali kwenye riwaya hizi. Isitoshe, uchanganuzi wa yaliyomo ulifanikisha ubainishi wa jumbe mbalimbali zilizokusudiwa kuwasilishwa kwa hadhira lengwa kupitia kwa mandhari anuwai.

### 3.7 Uwasilishaji wa Matokeo.

Kufuatia uchanganuzi wa data, matokeo ya utafiti yamewasilishwa kwa njia ya maelezo. Ufafanuzi wenyewe umetekelezwa kwa mujibu wa malengo na mihimili ya mseto wa nadharia zilizoongoza uchunguzi wenyewe. Adam (2014) anasema kwamba maelezo ni njia ya uchambuzi ambayo huidhinisha mtafiti kusoma au kusikiliza kazi ya fasihi, kufahamu maudhui, mitazamo ya kifalsafa

ya kazi hii miongoni mwa mengine muhimu.Kila hatua ya matokeo ya utafiti imeelezwa kwa uketo baada ya usomaji makini kwenye sehemu ya uchanganuzi wa data.

### 3.8 Maadili ya Utafiti.

Wizi wa kitaaluma ni hatia kwa vile huenda kinyume cha maadili ya uandishi wa kitaaluma. Wizi wa aina hii, kwa mujibu wa Mligo (2012) ni kule kuiba maneno, vifungu kutoka kwa kazi za wengine bila kuwatambua. Haya yameepukwa kwa kutambua kila mtafiti ambaye mchango wake umenukuliwa kufanikisha malengo ya huu utafiti.

Barua rasmi za kupata idhini ya kufanya huu utafiti ziliombwa kutoka chuo kikuu cha Mount Kenya. Mtafiti aliomba kibali cha kufanya utafiti kutoka katika kitengo cha idhini za ukusanyaji wa data nchini, NACOSTI. Utafiti huu ulifanywa na kuongozwa na uwazi pamoja na uadilifu. Data zilizokusanywa zilithibitishwa kuwa za kweli na kuaminika. Mtafiti alipata kibali kuingia maktaba mbalimbali kusoma tasnifu na vitabu teule.

### 3.9 Hitimisho.

Sura hii ndiyo ilikuwa mhimili mkuu wa utafiti huu. Ndiyo iliyotekeleza dhima muhimu katika kufafanua jinsi utafiti mzima ulivyofanikishwa. Kupitia kwayo tumebainisha muundo wa utafiti huu, eneo la kufanyia utafiti (fasihi andishi), idadi iliyolengwa na utafiti, sampuli na usampulishaji, njia za zilizotumika kukusanyia data ya utafiti, uchanganuzi wa data pamoja na mazingatio ya maadili ya kitafiti.

# SURA YA NNE

# UCHANGANUZI WA DATA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO

## 4.0 Utangulizi.

Mandhari hufasiliwa kwingi kuwa ni mahali au wakati ambapo sanaa ya fasihi hutendwa. Utafiti huu uliazimiwa kuchunguza jinsi usawiri wa mandhari kwenye riwaya ya *Kiu* na *Kidagaa Kimemwozea* ulivyobainisha uhusiano uliopo kati ya mandhari yenyewe na sifa za wahusika, uwasilishaji na ukuzaji wa ujumbe pamoja na kudadavua uhusiano uliopo kati ya mandhari na uendelezwaji wa ploti. Kwa hali hiyo, sura yenyewe imegawika katika sehemu kuu tano. Sehemu ya kwanza ni utangulizi, ikifuatiwa sehemu ya pili inayobainisha mandhari anuwai yatumiwayo kuwasilisha ujumbe katika riwaya teule. Sehemu ya tatu inatathmini mchango wa mandhari katika ujenzi wa sifa za wahusika ilhali sehemu ya nne inajadili mchango wa mandhari katika ukuzaji wa ploti za riwaya teule. Hatimaye, muhtasari wa yaliyomo umewasilishwa kama hitimisho la sura.

## 4.1 Matumizi ya Mandhari Kuwasilisha Ujumbe wa Riwaya.

Mandhari yanayosawiriwa katika kazi ya fasihi yana nafasi adhimu ya kuwasilisha yaliyomo na aghalabu huathiri dhamira za tungo zinazohusika (Wamitila, 2002). Mandhari anuwai yanasawiriwa kwenye riwaya teule za *Kidagaa Kimemwozea* na *Kiu* kwa minajili ya kutekeleza majukumu tofauti tofauti. Hata hivyo, utafiti huu ulijishughulisha na uchunguzi wa mandhari ili kuyafikia malengo yake. Vijisehemu viwili vifuatavyo vinajadili jinsi mandhari mbalimbali yalivyotumika kuwasilisha ujumbe au maudhui ya riwaya teule. Mjadala unaanza kwa kushughulikia riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* kabla ya kuzamia riwaya *Kiu*.

### 4.1.1 Mandhari Yawasilishavyo Maudhui ya *Kidagaa Kimemwozea.*

Riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* ilichapishwa na Ken Walibora mnamo mwaka wa 2012. Anwani yake iliandikwa kwa kutumia mbinu ya jazanda kwa lengo la kumfanya msomaji aweze kuibua hoja nzito nzito ambazo mwandishi alinuia kuziwasilishia hadhira yake. Riwaya ya *Kidagaa kimemwozea* inadhihirisha namna wahusika kadhaa kwenye kazi hii walivyoendewa mrama na masuala mbalimbali kwa njia moja au nyingine kwenye mazingira mbalimbali wanamojikuta au hata kuishi. Baadhi ya wahusika hao ni: Mtemi Nasaba Bora, Mwalimu Majisifu, Dora, DJ, Amani, Imani na wengineo.

Mwandishi wa riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* anatumia mandhari za aina mbili kuwasilishia jumbe zake - mandhari ya mahali na mandhari ya wakati. Mandhari ya mahali yaliyojitokeza katika riwaya hii ni kama vile: Mto Kiberenge, Sokomoko, Nyumbani kwa Mwalimu Majisifu, Kibanda cha Amani, Shuleni Ulitima, Kasri la Mtemi Nasaba Bora, Barabarani, Shuleni Nasaba Bora, Seli ya Mtemi Nasaba Bora, Ukumbini kwa Mtemi Nasaba Bora, Ukumbini chuoni Mkokotoni, Chumba cha kulala kwa Mtemi Nasaba Bora, Zahanati ya Nasaba Bora, Misitu na Barazani kwa Amani. Nayo mandhari ya wakati pia yamejitokeza kupitia madondoo yanayozungumzia enzi za Ukoloni na Vita Vikuu Vya Dunia vya Pili.

#### 4.1.1.1 Mto Kiberenge.

Mandhari ni mahali palipotengewa shughuli fulani katika kazi ya utunzi (White, 1983). Masimulizi kwenye riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* yanapoanza, tunajipata kwenye mandhari kando kando ya Mto Kiberenge ambapo tunawapata vijana wawili walioketi chini ya mti, mvulana anajulikana kama Amani Chichiri Hamadi na msichana Imani Mtembezi. Katika mandhari haya tunapata kuelezwa na msimulizi kwamba wahusika hawa walikuwa wameketi pale chini ya mti kando ya

Mto Kiberenge kwa sababu walikuwa wamechoka baada ya safari ndefu, katika ile hali ya kuchoka kwao walihisi kiu sana. Ikatokea bahati kwamba walifika pahali ambapo maji yalikuwa mengi mno. Hata hivyo, maji hayo yalikuwa na mwiko, wakaazi wa Sokomoko walikuwa hawayanywi maji ya mto huo (uk. 3). Inasemekana kwamba hapo awali mwanamume mwenye kifafa alikuja kuoga kwenye mto huo na aliposimama kwenye jabali moja telezi, ghafla alianza kufafaruka, akateleza na kuanguka humo majini na kuzama. Maiti yake ilitafutwa kwa siku kadha bila mafaniko. Hapo ndipo palizuka itikadi kwamba miungu hawakutaka Wanasokomoko kunywa maji ya Mto Kiberenge. Itikadi hii ilienea ng'ambo zote mbili na hata wimbo ukatungwa ili kuzuia watu kunywa maji ya mto huo. Maji hayo yakasalia kuwa ya kunywesha mifugo na watoto kupigia mbizi.

Msichana huyu mdogo kwa jina Amani, mwenye umri wa miaka kumi na minne hivi, kwa sababu ya kukabwa na kiu, alichuchumaa na kuteka yale maji kwa vitanga vyake na kupiga mafunda kadhaa. Watoto waliokuwa wakiogelea walishangaa na kutoka majini kumtazama Imani. Mmoja wao kwa jina DJ akasikika akimaka kwa kusema,

> *"Mazee mcheki ule dame. Anakunywa maji ya Kiberenge mazee!*" (Uk. 5).

Kwa mujibu wa masimulizi haya ni dhahiri kwamba maudhui ya utamaduni yanajitokeza katika mandhari haya. Mwandishi kupitia msimulizi wake amedhihirisha jinsi maudhui ya utamaduni yanavyojitokeza miongoni mwa Wanasokomoko kupitia itikadi ya kutokunywa maji ya Mto Kibengere na jinsi ambavyo itikadi hii inavyowakandamiza bila wao kujua. Hawawezi kukata kiu yao kwa maji kutokana na itikadi hiyo potovu. Maji yakasalia ya kunywesha mifugo na watu kuogelea tu.

Kupitia mandhari yaya haya ya Mto Kiberenge msimulizi pia anatueleza kuhusu mhusika kwa jina DJ ambaye alikuwa ametekwa nathari na yale ambayo Imani alitenda, kunywa maji ya Mto Kiberenge, akasahau kwamba yeye pamoja na wachungaji wengine walikuwa na jukumu la kuchunga ng'ombe na kwamba tayari fahali mmoja mweusi kati ya wale waliokuwa wakichunga, tayari alijongea karibu na kaptura yake kuu kuu na kuanza kuitafunatafuna. Juhudi za kumfukuza hazikufua dafu kwa sababu hatimaye fahali yule alimeza kaptura ile yote. Msimulizi anaendelea kueleza kwamba wale ng'ombe ambao walikuwa wakichungwa na DJ pamoja na wale watoto wengine walikuwa ni wa waajiri wao. Kwa maana kwamba vijana hawa walikuwa wameajiriwa licha ya umri wao mdogo.

Kufuatia kisa hiki cha kaptura ya DJ kuliwa na ng'ombe msimulizi anatufanya tunagundue kwamba watoto hawa walikuwa wameajiriwa na matajiri tofauti tofauti, na kwamba walipata fursa ya kuogelea mtoni kwa sababu ng'ombe wale waliletwa pale kunywa maji. Kwa hivyo, tunapata kwamba maudhui ya ajira ya watoto inajitokeza katika mandhari haya.

Zaidi ya hayo msimulizi alidokeza kwamba kaptura ya DJ ilikuwa kuu kuu na ilipoliwa na yule fahali mweusi Amani alifungua mkoba wake mweusi kisha akatoa ndani shati moja la kaki akamwita kijana huyo toka ng'ambo ya pili na kumkabidhi shati hilo.

> *"Nyamaza kulia," Amani alimwambia,"shika hili shati nadhani litakufaa"*
> *"Ahsante," mvulana yule alisema hima hima huku akivalia hima hima.* (Uk. 8).

Inadhihirika kwamba kijana huyu alitoka katika aila maskini na haya yanajitokeza pale kwenye Mto Kiberenge jinsi alivyolia sana kaptura yake ilipoliwa na yule fahali mweusi. Kwa hivyo ni vyema kusema kwamba maudhui ya umaskini yanajitokeza kupitia masimulizi haya katika mandhari haya ya Mto Kiberenge. Isitoshe, umaskini wa akina DJ vilevile unadhihirika pale ambapo anawahadithia Amani na Imani kuhusu maisha yake bado wakiwa pale kando ya mto

akiwaarifu kwamba mama yake alikuwa mjane na alikuwa akipika pombe haramu katika mtaa wa Madongoporomoka mjini Songoa, si ajabu kwamba hata chanzo cha kijana huyu mdogo kwenda kutafuta kazi ya kuchunga ng'ombe wa Bwana Maozi ilikuwa kwa sababu ya umaskini ambao alikuwa anapitia maishani.

**4.1.1.2 Sokomoko.**

Mandhari ni eneo ambalo hutumiwa na mwandishi kumsaidia kukuza dhamira aliyonuia kuwasilisha kwa hadhira (Izadi, 2017). Msimulizi anatueleza kwamba eneo la Sokomoko lilitengewa Wazungu katika enzi za ukoloni. Anaendelea kusema kwamba baada ya Wazungu kuondoka, Bwana Nasaba Bora alikuwa miongoni mwa Waafrika wachache waliojua mizungu ya "kurithi" ulwa na mali baada ya Wazungu waliozimiliki kuondoka (uk. 13). Anaendelea kusema kwamba Bwana Nasaba Bora aliajiriwa kama karani wa Mzungu katika enzi za ukoloni kisha akajiunga na wizara ya Ardhi na Makao punde tu baada ya uhuru. Inaaminika kwamba ni huku ndiko,

> *"... akajifunza mengi, mbali na kuambukizwa yale maradhi yasiyosikia dawa ambayo baadhi ya dalili zake ni kufichaficha faili za watu ili kujipatia milungula. Maradhi ambayo mhasiriwa wake haoni haya kumwibia hata asiyekuwa na chochote."* (Uk. 13).

Kwa mujibu wa maelezo haya, moja kwa moja tunapata kwamba maudhui ya ufisadi yanachimuzwa. Ufisadi huu unaonekana ulikolea sana hususan katika wizara hii ya Ardhi na Makao ambako Bwana Mtemi Nasaba Bora alikuwa akifanyia kazi. Ikumbukwe kwamba ni huyu huyu mhusika ambaye hatimaye anatawazwa kuwa mtemi wa Sokomoko.

#### 4.1.1.3 Nyumbani kwa Mwalimu Majisifu.

Katika mandhari haya tunapata mhusika kwa jina Mwalimu Majisifu na mkewe Dora ambao wamejaliwa watoto wanne, wadogo wawili ni mapacha kisha kulikuwa na wengine wawili msichana na mvulana. Msimulizi anaeleza kwamba msichana alikuwa na umri wa miaka kumi na saba na kumzidi mnuna wake na mwaka mmoja tu. Hawa waliwapa mwalimu Majisifu na mkewe dhiki ya kuwatunza kwa sababu walikuwa wakitoka udenda mdomoni mfululizo na kwenda haja zote; kubwa na ndogo kwenye nguo zao. Nao wale mapacha walizaliwa bila uwezo wa kutembea. Kutunza watoto kama hawa kulihitaji kujitolea na kuwa na moyo kama inavyodokezwa na dondoo hili:

> *"... lakini Imani hakujikaza tu kisabuni, alikuwa na imani na ndiye aliyekuwa mtu wa kwanza kuwaonea na kuwatendea watoto hawa kama binadamu."* (Uk. 30).

Kwa kuzingatia maelezo hayo ya msimulizi tunapata kwamba matendo ya Imani kwenye nyumba ya mwalimu Majisifu kwa wanawe walemavu yanadhihirisha uwepo wa maudhui ya utu kwenye mandhari haya.

Vilevile, katika mandhari haya msimulizi anatoa maelezo mengine ambayo yanatusaidia kupata maudhui mengineyo. Tunaelezwa kuhusu mandhari ya nyumba ya mwalimu Majisifu. Kwamba palikuwepo makochi, vibweta, kabati na kila aina ya samani za kupendeza. Kadhalika, alikuwa na vyombo vya kisasa vya tafrija kama vile video-kaseti, runinga, video, CD-changer na vinginevyo (uk. 29). Hii ni ishara kwamba mwalimu Majisifu alikuwa tajiri na kwamba tabaka lake lilikuwa la juu katika jamii. Kwa hivyo, kupitia maelezo haya inahalisi kusema kwamba maudhui ya utabaka yanajitokeza kupitia mandhari haya. Isitoshe, kwa kufahamishwa kwamba Mwalimu Majisifu alikuwa na mke pamoja na watoto ni ishara tosha kwamba mandhari haya yamechangia

kutufahamisha kwamba maudhui za ndoa pamoja na malezi yanajitokeza. Ithibati hii inaafiki dai hili,

> *"Mwalimu Majisifu hakuwa mgumba wala mkewe Dora hakuwa tasa. Lakini walijiona wazazi wa laana.*" (Uk. 30)

Msimulizi pia anaendelea kuchimuza maudhui zaidi kwa kutueleza kwamba ipo barua Amani alimwandikia Imani kumweleza kuhusu kile ambacho alikitupa ziwani Mawewa walipokutana mara ya kwanza kabla ya wao kuanza safari ya pamoja kuelekea Sokomoko. Barua hii anamwandikia Imani akiwa sasa mfanyikazi wa nyumbani wa Mwalimu Majisifu. Katika barua hii anamweleza kuwa ule ulikuwa mswada wake uliokataliwa na wachapishaji na kwamba amegundua kuwa mswada huo haukukataliwa jinsi alivyofanywa kuamini. Anamweleza kwamba mswada huo ulichapishwa na kuwekwa kwa jina la mwandishi mwingine tofauti ambaye si mwingine ila ni Mwalimu Majisifu mwenyewe. Barua hiyo haikupaswa kuonwa na mtu yeyote ila kwa bahati mbaya Imani aliitwa ghafla na Dora akaisahau ukumbini alipokuwa akiisoma, aliporudi alimpata Mwalimu Majisifu akiisoma.

Majibizano yakazuka kati ya Imani na Mwalimu Majisifu kuhusu tabia yake ya kusoma barua ambayo si yake.

> "*Ahaa, Mwalimu wasoma barua za watu jamani?" Imani alimuuliza.*
>
> *"Kunradhi bibie. Kunradhi sana," mwalimu Majisifu akajibu huku anatetemeka na kijasho kumchiriza.*
>
> *"Kumbe wewe si mwandishi?"*
>
> *"Lakini usimwambie mtu Imani tafadhali"*
>
> *"Umepata sifa za bure!"* (Uk. 142)
>
> *"Tuambie ulifanikiwaje?"*
>
> "*Nili ... kuwa ninatolesha nakala miswada niliyopewa na mashirika ya uchapishaji niisome, kisha niliwashauri wahariri wawarudishie waandishi*

*miswada na kuwaeleza ni chapwa, haichapishiki. Halafu nakala nilizorudufisha nilizisahihisha kidogo na kuwapelekea wachapishaji wengine kwa jina langu mwenyewe."* (Uk. 143)

Majibizano haya kati ya mwalimu Majisifu na Imani yanachimuza maudhui ya wizi wa kitaaluma.

Mandhari hurejelewa kuwa ni muda na mazingira kijiografia ambayo huwa na msingi mkubwa kwenye utunzi wa tungo za kifasihi (Wamitila, 2008). Msimulizi anaeleza kwamba Mwalimu Majisifu alikuwa mwalimu katika shule ya upili ya Nasaba Bora. Hata hivyo, aliingilia ulevi na akashindwa kabisa kuhudhuria vipindi vyake shuleni. Haya yanadhihirika wazi wakati ambapo Mashaka alipomtembelea kwake na kumkabidhi barua ya mwaliko kwenda Wangwani kutoa mihadhara. Baada ya kuamkiana Mashaka anasema,

*"... twakuona darasani kwa nadra sana.*" (Uk. 47)

Majibizano yanaibuka kati ya Mashaka na amu yake hivi:

"*Nasi twakutaka wewe uje utukomboe toka katika matatizo yetu drasani."*

*"N'takuja. Wajua niko busy sana. Nina kazi nyinyi sana lakini n'takuja karibuni*,"alitoa udhuru Majisifu. (uk 47)

Kwa mujibu wa mazungumzo haya ambayo yanatokea katika mandhari yaliyoleta pamoja Mashaka na Amu yake, Mwalimu Majisifu ambaye kwa wakati huu alikuwa nyumbani kwake badala ya kuwa shuleni,zaidi ya hayo, alikuwa amelewa maudhui ya utepetevu kazini yanajitokeza. Mwalimu Majisifu hajali kazi yake ya ualimu na muda anaowaharibia wanafunzi wake shuleni.

#### 4.1.1.4 Kibanda cha Amani.

Mandhari yanaweza kutazamwa kama eneo la matukio ambalo husaidia kuzijua taaluma za wanajamii na kurithishwa kwao kutoka kizazi kimoja hadi kingine (Jesse, 2017). Msimulizi anaeleza kwamba Amani alifanikiwa kupata kazi katika boma la Bwana Nasaba Bora ambaye kwa sasa alikuwa keshakuwa mtemi na alijulikana kama Mtemi Nasaba Bora. Alipewa kibanda kimoja



Mount Kenya University

kiwe makao yake pale nyumbani kwa Mtemi. Kibanda chenyewe kilizingirwa na ua wa mabua ya matete, paa la nyasi na kuta zilizokandikwa kwa udongo. Sakafuni ilitalizwa samadi ya ng'ombe, mlango wa vipande vya madebe, kitanda kilikuwa cha teremka tukaze. Mazingira haya yanadhihirisha maudhui ya mapuuza upande wa Mtemi Nasaba Bora. Alipuuza hali ya makao ya wafanyakazi wake ndiyo maana aliwaweka kuishi katika hali kama hiyo licha ya kwamba yeye mwenyewe aliishi katika kasri katika boma lilo hilo moja. Vilevile, mapuuza haya yanaonyesha kwamba mtemi hakuwathamini wafanyakazi wake hata kidogo.

Ni katika kibanda hiki pia ndipo tunaelezwa kwamba alfajiri moja kuu Amani aligutushwa kutoka usingizini kwa mlio wa kitoto kichanga. Alipoamka alikikuta kitoto kichanga ambacho hakikuwa kimemaliza hata siku moja tangu kuzaliwa msimulizi anaeleza kuwa,

> *"... Alikionea kite kitoto kile kichanga, akakiokota huku mikono ikitetemeka na kuingia nacho kibandani*." (Uk. 35).

Tendo hili la Amani linadhihirisha kwamba alikuwa na utu na hivyo basi linachimuza maudhui ya utu. Amani hakujua kilipotoka kile kitoto lakini kwa sababu ya utu wake aliamua kumkumbatia na kumwokoa kutoka kwenye kibaridi kikali cha alfajiri.

Msimulizi anaeleza kwamba mazungumzo yalinoga kati ya Amani na Madhubuti mwanawe Mtemi Nasaba Bora baada ya kutoka Urusi alikoenda kusomea. Mazungumzo haya yalikuwa ya kirafiki kati yao. Madhubuti ambaye sasa alikuwa mwasi mkubwa wa baba yake alienda kwake Amani ili aweze kumfahamisha lengo lake la kutaka kumwanika babake kwa matendo yake maovu. Aliona Amani kama wa manufaa kwake kwa lengo lake. Anasema kwamba, babake ndiye chanzo cha matatizo ambayo yanakumba Sokomoko na anapaswa kukabiliwa vikali, anafafanua,

> *"Hebu sikiza ndugu yangu. Nimerudi na hamasa kubwa ya kuwasaidia wanyonge kutimua mfumo huu usiokuwa na haki na usawa. Naanza kwetu hapa*

> *kiamboni nilikozaliwa. Nataka mtu wa kunisaidia kukomesha madhila ... ambayo chanzo chake ni huyu huyu umwitaye babangu.*" (Uk. 116)

Kwa mujibu wa maelezo haya yanayojiri kibandani mwa Amani, kilichorahisisha kukutana kwake na Madhubuti (huenda wasingejuana kama si kuja kwake Sokomomko na kuishi kibandani humo) ni kwamba Madhubuti anaazimia kuuhamasisha umma ili uutimue uongozi dhalimu wa babake. Maudhui ya mabadiliko yanajitokeza hapa; mabadiliko kutoka uongozi mbaya na kuupata uongozi bora.

#### 4.1.1.5 Shuleni Ulitima.

Kupitia kumbukizi yake Amani, msimulizi anaeleza kwamba alikuwa na rafiki yake kwa jina Fao. Anasema kwamba Fao hakuwa mjinga darasani ila wazazi wake hawakumwamini sana masomoni. Imebainika kwamba Fao hakufanya mtihani wa shule ya msingi bali alifanyiwa. Akaitwa katika shule ya sekondari maarufu zaidi Ulitima. Shuleni hapa alichechemea na kuyumbayumba masomoni pia. Hatimaye, akafanyiwa tena mtihani wa shule ya sekondari. Amani anasimulia kwamba,

> *"... matokeo yalipotangazwa wote walikuwa wameushinda mtihani; Amani kwa jasho lake mwenyewe na Fao kwa kufanyiwa*." (Uk. 36).

Maelezo haya yanadhihirisha moja kwa moja kwamba kufaulu mtihani kwa Fao shuleni Ulitima kulichangiwa pakubwa na ufisadi. Kuna uwezekano kwamba waliomfanyia Fao mitihani ya shule ya msingi na upili walilipwa ili kufanikisha udanganyifu huo. Kwa hali hiyo, mandhari ya shuleni yanachimuza maudhui ya ufisadi unaowashirikisha watoto,wazazi na walimu.

#### 4.1.1.6 Kasri ya Mtemi Nasaba Bora.

Msimulizi aneleza kwamba Zuhura mkewe Mtemi Nasaba Bora alijaliwa watoto wawili; mmoja mvulana kwa jina Madhubuti na binti kwa jina Mashaka. Anasimulia kwamba pengo kati yao

lilikuwa kubwa kwa sababu ya uzazi wa mpango. Madhubuti alipohitimu shule ya sekondari alielekea Urusi kusomea elimu ya juu katika chuo kikuu cha Moscow. Kwenda kwake Urusi halikuwa jambo rahisi kwa wanasokomoko kwa sababu,

> *"Ulikuwa ni msukumo kwa kila mmoja Sokomoko. Hapakuwa na hiari. Watu walitozwa hata wasiokuwa navyo kwa ajili ya safari ya mtoto wa mtemi kwenda kusomea urusi."* (Uk. 40).

Hii inaashiria kwamba Mtemi Nasaba Bora alitumia wadhifa, uwezo na nguvu alizokuwa nazo kimamlaka kuwashurutisha wanasokomoko kutoa pesa ili mwanawe akasomee Urusi. Kwa hivyo, kupitia masimulizi haya tunapata maudhui ya unyanyasaji. Utozwaji wa pesa tena kwa lazima kwa matumizi ya kibinafsi upande wa kiongozi ni unyanyasaji wa hali ya juu.

Vilevile, katika mandhari haya, hila na njama za Mtemi Nasaba Bora hatimaye zinagunduliwa na Amani. Mtemi anakumbwa na uasi wa mwanawe Madhubuti baada ya kutoka Urusi. Msimulizi anaeleza kwamba Mtemi Nasaba Bora anaishia kuungama dhambi zake,

> *"Kwa kweli najuta," alisema Mtemi Nasaba Bora. "Nilifanya mengi mabaya, lakini siwezi kukueleza yote. Katika wizara na Makao nilikoanzia ajira niligundua kwamba yupo Mtomoko aishiye nchi ya nje ambaye amenunua shamba la mzungu, yaani **special plot** Nikawalipa majambazi kummaliza pindi awasilipo nchini. Nilijua fika kwamba mwanawe Yusufu angempokea uwanja wa ndege. Nilitaka kuwamaliza wote. Lakini watu niliowalipa kuitekeleza njama hawakufuata maagizo (waliua Mtomoko mwenye shamba; Chichiri Hamadi na kumwacha mwanawe Yusufu). Ikawa lazima kutafuta njia ya kumfungisha jela kwa kumnasibisha na mauaji ya babake. Ilibidi kulipa hela nyingi ya kadhongo kuwalipa polisi, makarani wa mahakama, majaji ..."* (Uk. 150)

Kwa mujibu wa mazungumzo haya baina ya Mtemi Nasaba Bora na Amani nyumbani kwa Mtemi maudhui ya kifo na ufisadi yanajitokeza. Mandhari haya yanawakutanisha wahusika wawili ambao mmoja ni mhini (Mtemi) na mwingine mhiniwa (Amani). Kuungama kwa Mtemi kunafichua ukweli uliofichika kwa muda mrefu.

Mtemi Nasaba Bora anapotoa hatimiliki zilizokuwa kwenye sefu katika chumba chake cha kulala, Amani anamsaili kuhusu mambo fulani kuzihusu. Mazungumzo baina yao yanaendelea hivi:

> *"Mbona kuna hatimiliki tofauti kwa kila shamba?" Amani aliuliza.*
>
> *"Moja ni bandia na nyingine halali," alijibu Mtemi Nasaba Bora.*
>
> *"Kwa nini?"*
>
> *"Kijana we' ni nani ?" aliuliza Mtemi hatimaye.*
>
> *"Mimi ni mjukuu wa Chichiri Hamadi na mpwa wake Yusufu Hamadi uliowatenda uliyoyatenda*"(kur 148-149)

Kutokana na mazungumzo haya maudhui ya uozo katika jamii yanajitokeza. Uozo wa kughushi stakabadhi muhimu za watu na kuwapokonya mashamba yao halali.

#### 4.1.1.7 Uwanja wa Nasaba Bora.

Kwa mujibu wa maelezo ya msimulizi, ilikuwa ni siku ya kusherehekea Sikukuu ya Wazalendo na kwamba uwanja wa Nasaba Bora ulijaa hadi pomoni na watu waliokuja au kulazimishwa kufika katika sherehe hizo kama anavyoilalamikia hali hiyo Bi. Kizee,

> *"Afadhali wangeniacha nende kondeni nipalilie mtama wangu*" (Uk. 70).

Amani alikuwa miongoni mwa waliohudhuria, alishuhudia wageni wateule wameketi kwenye viti ndani ya banda lililotandaziwa tarubai la kijani kibichi. Wananchi wa kawaida kama yeye walisimama uwanjani, anga ndilo lilikuwa paa lao. Jua la utosini liliwaunguza kama tanuri ya moto. Msimulizi anafafanua kwamba punde baada ya wimbo wa taifa kuimbwa waheshimiwa waliketi vitini huku akina yakhe wengine wakaketi chini. Haikuwa hoja kama palikuwa na nyasi au vumbi.

Mtemi Nasaba Bora anapopanda jukwaani anawahutubia wananchi akitumia lugha ya Kiingereza, waliohudhuria kama vile Bi. Kizee wananung'unika wakisema kwamba,

"*Jua litatua kama bado tunasikiliza hizi fwot fwot.*" Uk. 70.

Maelezo haya yanachimuza maudhui ya ukoloni mamboleo, hapakuwa na haja ya kutumia lugha ya wakoloni katika sherehe ya wazalendo wa nchi huru ya Tomoko.

Kwa mujibu wa Munyao (2017) mandhari ni kipindi fulani katika jamii ambapo matukio hujengeka baada ya muda fulani. Baada ya sherehe za Sikukuu ya Wazalendo kuisha, msimulizi anasema kwamba mvua kubwa ilianza kunyesha. Makabwela na akina yakhe waliothubutu kuingia hemani walizuiliwa na Askari kwa amri ya Mtemi Nasaba Bora. Ikabidi Amani kukimbia na kwenda kujisitiri mvua katika veranda moja ambayo tayari ilikuwa imejaa watu. Maelezo haya yanachimuza maudhui ya utabaka. Kwenye mandhari haya tunaonyeshwa watawala na watawaliwa, wakuu na wadogo,walala hai na walala hoi. Hii ndiyo sababu kuna tabaka la wale wanaochomwa na jua kama Amani na wenzake na tabaka la wale wa kusitiriwa kutoka kwenye makali ya jua kama Mtemi na wenzake. Wanaonyeshewa na mvua pamoja na wanaositiriwa kutokana na mvua hiyo.

#### 4.1.1.8 Barabara.

Baada ya mahudhurio ya sherehe ya Sikuu ya Wazalendo, Amani anapata habari kutoka kwa Imani kupitia kwa DJ kwamba kitoto chao walichokipa jina Uhuru kilikuwa kinaugua. Hiki ni kile kitoto kilichookotwa mlangoni pa Amani alfajiri moja. Kilikuwa kinaumwa. Amani analazimika kutoka uwanjani Nasaba Bora na kuelekea kwenye kibanda chake kwa Mtemi Nasaba Bora. Anapofika anamchukuwa Imani pamoja na kitoto kile kisha wanakaanza safari kuelekea zahanatini kutafuta matibabu. Zahanati yenyewe inafahamika kama Zahanati ya Nasaba Bora. Wauguzi waliokuwa zahanatini wanadinda kukihudumia kitoto hiki. Isitoshe, mmoja wao anasikika akiwakaripia kwa maneno,

> "*Kwani hamjui leo ni Sikukuu? Leo hatufanyi kazi. Nendeni mje kesho.*" (Uk. 77)

Amani na Imani wakatoka pale na kuanza safari ya kurudi walikotoka. Wanapokuwa barabarani, Amani anakichukuwa kitoto kutoka kwa Imani ili amsaidie kukibeba,

> "*Kikakohoa punde. Lilikuwa kohozi kavu. Kilikuwa kimenyongea na kunyong'onyea mno ... kikaanza kufafaruka mikononi mwa Amani na kupumua kwa shida kama mgonjwa wa pumu. Kikanyosha miguu na mikono na kutulia tuli. Kikawa baridi kama barafu.* (Uk. 77)

Hivi ndivyo kitoto Uhuru kinavyofariki na kuiaga dunia. Maelezo haya yanadhihirisha maudhui ya kifo. Kitoto Uhuru kinaaga dunia barabarani baada ya kutohudumiwa na wauguzi. Kwa kukataa kukihudumia Kitoto kinachougua na kuendelea kufuma fulana zao, wauguzi wanatumika kudhihirisha maudhui ya mapuuza na utepetevu kazini.

#### 4.1.1.9 Chumbani Shuleni Nasaba Bora.

Msimulizi anaeleza kwamba ipo barua ambayo Ben Bella alimkabidhi Mashaka. Mashaka ni bintiye Mtemi Nasaba Bora ilhali Ben Bella ni mpenziwe wa kiume. Alimkabidhi barua hiyo kisiri katika Uwanja wa Nasaba Bora siku ya Sikukuu ya Wazalendo. Mashaka aliipokea barua yenyewe kwa ujanja mwingi kwa kujifanya anaenda msalani. Aipokeapo haisomi mara moja bali anaamua kuificha ili kuisomea shuleni chumbani mwake. Afikapo shuleni na kuusoma ujumbe wa barua, Ben Bella anamweleza jinsi dadake, Lowela, alivyotungwa mimba na babake, Mtemi Nasaba Bora. Ben Bella anaeleza jinsi Lowela alivyopata mimba na kuificha,

> *"... alisema kapata mimba aliyoificha kwa kujifunga kamba tumboni wala wazazi wangu hawakuweza kuigundua. Naye babako ndiye kamtunga mimba hiyo ...*" (Uk. 81).

Barua yenyewe inaendelea kufichua mambo kadhaa ambayo yamekuwa siri kwa muda mrefu,

“*Siku zake zilipokaribia babako alimtoa nyumbani kisirisiri na kumpeleka mtoto aliyezaliwa mlangoni kwa mchungaji wenu Sokomoko*” (Uk. 81).

Baada ya kuisoma barua hii Mashaka anashikwa na wehu na kuanza kupiga kelele ovyo chumbani. Haamini anayoyasoma katika barua hiyo. Zaidi ya yote, anashindwa kustahimili kuachwa na mpenziwe, Ben Bella. Ni kwenye mandhari haya ambapo maudhui ya mapenzi yanajitokeza. Mapenzi kati ya Mashaka na Ben Bella.

**4.1.1.10 Mandhari ya Seli ya Mtemi Nasaba Bora.**

Eneo hili linaelezwa kuwa ni choo ambacho kilikuwa ni cha umma, chenye harufu kali. Hapa ndipo palikuwa seli ya Mtemi Nasaba Bora kuwafungia mahabusu wake. Miongoni mwa mahabusu waliokuwa kwenye seli hii ni Amani, Imani na Matuko Weye. Amani na Imani wanakamatwa kwa tuhuma za mauaji ya kitoto Uhuru. Naye Matuko Weye anakamatwa kwa madai ya kuzua rabsha kwenye sherehe za Sikukuu ya Wazalendo.

Maudhui ya ukatili yanajitokeza Amani, Imani na Matuko Weye wanapofungiwa kwenye mandhari ya choo kimoja kinachovunda. Isitoshe, Askari wanasubiri Mtemi atoke kisha wanaanza kuwafanyia “kazi”. Wanafunga mlango wa seli na kuwanyaka makofi bila huruma. Wanawaripua viboko na kuwazaba makonde na mateke mfululizo (uk. 89). Maelezo haya yanachimuza maudhui ya ukatili na dhuluma dhidi ya wafungwa. Hapakuwa na sababu za kuwatendea wafungwa hawa matendo ya kidhalimu kama haya.

**4.1.1.11 Mandhari ya Ukumbi wa Mtemi Nasaba Bora.**

Mandhari ni nguzo muhimu kwenye kazi ya fasihi ambazo hujikita kwenye kanuni za ushabihikweli (Wamitila, 2008). Kanuni za aina hii husisitiza uhusiano uliopo kati ya ulimwengu

bunilizi na ulimwengu halisia na hivyo kumfanya anayesoma aamini kwamba tukio, mazingira na maingiliano ya wahusika yanayotokana na mazingira haya bunilizi ni ya kukubalika.

Msimulizi anaeleza kwamba Mwalimu Majisifu alirauka kwenda kumtembelea nduguye, Mtemi kwake nyumbani. Sababu zilizopelekea ziara yake asubuhi ile zilikuwa nyingi mno: mwanzo, alitaka kumweleza kwamba alikuwa amepokea tikiti ya ndege kutoka nchini Wangwani ili aende atoe mihadhara huko katika chuo kikuu cha Mkokotoni, pia alitaka kumweleza kuwa mkewe anateseka sana kuwatunza watoto wao wenye ulemavu baada ya mjakazi aliyechukuwa nafasi ya Imani kutoroka, alitaka kumweleza kuwa alitaka Imani aachiliwe huru ili aende amsaidie mkewe akiwa safarini Wangwani na mwisho, alitaka kumweleza kwamba siku hizi hanywi chai yenye sukari. Hata hivyo, panaondokea mvutano mkubwa baina yao ukumbini na anashindwa kumweleza nduguye haya. Kinachosababisha mfarakano huu ni ulevi wa Mwalimu Majisifu. Chai inapoletwa Mwalimu Majisifu anashindwa kuinywa kwa sababu ulevi umekwisha mwathiri. Mtemi Nasaba Bora anapoingia ukumbini baada ya salamu anaanza kumzomea nduguye,

> *“Tembo itakuua ndugu yangu. Punguza ulevi bwana ... Hii ni aibu bwana. Kumbuka marehamu baba yetu alikua kasisi ndugu yangu. Alikuwa akisema kwamba walevi hawataingia katika ufalme wa mbinguni.*” (Uk. 93)

Maongezi haya yanayoendelezwa asubuhi ukumbini nyumbani kwa Mtemi Nasaba Bora yanachimuza maudhui ulevi. Mwalimu Majisifu ndiye anayeendeleza maudhui haya.

#### 4.1.1.12 Mandhari ya Ukumbi Chuoni Mkokotoni.

Tunaelezwa na msimulizi kwamba Mwalimu Majisifu alifika chuoni Mkokotoni nchini Wangwani kwa mwaliko wa chuo hicho ili kutoa mihadhara kwa wanafunzi kuhusu, *“Dhima ya mwandishi kwa jamii barani Afrika.”* Wanafunzi na wahadhiri walikuwa ukumbini kwa lengo la kuipokea mihadhara hiyo. Mwalimu Majisifu akatapatapa na kushindwa kutoa mihadhara yenyewe.

Wanafunzi wakachemka kwa hamaki huku wengine kama Rasta wakimfokea na hata kumuumbua hadharani, wengine wakitaka kujua kama kweli yeye ndiye mwandishi wa kitabu, *Kidagaa Kimemwozea.* Wengine wanamzomea kwa kusema yeye ni mwizi wa kazi za wengine na kwamba si mwandishi jinsi anavyodai. Ingawa anapata kinga kupitia kwa mhadhiri mmoja anayepanda jukwaani ghafla na kuwatuliza wanafunzi; anapata aibu kubwa.

Kwa hivyo, mandhari haya yanadhihirisha maudhui ya elimu kwa sababu wanafunzi wanafika chuoni kwa azma ya kusoma. Vivyo hivyo, wahadhiri wapo chuoni kutimiza wajibu wao wa kuwafundisha wanafunzi.

Vilevile, mandhari haya yametusaidia kubaini kwamba Mwalimu Majisifu hakuwa ndiye mwandishi wa kile kitabu maarufu cha *Kidagaa Kimemwozea* jinsi alivyodai; haya ni kwa mujibu wa maswali anayoulizwa na mwanafunzi mmoja,

> *"Je, wewe ndiye uliyeandika Kidagaa Kimemwozea*?" "*Twasikia tetesi kwamba hukuandika riwaya hiyo, kwamba ulichukuwa mswada wa mtu mwingine?*" (Uk 125)

Maelezo haya yanabainisha maudhui ya wizi wa kitaaluma. Maudhui ni ujumbe unazojitokeza kwenye kazi ya sanaa (Gatakaa, 2012). Kupitia kwa mandhari haya tumepata kuelezwa kuhusu jumbe mbalimbali kama elimu na wizi wa kitaaluma.

#### 4.1.1.13 Chumba cha Kulala kwa Mtemi Nasaba Bora.

Msimulizi anaeleza kwamba ipo siku Mtemi Nasaba Bora alielekea mjini Songoa kuomba muda wa kulipa madeni aliyokuwa nayo. Ikawa kwamba Mashaka, bintiye alizidiwa wehu. Ilichukuwa bidii ya Amani kumsaidia Bi. Zuhura kumfunga kwa kamba na kumpeleka katika chumba chake. Bi. Zuhura akamwomba Amani kulala kwenye kasri lao ili endapo Mashaka atazua rabsha tena

aweze kumsaidia. Amani anakubali kulala kwenye kochi. Usiku huo Zuhura anamwita Amani aende kwenye chumba chake cha kulala,

"*Hebu njoo uone kuna kitu hapa,*" Bi. Zuhura alimwita Amani. (Uk. 130).

Msimulizi anaendelea kueleza kwamba Amani anaenda huko kwenye chumba cha kulala, japo shingo upande. Anajaribu kutafuta alichomwitia Bi Zuhura. Hata hivyo, baada ya tafuta tafuta anaona kitu kama kipanya kikitembea mvunguni mwa kitanda. Wote wanakuwa katika hali ya kuangaza angazaa mvunguni mwa kitanda, mlango wa nje wa kasri hilo unapofunguliwa. Kwa vile Mashaka alikuwa akipiga kelele sana hawasikii chochote, hata Mtemi anapofika. Mlango wa chumba cha kulala unafunguliwa na Mtemi kuingia. Wote wawili wanashtuka. Mtemi Nasaba Bora hakutaka kujua kilichokuwa kinajiri pale, anafululiza mpaka kwenye sefu na kutoa bunduki yake ya mrao na kumtwanga Amani kinyama. Baadaye anambeba kwa gari lake na kumtupa kando ya barabara akiwa amepoteza fahamu. Maelezo haya ya hali na mandhari yanawasilisha maudhui ya ukatili.

#### 4.1.1.14 Zahanati ya Nasaba Bora.

Msimulizi anaeleza kwamba pesa zilizotumika kujenga zahanati ya Nasaba Bora zilikuwa auni ya fedha kutoka kwa serikali ya Uingereza. Lengo lilikuwa kujenga hospitali kuu. Inasemekana kwamba pesa hizi zilipofika zilitumiwa kwa matumizi mengine muhimu na sehemu ndogo iliyosalia ilitumika kujengea zahanati ndogo kisha ikapewa jina la mmoja wa wasimamizi waliofuja pesa zenyewe. Tunasimuliwa kwamba:

"*Akali kubwa ikaingia mfukoni mwa wasimamizi hao*." (Uk. 144).

Usimulizi kuhusu mandhari na hali ya Zahanati ya Mtemi Nasaba Baora ni ithibati ya maudhui ya ubadhirifu wa mali ya umma unaotekelezwa na viongozi wafisadi.

#### 4.1.1.15 Misitu.

Baada ya Amani kumwokoa Mtemi Nasaba Bora mikononi mwa Gadaffi na genge la majambazi ambao walitaka kumuua kwa sababu ya kilipiza kisasi kwa kuwafungia gerezani, msimulizi anaeleza kwamba Mtemi anambeba Amani garini mpaka kwake ambapo alikiri makosa yake kwa Amani. Kuanzia wizi wa mashamba, mauaji na kutia watu gerezani kwa visingizio. Baadaye Mtemi anapotea nyumbani kwake, siku kadhaa zinapita na haijulikani alipo. Hata hivyo, siku moja mwindaji, katika shughuli zake, anapata kimba cha mtu kilichooza kikining'inia kwenye mkuyu. Tunasimuliwa kwamba:

> "*Mwendazake alitambulikana kwa mkanda wake*." (Uk. 159).

Anayeelezwa hapa ni Mtemi Nasaba Bora. Matukio haya kwenye msitu yanachimuza maudhui ya mauko. Kifo cha Mtemi Nasaba Bora kwa njia ya kujitia kitanzi.

#### 4.1.1.16 Barazani kwa Amani.

Imethibitika kwamba mandhari huchangia ukuzaji wa maudhui ya kazi ya fasihi. Kupitia kwa mandhari, mwandishi anaweza kuwasilisha ujumbe wake kupitia ufafanuzi na usukaji wa matukio kwenye eneo fulani. Hii ni kwa sababu maudhui ni jumla ya fikra za mwandishi kwa kuzingatia muktadha, mandhari yakiwemo (Njogu & Chimerah, 1999).

Msimulizi anaeleza kwamba baada ya kuachiliwa huru kwa Amu ya Amani kwa jina Yusufu, Imani alimshawishi Amani aandike hadithi yote jinsi ilivyotokea. Msimulizi anaeleza kwamba hapa walishaingia katika gereza liitwalo ndoa baada ya wawili hawa kuvunja uhusiano wao wa ndugu na dada. Kwa sasa, walikuwa kwao na walikuwa mke na mume; wanandoa halisi. Kwa hivyo, maelezo haya yanachimuza maudhui ya ndoa. Usimulizi unajiri kwenye mandhari ya barazani nyumbani kwa kina Amani wakiwa wanandoa.

#### 4.1.1.17 Mandhari Kiwakati.

Mandhari katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* vilevile yamechukuwa mkondo wa kiwakati kama vile: Enzi ya ukoloni na Vita vikuu vya dunia. Wamitila (2008) anafafanua kwamba mandhari ni mazingira, pahali na majira yanayosawiriwa kwa mujibu wa wakati, muda au kipindi fulani kihistoria. Akishadidia hili msimulizi anasema kwamba,

> "*Wakati wa harakati za ukombozi dhidi ya ukoloni maiti za Waaafrika waliouawa na Wazungu zilitupwa katika Mto Kiberenge.*" (Uk. 4).

Hali hii inaashiria kwamba upo wakati ambapo wakoloni walikuwa katika nchi ya Tomoko na ulipotimia muda fulani vita vya ukombozi vilizuka ili Waafrika wajinasue kutokana na minyororo ya ukoloni. Vita vilizuka kati ya wapiganaji wa Kiafrika ambao walijitolea mhanga kukomboa nchi yao. Wengine waliangamia na miili yao kutupwa katika Mto Kiberenge, maelezo haya yanachimuza maudhui ya ukoloni mkongwe.

Kuhusu Vita vikuu vya dunia, tunasimuliwa kumhusu Major Noon almaarufu kama Majununi. Huyu alikuwa ni mlowezi aliyekuja Sokomoko enzi za ukoloni. Serikali yao ya Kikoloni ikawanyakulia mashamba. Wakawa na mashamba ya kukuzia mimea mbalimbali kama mchai, mpareto, kahawa, na kadhalika. Majununi akajenga hema lake na kuishi. Inasemekana mlowezi huyu alichumbiana na Mfaransa mmoja kwa jina Michelle kabla ya kuenda kupigania nchi yake ya Uingereza katika Vita Vikuu vya Dunia vya Pili ambavyo vilitokea ulimwenguni wakati mmoja. Maelezo haya yanaibua mandhari ya kiwakati ya Vita vikuu vya Dunia vya Pili ambavyo vilisababisha maafa makuu na uharibifu mkubwa wa mali na miundo msingi ya mataifa kadhaa. Maudhui yanayojitokeza hapa ni ya siasa.

### 4.1.2 Mandhari Yawasilishavyo Maudhui ya *Kiu.*

Riwaya ya *Kiu* ilitungwa na Mohamed S. Mohamed mnamo mwaka wa 1972. Riwaya hii inasawiri wahusika mbalimbali katika mandhari tofauti. Wahusika wenyewe wanasakamwa na tamaa za aina tofauti tofauti; wengine wakiwa na tamaa ya mali na wengine tamaa ya mapenzi na hata tamaa ya maisha mazuri. Kwa hivyo, riwaya ya *Kiu* inatumika kudhihirisha kiu au tamaa za wahusika. Baadhi ya wahusika wanaochimuzwa ni Mzee Mwinyi, Bahati, Idi, Cheusi, Jaku pamoja na wengineo

Mandhari mbalimbali yanatumika katika riwaya ya *Kiu.* Yapo mandhari ya mahali na vilevile mandhari ya wakati. Baadhi ya mandhari ya mahali yanayotumiwa kuwasilishia ujumbe katika utungo huu ni pamoja na: mandhari ya barabarani, Ukele, Benzi la Mwinyi, Benki, Selea, Vibyongoni kwa Idi, Chumba cha Kidawa, Chumba cha Tatu na Buraha. Nayo mandhari ya wakati yaliyotumiwa ni pamoja na madondoo yanayohusu siku ya tatu ambapo Bahati alishikwa na hamu ya kumwona Idi, miaka mitano baada ya kuolewa na Idi na mateso kuzidi kwenye ndoa kati yao, pamoja na miaka sita tunayoelezwa kwamba babake bahati alielekea Kongo.

#### 4.1.2.1 Chumba cha Mwinyi.

Wamitila (2008) anaonyesha jinsi ambavyo mandhari hutumika kuwasilisha maelezo na usimulizi wa tukio fulani ili kulipa mkondo au mwelekeo fulani. Mzee Mwinyi anasimuliwa kuwa ni mzee mwenye miaka sitini na miwili na alikuwa na ukwasi mkubwa wa mali. Chumba chake kinaelezwa kama ifuatavyo:

> *"Chini ya nyayo zake alikuwa amekanyaga zulia zuri ambalo thamani yake ingetosha kumfariji maskini kwa siku na miezi.*" (Uk. 1).

Ufafanuzi huu una maana kwamba mzee huyu alikuwa na utajiri mkubwa. Kwa mujibu wa ufafanuzi huo wa mandhari ya chumba chake, maudhui ya utajiri mkubwa yanachimuzwa.

#### 4.1.2.2 Benzi la Mwinyi.

Pamoja na gari la kifahari la Benzi kuashiria utajiri aliokuwa nao Mzee Mwinyi, mazungumzo yanayoendelea kwenye mandhari ya Benzi hilo wakiwa na Idi kuelekea Selea kumtafuta Bahati ni ya watu wanaongea kuhusu masuala ya mapenzi. Idi anaishadidia hali hii kwa kuuliza swali balagha lifuatalo:

> *"Ati watu husema mapenzi hayakutani, mbona yako wewe na Bahati yamekutana?" alisema Idi.* Uk.5

Inafahamika kwamba Idi anayasema maneno haya kumfurahisha tu Mzee Mwinyi ambaye amelemewa na kunogewa hisia za mapenzi kwa Bahati. Hata hivyo, Bahati hampendi ila anampenda Idi. Hivyo basi, inahalisi kusema kwamba maudhui ya mapenzi, dhati na bandia, yanajitokeza kwenye mandhari haya ya gari la kifahari.

#### 4.1.2.3 Makonde.

Inasimuliwa kwamba baada ya Idi kumzungusha Mzee Mwinyi barabarani anachoshwa mno. Hatimaye, Idi hamfikishi nyumbani kwa kina Bahati maeneo ya Selea. Wanaghairi nia na kuamua kuelekea Ukele, mahali ambapo Mwinyi alikuwa na jumba kubwa. Wanapokuwa garini wanapitia Tafuteni kisha katikati ya misitu na kutokea upande wa makonde ya karibu. Msimulizi anafafanua kwamba,

> *"Kama si ule moshi uliotoka katikati ya mabiwi yaliyokuwa yakichomwa konde za karibu anga lingetakata. Viwingu vya moshi vilijisokota juu ya gari lao kisha vikapotelea hewani na kuambukiza hewa yote harufu ya majani yanayoungua*." (Uk. 6)

Maudhui ya uchafuzi wa mazingira yanajitokeza moja kwa moja katika maelezo haya ya sehemu za makondeni.

#### 4.1.2.4 Mtaa wa Selea.

Kupitia kwa mandhari ya mtaa wa Selea maudhui ya umaskini na utamaduni yanadhihirishwa wazi. Anavyoeleza Ntaragwi (2004), maudhui ni ujumbe nyeti unaojitokeza kwenye sanaa nzima ya fasihi. Maelezo ya mandhari ya mtaa wa Selea yanajenga taswira halisi ya jinsi umaskini na utamaduni unachimuzwa kwenye riwaya hii. Huku ndiko mtaa anakoishi Bahati na mamake, Cheusi. Bahati ndiye msichana anayemtia Mzee Mwinyi kiwewe cha mapenzi. Mtaa wa Selea unaelezwa kuwa na nyumba zilizozeeka. Nyumba ya kina Bahati inasimuliwa kwa maelezo yafuatayo:

> *"... si kuta, si mlango, si paa, vyote vilionekana mfano wa kizee anayeomba mauti ... Nyumba ilikuwa na vidirisha vinne, viwili vilikuwa usoni na vingine ubavuni. Palikuwa na vibaraza viwili kimoja cha kushoto kimebomoka.*" (Uk. 18).

Tunaambiwa pia kwamba Bahati alipotoka msalani alipata mamake akiwa ameshapika chai ya mkandaa na mhogo wa kutosa. Hivi ni vyakula viliwavyo hasa na watu wenye kipato cha chini. Isitoshe, kwa vile hawakuwa na viti, Bahati anavuta mbuzi ya kukunia nazi na kuikalia. Maelezo haya yanasawiri na kuakisi vizuri maudhui ya umaskini yanayotokana ufafanuzi wa mtaa huu pamoja na mandhari ya nyumbani kwa kina Bahati.

Katika mandhari yaya haya tunaelezwa kwamba ulipotimia wakati wa Bahati kuposwa na Idi alirudi nyumbani kwao Selea na matayarisho ya kupokea posa na harusi yalifanyika hapo. Inasimuliwa kwamba mamake Bahati, Cheusi, alitaka sana shoga yake kwa jina Bi. Mvita awe mstari wa mbele katika maandalizi haya. Akafika. Msimulizi anaendelea kwa kusema kwamba huyu Bi. Mvita:

> "*... alipenda kuendesha arusi kwa mila za kizamani za Kiswahili ambazo zilihitaji mambo mengi ya kufanya. Chini ya uongozi wake Bahati hakuwa na hiari ila kufuata maagizo yake.*" (Uk. 82)

Maelezo haya yanadhihirisha maudhui ya utamaduni. Kwa mujibu wa ufafanuzi huu, ni dhahiri kwamba kulikuwa na mila za kitamaduni ambazo zilihitajika kufuatwa katika sherehe za arusi miongoni mwa wanajamii wa Uswahilini na kwamba mila hizi zilihitaji ada nyingi kama vile unyago kufanywa kabla ya ndoa kufungwa. Bi. Mvita anasimamia masuala ya kitamaduni vizuri kabla ya kumwasilisha Bahati kwake Idi ili waoane.

#### 4.1.2.5 Nyumba ya Idi Vibyongoni.

Maudhui hufasiliwa kuwa ni jumla ya mambo yashughulikiwayo kwenye kazi ya fasihi (Mbatiah, 2010). Maudhui ya uozo na biashara haramu yanajitokeza kupitia ufafanuzi wa mandhari ya mtaa wa Vibyongoni. Inasimuliwa kwamba Bahati alifululiza moja kwa moja mpaka mtaa wa Vibyongoni ambapo Idi alikuwa akiishi. Huu ulikuwa wakati baada ya wao kukutana awali na kutokubaliana kuhusu nia ya Idi kwamba Bahati "ampende" Mzee Mwinyi ili wanufaike na utajiri wake.

Idi alikuwa akitafuta njia bora ya kumlaghai Mzee Mwinyi mali yake kupitia kwa Bahati. Hata hivyo, Bahati alikataa. Kisa hiki kilimuudhi sana Idi na kumrejesha Bahati kwao akiwa na hasira nyingi; jambo ambalo halikumfurahisha Bahati kwa vile alimpenda Idi sana. Safari hii anayoichukuwa kwenda kwa Idi Vibyongoni ni kwa sababu anaamua na liwe liwalo hawezi akampoteza Idi wake. Angemsaidia kwa njia zozote zile hata kama ni kumlaghai Mzee Mwinyi mali yake.

Bahati anapofika pale Idi anacheka kicheko cha kejeli na kumnong'onezea kwamba amekuja kuomba msamaha na kukubali kushirikiana naye kwa hali na mali. Bahati anatikisa kichwa, ishara

ya kukubaliana naye. Ndipo Idi anamshika na kumtupa kitandani na kisha wakafanya mahaba kimya kwa kitambo (uk. 33). Matukio haya yanachimuza maudhui ya uasherati ambao unaendelezwa na wahusika hawa wawili katika mandhari haya.

Siku moja Idi akiwa katika nyumba yake Vibyongoni akihesabu pesa ambazo alikwimshalaghai Mzee Mwinyi kufikia wakati huo. Punde mtoto wa kiume akabisha mlango na alipoingia kwa haya akamkabidhi Idi barua kutoka kwake Bahati, barua yenyewe ilikuwa ya utani tu. Kwamba Bahati alikwishapanga arusi na Mzee Mwinyi na Idi hakupaswa kuingilia maisha yake tena. Alipoisoma barua ile, kwa vile hakujua ni ya utani, inasimuliwa kwamba:

> "*Idi alipiga kelele huku akishindilia risasi katika bastola yake ya magendo* ..."
> (Uk. 60).

Maelezo haya yanadhihirisha kwamba kulikuwa na biashara haramu ya magendo iliyokuwa ikiendelea kwenye janibu hizi za Vibyongoni. Kwa hali hiyo, maudhui ya uozo unaoambatana na biashara haramu yanajitokeza moja kwa moja kupitia kwa ufafanuzi wa mtaa wa Vibyongoni.

#### 4.1.2.6 Mandhari ya Benki.

Idi alimdanganya Mzee Mwinyi kwa muda mrefu jinsi Bahati alivyompenda na kwamba angekuja jioni ile. Kwa ushauri wa Idi, Mzee Mwinyi alimpa hundi ya shilingi elfu ishirini ya kufurahisha Bahati. Alipoipokea hundi ile Idi alifululiza hadi kwa kina Bahati na kumchukua baada ya chamcha alichokipata kwa Mzee Mwinyi. Walipofika benki,

> *"Makarani wawili, vijana waliokuwa kwenye chumba cha kioo walipomwona amefuatana na msichana nao wakamuamkia huku wakikohoa. Karibu watu wote katika ile benki walimjua Idi ...*" (Uk. 44).

Kwa mujibu wa maelezo haya ya mandhari ya benki, ni dhahiri kwamba maudhui ya kazi yanajitokeza. Wapo wafanyikazi kwenye benki wanaowahudumia wateja walagai kama Idi.

#### 4.1.2.7 Ukele.

Inasimuliwa kwamba baada ya Idi kumzungusha Mzee Mwinyi barabarani anamchosha mno. Hatimaye, hamfikishi kwa kina Bahati maeneo ya Selea. Badala yake, wanaghairi nia kuelekea Ukele mahali ambako Mwinyi anamiliki jumba la kifahari. Wanapokuwa garini wanapitia Tafuteni kisha katikati ya misitu na kutokea upande wa makonde ya karibu.

Msimulizi anaeleza kwamba, wanapofika Ukele wanavua nguo zao na kujitumbukiza majini. Wanaogelea na kurushiana maji kama watoto wadogo. Baadaye Idi anadai kwenda haja. Anatoka majini na kuingia nyumbani akifichua chupa yake ya mvinyo na kupiga mafunda ya haraka. Anafuta mdomo na kutafuna chembe ya karafuu kubabaisha harufu kwa sababu Mzee Mwinyi hakupenda harufu ya pombe. Hatimaye, anarudi majini (uk. 7). Maelezo ya mandhari ya Ukele yanachimuza maudhui ya unafiki, ulevi pamoja maisha ya starehe na ufahari unaoambatana na ukwasi.

#### 4.1.2.8 Mandhari Kiwakati.

Mandhari ya kiwakati pia yanajitokeza katika riwaya ya *Kiu*. Mifano ya mandhari haya ni pamoja na: ‘Siku ya tatu’, ‘Miaka mitano’ na ‘Miaka sita’. Mpito wa wakati wa siku ya tatu unasimuliwa kwa njia ifuatayo:

> “*Siku ya tatu, mnamo saa nne za asubuhi Bahati alishikwa na hamu ya kutaka kumwona Idi*.” (Uk. 30).

Kwa kuangalia maelezo haya ya mandhari kiwakati yatusawiria picha maalumu ya wakati ambapo tukio hili lilitendeka. Kwa hali hiyo, maudhui ya mapenzi yanaibuka. Kinachomsumbua na kumpa mwashawasha Bahati wakati unaorejelewa ni kiu au hisia za mapenzi kwa Idi. Ana mahangaiko haya kwa sababu ya namna walivyokuwa wameachana siku chache zilizotangulia. Walikuwa

wameachana katika hali ya mgogoro mkubwa kwa sababu Idi alimtaka Bahati ajifanye kampenda Mzee Mwinyi ili wamlaghai mali yake; tendo ambalo hakuliridhia.

Kipindi cha miaka mitano kinarejelewa na Bahati anapomhadithia Mwajuma masaibu yaliyomfika kwenye ndoa yake na Idi. Anamsimulia kwamba:

> "*Miaka mitano ikapita ... na miaka mitano si wakati mfupi kwa mwanadamu ambaye kila nukta ya uhai wake umejaa vituko vya namna kwa namna.*" (Kur. 94-95)

Maelezo haya ya mandhari ya wakati yanapoangaziwa, inathibitika kwamba Bahati na Idi walioana miaka mitano iliyopita. Hata hivyo, maisha kwenye ndoa yao yalijaa masaibu mengi. Idi anabadilika na kuingilia ulevi, anasa, uasherati na fujo. Ndoa yao ikakosa amani. Kwa hali hiyo, masimulizi haya ya mandhari kiwakati yanachimuza maudhui ya ndoa, ulevi, anasa na uasherati pamoja na ugumu wa maisha yanayoambatana hali hizi.

Isitoshe, inasimuliwa kwamba miaka sita iliyopita babake Bahati, Jaku, alielekea upande wa Kongo na kumwachia mkewe majukumu ya malezi ya Bahati. Tunafahamishwa kwamba:

> *"Mambo ya Jaku hayakuwahi sikika tena mpaka ripoti zilipofika baadaye kwamba alishikwa huko Kongo na kufungwa miaka sita gerezani kwa tuhuma za kupatikana na vipusa."* (Uk. 29)

Ufafanuzi huu wa mandhari kiwakati unadhihirisha maudhui ya mapuuza upande wa mzazi wa kiume, Jaku, pamoja na maudhui ya uwindaji haramu.

Kwa ujumla, riwaya zote mbili, *Kiu* na *Kidagaa Kimemwozea*, zimeonyesha kuyasawiri mandhari ya aina zote mbili, yaani mandhari ya kiwakati na mandhari ya kimaeneo. Aina za mandhari ambazo Wamitila (2008) anaaziita mandhari ya kihistoria na mandhari ya kijiografia, mtawalia. Mandhari ya kihistoria yameonyeshwa kuakisi kipindi maalumu cha wakati pamoja na matukio ya kihistoria kama vile vita vikuu vya dunia na enzi ya ukoloni. Mandhari ya kijiografia nayo, kama

aelezavyo Wamitila (2008), yameonyeshwa kusheheni ushabihikweli. Hali hii ina maana kwamba waandishi wa riwaya teule wameyatumia kuibua ukweli au hali halisi za maeneo yanayotumiwa kuwasilisha maudhui.

Ingawa riwaya zenyewe ni bunilizi za kisanii, matumizi ya mandhari haya kwenye tungo hizi mbili yamechangia kuzipa riwaya hizi uaminifu kwa sababu masuala yanayoibuliwa kwenye kila mandhari maalumu yana uhalisia wa kusadikika. Ni masuala yanayowapitikia wanajamii kila uchao katika hali zao za maisha. Kwa hivyo, wanariwaya hawa, ijapokuwa wanatunga riwaya zao kwenye vipindi tofauti vya wakati, wamefaulu kuyatumia mandhari kuwasilisha ujumbe wao kupitia usukaji wa maudhui yanayoingiliana na kuakisi vizuri na maeneo yaliyolengwa. Kwa njia hiyo, mandhari yanachangia ukuzaji wa ujumbe unaowasilishwa na riwaya zilizochanganuliwa katika sehemu hii. Sehemu inayofuata inachanganua na kujadili mandhari yanavyotumiwa na wanariwaya hawa katika uviringaji na ujenzi wa sifa za wahusika katika tungo zao.

### 4.2 Mandhari Yajengavyo Sifa za Wahusika.

Sifa za wahusika aghalabu huchangia kumtambua na kumpambanua mhusika fulani kwa urahisi. Sifa hizi mara nyingi hubainisha uraibu wake, mienendo au hata hulka yake kwenye kazi ya fasihi inayohusika. Imethibitika kwamba mandhari pia yanachangia namna ambavyo wahusika fulani wanasawiriwa. Vijisehemu vifuatavyo vimetumiwa kuchanganua na kujadili riwaya moja baada ya nyingine, tukianza na ujenzi wa sifa za wahusika katika *Kidagaa Kimemwozea*.

#### 4.2.1 Mandhari Yajengavyo Sifa za Wahusika kwenye *Kidagaa Kimemwozea.*

Mandhari yana uamilifu adhimu katika kuwapa wahusika sifa fulani (Wamitila, 2002). Kwa kiasi fulani, mahali na wakati ambapo mhusika hujikuta hudokeza na huathiri usawiri wa sifa zake. Ni kutokana na usuli huu ambapo utafiti uliangazia suala hili ili kubaini iwapo mahali na wakati katika

riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* unachangia ujenzi wa sifa za wahusika wake kama vile: Mtemi Nasaba Bora, Mwalimu Majisifu, Bi. Zuhura, DJ, Amani, Imani, Majununi, Wauguzi, Dora, Askari, Wafanyikazi wa Mtemi pamoja na Fao na Dadake.

#### 4.2.1.1 Mtemi Nasaba Bora.

Mtemi Nasaba Bora ndiye mhusika mkuu katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*. Ndiye kiongozi wa eneo la Sokomoko au Mtemi kama anavyojulikana miongoni mwa Wanasokomoko. Nasaba Bora ni mumewe Bi. Zuhura na babake Madhubuti na Mashaka. Mandhari anuwai yamechangia ujenzi wa sifa zake. Mathalan, mandhari ya kasri lake, gari lake, wizara ya ardhi alipokuwa akifanya kazi, barabarani na msituni anamojiulia.

Mtunzi anaweza kusawiri mandhari kisitiari kuhusu yale yanayomhusu mhusika, matukio na mengine. Hii ina maana kuwa mandhari yanaweza kutumika kama sitiari yenye uwezo mkubwa wa kuibua maana fiche na mtunzi (Wamitila, 2002). Tunaarifiwa kwamba kasri la Mtemi Nasaba Bora lilikuwa limechafuka mno, halikuwa limelengetwa ua kwa miaka mingi na kwamba mfanyikazi yeyote aliyejaribu kulengeta au kusafisha boma hili alifutwa kazi mara moja bila notisi. Kwa mujibu wa Mtemi Nasaba Bora mwenyewe:

> "*Sio kwamba nauchukia usafi. Lakini ni hatari sana kuwa safi kupindukia. Mtu anahitaji uchafu kiasi*." (Uk. 15).

Uchafu unaozungumziwa hapa umetumika kisitiari kwa maana kwamba Mtemi Nasaba Bora alikuwa mwovu. Kwa mujibu wa TUKI (2019) uovu ni hali ya kutenda mabaya. Mtemi alitenda maovu mengi kama kuua Chichiri Hamadi na kumwibia mamake Imani shamba lake na hivyo basi alitaka matendo haya yafichike na yeyote aliyetaka kuyaangazia alipata vitisho, kifo na hata kufutwa kazi. Jinsi alivyowafuta kazi wafanyikazi wake waliojaribu kulinadhifisha kasri lake. Kwa hivyo, uchafu wa kasri lile na kuishi kwa Mtemi Nasaba Bora katika kasri hilo kunaoana vyema

na tabia zake chafu chafu (maovu) jinsi zinavyojitokeza kwenye riwaya hii. Mandhari haya yanathibitisha uovu kama mojawapo ya sifa zake mbaya.Kwa hivyo Mtemi alikuwa mwovu.

Kwenye mandhari ya ukumbi wa Kasri la Mtemi Nasaba Bora, tunachorewa taswira ya makochi yayoachwa na Majununi yakiwa yamechanikachanika. Barabara ya kuelekea huko kwenye kasri pia inadhihirishwa kuwa ni mbovu. Nyumba yenyewe nayo imeandikwa andikwa kwenye kuta na wanawe Mtemi. Tunasimuliwa,

> *"Virukia vya madirisha vimepasukapasuka tangu Mtemi Nasaba Bora alipopata urithi wa kasri lile ... makochi yamechanikachanika na pamba kutawanyika. Buibui na utandabui katika kila pembe ya kasri, watoto walikuwa wamechora ukutani kwa makaa na kuandika maneno yasiyosomeka.*" (Uk. 15)

Kupitia maelezo haya ya mandhari ya ukumbi wa kasri tunapata kuelewa kwamba Mtemi Nasaba Bora alikuwa mwenye mapuuza. Mwenye mapuuza ni mtu ambaye hajali wala hatilii maanani jambo ambalo anapaswa kulitenda. Mtemi Nasaba Bora hakutilia maanani usafi wa ukumbi wa kasri alilokuwa akiishi ndiyo maana mazingira yake yalikuwa ya kuchukiza hivyo.

Vilevile, mapuuza yake yanajitokeza pale ambapo hata gari lake lenyewe lilikuwa mkweche na hajali, jibwa lake ni gonjwa linahitaji matibabu na hana wakati wa kulitibu. Hata maegesho yenyewe ya gari yanaonyeshwa kuchakaa kama ielezavyo sauti ya msimulizi,

> *"Mwenyewe Mtemi alikuwa amesimamia fundi wa gari aliyekuwa amefungua mbele ya gari* [mkweche] *anabambanyabambanya katika injini, katika maegesho ya gari mafuta meusi yalikuwa yamezagaa chini kote. Maegesho yenyewe yalikuwa ni kibanda kilichoezekwa mabati yaliyovuja kila mvua iliponyesha karibu na maegesho ya gari palikuwa na baki la tingatinga aina ya Massey Fergusson nyasi zilikuwa zimeiotea mahali liliposimama, magurudumu yote yalikuwa yameng'olewa na wezi ... majibwa matatu yaliyokuwa yamefungwa minyororo shingoni karibu na aliposimamia Mtemi Nasaba Bora yalibweka kwa hamaki. Mmoja wa majibwa yale alikuwa mweupe na mwenye madonda yaliyoshamiri mwili mzima*. (Uk. 20)

Tunaelezwa kwamba Mtemi Nasaba Bora alikuwa karani katika enzi za ukoloni. Baadaye, aliingia katika Wizara ya Ardhi na Makao baada ya Tomoko kupata uhuru na ni katika mazingira haya alipokuwa akifanyia kazi ndipo mwandishi anasema,

> *"... ni huko ndiko alikojifunza mengi zaidi, mbali na kuambukizwa yale maradhi ya kufichaficha faili za watu ili kujipatia mlungura ... alitengeneza faili barabara ili zimfae yeye."* (uk. 13)

Kwa mujibu wa maelezo haya tunapata kufahamu kwamba Mtemi Nasaba Bora alikuwa fisadi na laghai. Ufisadi wake unajitokeza pale ambapo anapokea hongo kutoka kwa watu waliohitaji huduma kwenye wizara alikofanyia kazi. Ikumbukwe kwamba hapo ndipo faili zote za ardhi zilipatikana na kuhifadhiwa na hata hatimiliki za mashamba kutolewa kwa umma. Nao ulaghai wake unajitokeza pale ambapo alikuwa akibadili faili za watu ili kujiundia hatimiliki ghushi na kuwapokonya mashamba yao jinsi alivyomfanyia babu yake Amani kwa jina Chichiri Hamadi. Ulaghai ni hali ya kushawishi au kupumbaza mtu kwa hila ili kumdanganya (TUKI, 2019). Ufisadi nao ni upokeaji au utoaji wa hongo au hata wizi wa mali katika mashirika ya serikali. Mandhari haya na shughuli muhimu zinazotekelezwa humo yanaonyeshwa kuchangia pakubwa katika kukuza sifa za Nasaba Bora kama laghai na fisadi. Kabla ya kuja hapa, Nasaba Bora hakuzijua mbinu hizi. Yamkini hii ndiyo maana mwandishi anasema, *"... huko ndiko alikojifunza*" tabia hizi (uk. 13).

Mtemi Nasaba Bora anajitokeza kama kiongozi mbinafsi. Ubinafsi ni ile hali ya mtu kujifikiria na kujipenda yeye mwenyewe (TUKI, 2019). Sifa hii inadhihirika wazi pale ambapo miundo misingi muhimu yote inapewe jina la Mtemi Nasaba Bora. Mwandishi anaeleza kwamba,

> *"Shule ya bweni katika eneo la Sokomoko lilipewe jina la Mtemi Nasaba Bora, zahanati iliyoko Sokomoko iliitwa Zahanati ya Nasaba Bora. Daraja lililokuwa katika Mto Kiberenge lilijulikana kama Daraja la Nasaba Bora. Uwanja wa kandanda uliitwa Uwanja wa Nasaba Bora na hata shule ya msingi mojawapo*

> *iliitwa Shule ya Msingi ya Nasaba Bora na hata kulikuwa na fununu kwamba Mto Kiberenge ulikuwa katika hatari ya kugeuzwa jina wakati wowote."* (Uk. 27)

Unaosimuliwa hapa ni ubinafsi mkubwa kwa sababu kulikuwa na watu wengine wengi ambao pia majina yao yangetumika. Mfano mzuri ni shujaa Matuko Weye aliyeenda kupigania Uingereza katika Vita Vikuu vya Pili vya Dunia au Chwechwe Makweche ambaye alikuwa mchezaji kandanda hodari katika timu ya taifa la Tomoko, Songoa FC. Inasemekana Chwechwe Makweche aliwahi kufunga bao la ushindi kwenye mchuano kati ya Songoa FC na Meza Wembe FC kutoka Wangwani. Hata hivyo, Nasaba Bora alikuwa akijifikiria tu yeye mwenyewe na hivyo basi kutaka jina lake litumike kila mahali jinsi inavyothibitika kwenye dondoo hilo.

Mtemi Nasaba Bora anapotoka kwenye Uwanja wa Nasaba Bora baada ya kuongoza sherehe za Siku Kuu ya Wazalendo, anaingia kwenya gari lake na kuanza safari ya kuelekea kwake. Barabarani, anampata mwanamke mjamzito ambaye pia anatoka kwenye sherehe hizo na anajifungua kando ya barabara bila msaidizi. Msimulizi anasema kwamba,

> *"Mtemi Nasaba Bora alipofika karibu naye Bi. Zuhura alimwomba mumewe asimamishe gari wamsaidie yule mjamzito. Bwana Mtemi Nasaba Bora alikenua mdomo na kumwambia Bi. Zuhura, "Wacha upuuzi.*" (uk. 74)

Mienendo kama hii katika mandhari haya hatarishi yanadhihirisha kwamba Mtemi Nasaba Bora alikuwa hana utu. Utu ni hali ya kuwa na tabia zinazolingana na hadhi ya mtu au ubinadamu. Binadamu yeyote mwenye utu angalisimamisha gari na kutafuta njia ya haraka ya kumfikisha mwanamke yule hospitalini haraka iwezekanavyo na siyo kumpita katika hali ile ambayo kwa kiasi kikubwa ilihatarisha maisha yake na mwanawe. Mandhari ambayo yangechangia ukuzaji wa utu kwa anayejali, yametusaidia pakubwa kutuonyesha kwamba si wote wenye utu jinsi inavyopaswa kuwa na kwamba Mtemi Nasaba Bora ni mfano mzuri wa watu kama hao.

Jioni moja, Amani anatoka kwenye Zahanati ya Nasaba Bora baada ya kumwona daktari. Huu ulikuwa wakati baada ya kupigwa kitutu na Mtemi Nasaba Bora alipompata kwenye chumba chake cha kulala na mkewe. Mtemi hakutaka kujua ni nini kilichompeleka Amani mle chumbani. Badala yake, kwa ghadhabu, alimrukia kwa bunduki ya mrao na kumpiga akapoteza fahamu. Kisha akambeba na kumtupa kando ya barabara akiwa hoi. Wasamaria wema ndio waliompeleka zahanatini. Baada ya kupata nafuu alitoka kule na alikuwa akirejea tu kwa miadi ya daktari. Siku hii akiwa barabarani akirudi kwa Mwalimu majisifu alikohamishwa na Imani, barabarani *Nissan Sunny* ya Mtemi Nasaba Bora ilimpita, ndani yake alimwona Mtemi Mwenyewe na Msichana aliyemjua kwa jina Lowela. Mandhari ya gari lile linachimuza sifa ya Mtemi Nasaba Bora kama mwasherati anavyoeleza msimulizi kwamba,

> *"Nissan Sunny ya Mtemi ilimpita Amani punde, Mtemi alifululiza kuendesha gari, kashika usukani kwa mkono mmoja huku mwingine kauzungusha kwenye shingo ya janajari moja lililomwegemea begani, hapo ndipo Amani alipobaini kwamba janajike lile lilikuwa Lowela Binti Maozi."* (Uk. 144).

Lowela hakuwa mkewe Mtemi Nasaba Bora bali ni Bi. Zuhura. Kwa hivyo, kumbeba kwenye gari lake na zaidi ya hayo kumshika kimahaba jinsi alivyofanya garini ni ishara ya kujihusisha katika mapenzi nje ya ndoa. Huku ni kuendeleza na kujihusisha katika uasherati. Hivyo basi mandhari haya yanadhihirisha Mtemi Nasaba Bora kuwa ni mwasherati.

Baada ya Mtemi Nasaba Bora kufikwa na uasi kutoka kwa mwanawe Madhubuti, hila zake kugundulika na kuanza kuandamwa na maadui wake kama Gaddafi na majambazi wengine aliowatia mbaroni bila sababu maalumu pamoja na wadeni kuanza kumdai kila kuchao alianza kuhaingaika na kuwa na mafadhaiko moyoni, mafadhaiko ambayo yalichangia Mtemi kuamua kujiangamiza. Mwandishi anasema kwamba,

> *"Siku isiyokuwa na jina ikafika pale wasasi waliokuwa kwenye gongo la msitu walipolikuta kimba cha mtu kimeoza na kuozeana kikining'inia kama bembea mkuyuni. Mwendazake alitambulikana kwa mkanda wake (kuwa alikuwa Mtemi Nasaba Bora)"* (uk. 159)

Mandhari haya ya msituni ambapo mwili wa Mtemi Nasaba Bora ulilipatikana ukiwa unaning'inia kwenye mti wa mbuyu ni ishara kwamba Mtemi Nasaba Bora alipoteza matumaini ya kuishi hivyo akaamua kujitoa uhai. Kwa hivyo, hali hii inadhihirisha Mtemi Nasaba Bora alikuwa ametamauka. Sifa yake ya kuwa mkosa matumaini inajitokeza waziwazi kwenye mandhari haya.

#### 4.2.1.2 Mwalimu Majisifu.

Mwalimu Majisifu ni nduguye Mtemi Nasaba Bora. Marehemu baba yao alikuwa kasisi. Mkewe Mwalimu Majisifu alikuwa Dora. Alisoma mpaka nga'mbo na kurudi Sokomoko akiwa na digrii mbili kutoka katika vyuo vikuu ambavyo majina yao hayangeweza kutamkika kwa urahisi na wenyeji. Mandhari ya nyumba ya Mwalimu Majisifu yanaelezwa kuwa ndani mwake mlikuwa na vitu kadhaa vya thamani. Msimulizi anaeleza,

> *"palikuwa na makochi, vibweta, kabati na kila aina ya samani za kupendeza. Kadhalika alikuwa na vyombo vya kisasa vya tafrija kama vile video-kaseti, runinga, video, CD-changer na mengineo"* (uk. 29)

Mandhari yanayosimuliwa hapa yanadhihirisha kwamba Mwalimu Majisifu alikuwa tajiri. Tajiri ni mtu mwenye mali nyingi (TUKI, 2019). Vitu vyote vya thamani kubwa alivyokuwa navyo Mwalimu Majisifu ni ishara ya ukwasi wake.

Vilevile, katika mandhari haya tunaelezwa kwamba kwenye jiko la Mwalimu Majisifu palikuwa na vitu vifuatavyo:

> *"palikuwa na jokofu lililojazwa chupa za vileo anuwai; si Tusker, si Vodka, si Pilsner, si Kilimanjaro, si Heineken na Guiness."* (uk. 29)

Kwa mujibu wa maelezo haya, ni bayana kwamba Mwalimu Majisifu alikuwa mlevi. Alikuwa akitumia vileo hivi kwa sababu hakuna vile vingepatikana kwake ilhali si mraibu wavyo. Ndiyo maana hata tunaelezwa kwamba alikuwa akilewa na kushindwa kuhudhuria vipindi vyake shuleni Nasaba Bora. Maelezo ya Mashaka yanadhihirisha haya alipokwenda kwake kumpelekea barua ya mwaliko kutoa mhadhara Chuoni Mkokotoni, Wangwani.

> *"... tunakuona darasani kwa nadra sana"* (uk. 47)

Mwalimu Majisifu anapofika nchi ya Wangwani katika Chuo Kikuu cha Mkokotoni, tunaelezwa kwamba wanafunzi pamoja na wahadhiri walikuwa wameketi ukumbini tayari kusikiliza mihadhara kutoka kwake. Baada ya kukaribishwa kwa makofi tunaelezwa kwamba alishikwa na wasiwasi mwingi.

> *"Kijasho chembamba kikaanza kumtoka kisha karatasi zile alizotoa kwenye mkoba wake zikatota akanyanyuka na kupanda jukwaa ... Aliona macho mengi, pengine elfu au zaidi yakimwangalia. Karatasi alizokuwa nazo mkononi zikaanguka na kutawanyika."* (Kur. 122-123)

Maelezo haya ni ishara kwamba Mwalimu Majisifu aliingiwa na woga pamoja na wasiwasi mbele ya hadhira yake. Hivyo basi, mandhari haya ya ukumbi chuoni Mkokotoni yanadhihirisha wazi mchango wa mandhari katika kukuza sifa za mhusika huyu kama mtu mwoga na mwenye wasiwasi.

#### 4.2.1.3 Bi. Zuhura.

Bi. Zuhura ni mkewe Mtemi Nasaba Bora na mamake Mashaka na Madhubuti. Mandhari ya nyumbani kwake yamechangia katika kukuza sifa zake. Kama anavyoeleza msimulizi, ipo siku ambayo mumewe aliondoka kwenda Songoa kuomba muda wa kulipa madeni yake. Ikasadifu kwamba siku hiyo, Mashaka, mwanawe alizidiwa ugonjwa wake akaanza kuzua rabsha nyumbani. Ilibidi Bi. Zuhura kumwita Amani kwake aje amsaidie kumfungia chumbani mwake. Baada ya



Mount Kenya University

msaada huu, kwa vile ulikuwa ni usiku alimrai Amani kulala katika jumba lake ili endapo rabsha za Mashaka zitazidi amsaidie. Amani alikubali na kulala kwenya kiti. Alipokuwa usingizini punde aligutushwa na mwito wa Bi. Zuhura kutoka katika chumba chao cha kulala. Amani aliamka haraka na kuelekea mlangoni pa chumba hicho.

*"Hebu ingia ndani,"alisema Bi. Zuhura.* (uk. 130)

Msimulizi anaeleza kwamba Amani aliogopa kuingia. Hata, hivyo alipiga moyo konde na kuingia mle chumbani. Wakati huo wote Bi. Zuhura alikuwa kasimama karibu na kitanda, kajivika gauni lake la kulala lisilojua *"kuficha vya kufichwa."* (uk. 131)

Matukio haya yanayojiri usiku kwenye chumba cha kulala yanadhihirisha wazi kwamba lengo la Bi. Zuhura lilikuwa bayana. Alikuwa na uchu wa mapenzi kwa Amani japo alikuwa anasingizia uwepo wa kitu chini ya kitanda chao. Kwa hali hiyo, tunapata kujuzwa sifa zake kwamba alikuwa mwenye uchu wa mapenzi na mdanganyifu. Udanganyifu ni kumfanyia mtu matendo ambayo unajua ni ya uongo. Bi. Zuhura alijua vizuri sana hakuna kitu cha kumwitia Amani chumbani mwake ila huu ulikuwa mtego tu ili aingie mle amtimizie haja yake ya kimwili. Asingalifika kwa wakati Mtemi Nasaba Bora mambo yangekuwa mengine. Huenda angemnajisi Amani kwa kutumia hila zake.

Usiku mmoja Amani anakiokota kitoto mlangoni pake. Ilipotimia asubuhi, alikipeleka kitoto kile kwake Bi. Zuhura. Msimulizi anatueleza kwamba,

> *"Bi. Zuhura alimwamuru mjakazi kuyatwaa maziwa kutoka katika jirafu na kuyatia kwenye chupa ya kunyonyeshea watoto iliyokuwa shubakani."* (uk. 39)

Kwa mujibu wa maelezo haya, inathibitika wazi kwamba katika jumba la Bi. Zuhura na Mtemi Nasaba Bora palikuwa na jirafu ambalo lilihifadhiwa maziwa. Pamoja na hayo, Bi. Zuhura alikuwa amehifadhi chupa alizonyonyeshea wanawe walipokuwa wadogo. Hii ni ishara kwamba Bi.

Zuhura alikuwa mwajibikaji. Kuwajibika ni kutenda jambo la lazima au kukosa hiari katika kutenda jambo (TUKI, 2019). Bi. Zuhura aliwajibika kuhifadhi maziwa kwenye jirafu. Aliwajibika kutunza chupa za kunyonyeshea watoto wake pamoja na kuwajibika kukipa kile kitoto maziwa kinywe ingawa hakujua kimetolewa wapi.

**4.2.1.4 DJ.**

Hata baada ya Imani kukatazwa kunywa maji ya Mto Kiberenge na DJ, msimulizi anaeleza kwamba alijasirika na kuchota maji yale kwa vitanga vyake vya mkono na kupiga funda na kwamba aliendelea mpaka akakata kiu alichokuwa nacho.

*“Mazee usinywe maji haya jo,” DJ alimwambia, “ni haramu jo.”* (uk. 6)

Maelezo haya yanadhihirisha kwamba maji yanayozungumziwa hayakupaswa kunywewa na mtu yeyote na ndiyo maana DJ anapomwona Imani akiyanywa anashangaa na kutoka majini mbio ili amkanye. Maji yenyewe yalikuwa tu ya kuwanywesha ng’ombe na kupigia mbizi pekee. Hata wakati Imani na Amani walipofika kando ya Mto Kiberenge, walipata ng’ombe wakiyanywa ilhali kina DJ wakipiga mbizi tu. Kutoka kwake DJ majini mbio kwa mshangao na kumkanya alipomwana Imani akinywa maji yale ni ishara ya jinsi alivyokolea kwenye utamaduni ulioharamisha unywaji wa maji yale. Kwa hivyo, mandhari haya yanatujengea sifa ya DJ kwamba alikuwa mtamaduni. Utamaduni ni mila, asili, jadi na desturi za kundi la jamii fulani (TuKI, 2019). Utamaduni ndio uliowafunga kina DJ kutokunywa maji ya Mto Kiberenge na kuyatumia kwa kuogelea na kunywesha ng’ombe jinsi Amani na Imani walivyowapata wakifanya.

**4.2.1.5 Amani.**

Amani ni kijana kutoka Ulitima. Ndiye mjukuu wa Chichiri Hamadi na amu yake alikuwa akiitwa Yusufu Hamadi. Ni mtoto wa mama mmoja mjane ambaye jina halijatajwa kwenye utungu huu.

Baada ya Amani kuajiriwa kazi ya kutunza na kukamua ng'ombe nyumbani kwa Mtemi Nasaba Bora, msimulizi anatuchorea picha ya makazi anayopewa kuishi. Inasemekana kwamba palikuwa mahali ambapo ni kibanda. Kibanda chenyewe kiliezekwa paa la nyasi na kuta zake zilikandikwa kwa udongo. Sakafu nayo ilikuwa na vibonde vibonde na kutalizwa kwa samadi ya ng'ombe. Mlango ulikuwa vipande vya madebe na dirisha la katoni. Zaidi ya hayo, msimulizi anasema kwamba alilalia kitanda cha teremka tukaze na blanketi lilikuwa fupi lenye mianya. Anasisitiza kwamba,

> "*Lakini hakuishi pekee yake ... alikuwa na marafiki wake wa daima, yaani jeshi kubwa la mijipanya. Mijipanya yale yalikatalia pale licha ya juhudi zake ya kuitoa."* (uk. 32)

Kwa mujibu wa maelezo haya, inabainika kwamba huyu ni kijana mstahamilivu. Kuishi katika mazingira kama haya na mijipanya pia kunahitaji stahamala ya hali ya juu. Kustahimili ni ile hali ya kuchukulia mambo mazito bila ya kulalamika. Amani aliishi kwenye mazingira haya kwa muda mrefu bila kulalamikia yeyote alipokuwa akimfanyia Mtemi Nasaba Bora kazi.

**4.2.1.6 Imani.**

Mandhari huwa na wajibu mkubwa kwa vile yanachangia katika kuwajengea wahusika sifa. Wakati na mahali ambapo mhusika hujikuta huathiri sifa zake kwa kiasi kikubwa (Wamitila, 2002). Imani anajikuta katika mandhari mamoja na wanandoa, Mwalimu Majisifu na mkewe Dora ambao walijaliwa watoto wanne. Wadogo wawili ni mapacha, kisha wapo wengine wawili msichana na mvulana. Msimulizi anaeleza kwamba msichana alikuwa na umri wa miaka kumi na saba na kumzidi mnuna wake na mwaka mmoja tu. Watoto wenyewe waliwapa mwalimu Majisifu na mkewe dhiki ya kuwatunza kwa sababu walikuwa wakitoka udenda mdomoni mfululizo na kwenda haja zote; kubwa na ndogo kwenye nguo zao. Nao wale mapacha walizaliwa bila uwezo

wa kutembea. Kutunza watoto wenye ulemavu kama hawa kulihitaji kujitolea na kuwa na moyo. Inasimuliwa kwamba,

> "... *lakini Imani hakujikaza tu kisabuni, alikuwa na imani na ndiye aliyekuwa mtu wa kwanza kuwaonea na kuwatendea watoto hawa kama binadamu.*" (Uk. 30)

Imani alijitolea kufanya kazi ya kulinda watoto hawa wa Dora na Mwalimu Majisifu kwa moyo wake wote licha ya kwamba wote walikuwa na ulemavu. Kwa hali hii, kupitia mandhari haya tunaona juhudi na upendo wa Imani. Katika kuwatumikia watoto hawa, wema wa Imani unachimuzwa. Alikuwa mwenye bidii, utu na mapenzi ya dhati kwa watoto wanaoishi na ulemavu. Bidii ni ari ya kufanya jambo au jitihada, utu ni matendo yanayolingana na hadhi ya ubinadamu ilhali mapenzi nayo ni hali ya kuingiwa moyoni na kuthamini mtu (TUKI, 2019).

**4.2.1.7 Majununi.**

Majununi alikuwa mlowezi kutoka Uingereza. Mandhari kihistoria na kimaeneo yanatumiwa kuzijenga sifa na uhusika wake kwenye jumuiya ya *Kidagaa Kimemwozea*. Inasimuliwa kwamba alipotua Sokomkoko alijinyakulia ardhi kubwa ya kujengea makazi yake. Msimulizi anaeleza kwamba alikuwa keshasubuhiana na msichana mmoja Mfaransa kwa jina Mitchelle. Makazi yake ya kwanza yalikuwa ni hema ambayo alimwarifu mpenziwe aje aone kutoka Ufaransa. Hata hivyo, alipowasili aliudhika kutokana na taswira ya makazi hayo. Inasimuliwa kwamba aliilalamikia hali hii kwa maneno,

> *"Monsieur Major Noon,"alisema Mitchelle."Nasikitika sana sitakanyaga chini wayo wa mguu wangu. Jenga nyumba wacha ujuba.*" (Uk. 17) Akarudi kwao.

Majununi aliendelea na kujenga nyumba yenye vyumba vinne kisha akamwarifu Mitchelle aje aione. Punde alipowasili alikataa kutoka kwenye ndege na kusema,

"*Monsieur Major Noon, wacha ujuba wewe ile si nyumba*." (Uk. 17).

Hatimaye, Majununi alijenga kasri, ambalo kwa sasa lilikuwa linamilikiwa na Mtemi Nasaba Bora. Alipomwandikia Mitchelle barua tena. Wakati huu alishuka chini kuona jumba lile lakini hakupendezwa na idadi ya vyumba na rangi nyekundu kwenye sakafu. Kwa hivyo, alirudi kwao Ufaransa na kumjulisha Majununi kwamba aoe mwanamke kufu yake.

Kwa kuzingatia maelezo haya, inaweza kusemwa kwamba Majununi alikuwa mvumilivu na mwenye bidii. Alijibidiisha na kuvumilia kumfurahisha Mitchelle kwa hali na mali lakini hakubahatika. Bidii ni jitihada anazofanya mtu ili kufanikiwa katika kila analolifanya. Nao uvumilivu ni hali ya kustahimili taabu au mambo mazito kama inavyoonekana kupitia kwa mandhari yanayotumiwa kuzijenga sifa aali za mhusika Majununi.

**4.2.1.8 Wauguzi.**

Mandhari ya Zahanati ya Nasaba Bora yanatumiwa kusawiri sifa za Wauguzi wakati Amani na Imani wanakipeleka kitoto Uhuru kupata matibabu baada ya kuugua. Wanapofika zahanatini inasimuliwa kwamba wanawapata Wauguzi, *wakifuma fulana na kupiga zohali* (uk. 76). Wanawaomba wakihudumie kitoto Uhuru. Hata hivyo, maombi yao yanagonga mwamba. Wauguzi wanawafanyia bezo na kukataa kukitibu kitoto Uhuru kwa sababu ilikuwa Siku Kuu ya Wazalendo. Hatimaye, wanaamua kutoka nacho huko zahanatini na kitoto hicho kinafariki njiani.

Kwa mujibu wa mandhari yanayosawiriwa, mapuuza na utepetevu wa wauguzi kazini unadhihirishwa. Utepetevu ni ile hali ya kukosa bidii kazini. Licha ya kwamba wanapaswa kuwa watoa huduma msingi na muhimu, Wauguzi waliketi tu na kuendelea kupiga zohali ilhali kitoto kilikuwa kinalemewa na maradhi. Mapuuza yao yanajitokeza pale ambapo wanaendelea kufuma fulana zao badala ya kuhudumia mgonjwa.

#### 4.2.1.9 Dora.

Dora ni mkewe mwalimu Majisifu. Huyu ni mama aliyejaaliwa watoto wanne. Mapacha wawili wachanga pamoja na msichana mkubwa mwenye umri wa miaka kumi na saba. Mvulana anayemfuata ana umri wa miaka kumi na sita. Hata hivyo, ajabu ni kwamba watoto wake wote wanaishi na ulemavu.

Kabla ya wale mapacha kuzaliwa wanandoa hawa walikaa kwa miaka kumi na mitano bila watoto wengine kwa sababu Mwalimu Majisifu hakupenda wale wanawe wawili wa mwanzo kwa vile walikuwa na ulemavu. Alikatisha uhusiano wote na mkewe. Hata hivyo, asemavyo msimulizi,

> *"baridi ilimzidi wakati mmoja akalegeza kidogo kamba ya vikwazo vyake vya kidiplomasia. Ndipo ikasadifu kwamba Dora alipata mimba*" (uk. 31)

Watoto waliozaliwa wakawa mapacha waliokuwa na ulemavu, pia wa kutotembea. Mwalimu Majisifu alitaka kuwatupa majini lakini Dora mkewe alimzuia kwa kusema,

> *"Mtoto ni mtoto hata likiwa bonge la nyama. Nitawalea tu hata kama kwa kuuma meno."* (uk. 31)

Dora anafanya kila jitihada kuwalea wale wanawe akishirikiana na Imani kwa mapenzi ya dhati japo kazi yenyewe ilikuwa ngumu sana. Wakati mwingine kazi ya kuwalea wanawe inamzidia, hususan wakati ambapo Imani anashikwa na kutiwa kwenye seli ya Mtemi Nasaba Bora kwa tuhuma za mauaji ya kitoto Uhuru. Matendo haya kwenye mandhari ya malezi ya watoto wanne wanaoishi na ulemavu yanadhihirisha kwamba Dora ana mapenzi dhati kwa wanawe wenye ulemavu. Kwa hivyo, mandhari haya yanaangaza sifa za Dora kama mama mwenye mapenzi kwa mume na watoto wake wenye ulemavu.

#### 4.2.1.10 Askari.

Seli ya Mtemi Nasaba Bora inaelezwa kuwa ni choo ambacho kilikuwa ni cha umma. Hiki ni chumba chenye harufu kali na ndipo Mtemi Nasaba Bora alipowafungia mahabusu wake. Miongoni mwa watu waliokuwa kwenye seli hii ni pamoja na Amani, Imani na Matuko Weye. Amani na Imani wanakamatwa kwa tuhuma za mauaji wa kitoto Uhuru. Naye Matuko Weye anakamatwa kwa madai ya kuzua rabsha katika sherehe za Siku Kuu ya Wazalendo.

Kwa kuwafungia Amani, Imani na Matuko Weye kwenye choo kimoja kinachovunda kama palipo na mfu, inadhihirisha kwamba Askari walikuwa dhalimu. Isitoshe, wanasubiri Mtemi atoke ndipo wanaanza kuwafanyia "kazi" mahabusu. Askari wanafunga mlango wa seli na kuwanyaka wafungwa makofi bila huruma. Wanawaripua viboko na kuwazaba makonde na mateke mfululizo (uk. 89).

Maelezo ya mandhari haya yanachimuza sifa hasi za Askari kama watu katili, wenye hasira na dhalimu dhidi ya wafungwa. Hapakuwa na sababu za kuwatendea wahusika hawa matendo ya kidhalimu kama haya. Ukatili ni hali ya kutokuwa na huruma, ni kuwa na hasira au ghadhabu ilhali udhalimu ni uonevu au unyanyasaji (TUKI, 2019).

#### 4.2.1.11 Wafanyikazi wa Mtemi.

Msimulizi anatuarifu kwamba punde tu baada ya kukamatwa kwa Amani kwa tuhuma za mauaji ya kitoto Uhuru na kutiwa kwenye seli ya Mtemi Nasaba Bora, Mtemi alipikiwa chai ya mkandaa yenye sukari kidogo na kuletewa na mjakazi. Hapo ndipo alipogundua kwamba zilishapita siku tatu bila kukamwa kwa ng'ombe wake. Msimulizi anatueleza kuwa,

> *"Hakuna hata mfanyikazi mwingine mmoja wa Mtemi aliyetaka kuhusishwa na ukamaji;waliona bora waache kazi kabisa."* (uk. 94)

Bi. Zuhura alilazimika yeye mwenyewe kuwafungulia ndama ili wanyonye mama zao japo alikuwa na wafanyikazi katika boma lake ambao wangefanya kazi hiyo. Iliifikie kiwango cha Bi. Zuhura mwenyewe kuwafungulia ndama wanyonye, ilikuwa bayana kwamba wafanyakazi wale walikaidi agizo lake la kuwa kama wale ng'ombe. Hali hii inadhihirisha kwamba Wafanyakazi hawa walikuwa wakaidi. Ukaidi ni ile hali ya kukosa utiifu au kukosa kutii au kusikiliza ushauri wa mtu (TUKI, 2019).

#### 4.2.1.12 Fao na Dadake.

Amani anaeleza kwamba baada ya kutoka gerezani, aliamua siku moja kwenda kumtembelea rafiki yake Fao. Alipofika huko hakumpata. Hata hivyo alimpata dadake. Msimulizi anaeleza kwamba huyu dada alikuwa msichana aliyekuwa kazaa mtoto na hajaolewa. Hali hii ina maana kwamba alipata uja uzito nje ya ndoa. Dadake Fao na Amani walipokuwa barazani wakizungumza kiliingia kivulana kingine kidogo cha umri wa miaka mitano au sita hivi.

> *"Hiki ni cha nani?" aliuliza Amani.*
> *"Cha Fao," dadake Fao akajibu huku akimkonyezea Amani jicho.* (uk. 37)

Kwa mujibu wa matukio haya kwenye mandhari ya boma la kina Fao, inadhihirika kwamba Fao na dadake walikuwa waasherati. Hali hii ndiyo maana walipata watoto nje ya ndoa. Uasherati waweza kuelezwa kuwa ni tabia ya kupenda kuzini au uzinzi (TUKI, 2019).

### 4.2.2 Mandhari Yajengavyo Sifa za Wahusika wa *Kiu.*

Mandhari ni elementi muhimu ambayo hueleza ni wapi na lini tukio fulani lilifanyika (Wamitila, 2002). Mandhari ni sehemu ambapo matukio muhimu ya msuko hutokea. Vilevile, mandhari aghalabu hutekeleza wajibu mkubwa kwa kuchangia uviringaji na ujenzi wa sifa za wahusika. Baadhi ya mandhari katika riwaya ya *Kiu* ni pamoja na barabarani, Ukele, Selea, Vibyongoni

nyumbani kwake Idi, Chumba cha Kidawa, Chumba cha Tatu, na Buraha. Vilevile, mandhari ya wakati pia yamechangia ujenzi na usawiri wa sifa za wahusika. Vijisehemu vifuatavyo vinajadili dhima ya mandhari hayo katika ujenzi wa wahusika kama vile mzee Mwinyi, Idi, Bahati, Cheusi, na Bi. Mvita katika jumuiya ya *Kiu*.

#### 4.2.2.1 Mzee Mwinyi.

Mzee Mwinyi ndiye mhusika mkuu katika riwaya hii. Mwinyi ni babake Rehema ambaye kwa muda alikuwa akisomea Ulaya. Alikuwa anaishi maeneo ya Ukele. Mhusika huyu inasemakana kwamba alikuwa na mali chungu nzima. Kwa mfano, mandhari ya chumbani mwake, kama anavyoeleza msimulizi,

> " *chini ya nyayo zake alikuwa amekanyaga zulia zuri ambalo thamani yake ingetosha kumfariji maskini kwa siku na miezi"* (uk. 1)

Zaidi ya hayo, mzee huyu alikuwa mmiliki wa gari aina ya Benzi ambalo lilikuwa likiendeshwa na dereva wake kwa jina Idi. Pia, alikuwa na kijakazi kwa jina Mwajuma ambaye ndiye alikuwa akishughulikia masuala ya mapishi na unadhifishaji wa jumba lake la kifahari. Msimulizi anatueleza zaidi kuhusu mandhari ya jumba hili kwamba,

> *"Jumba hili kwa ndani pia lilikuwa na pambo zuri la thamani, pembe mbili za faru, bunduki mbili nzuri za kiasili zenye vitako vya mpigo wa visumari vya shaba na dhahabu".* (uk. 9)

Kwa mujibu wa maelezo haya tunawezasema kwamba mzee huyu alikuwa bwanyenye au tajiri. Bwanyenye ni mtu mwenye mali nyingi (TUKI, 2019). Kwa hivyo, mandhari ya jumbani mwake Mwinyi yanasawiri mtu mwenye utajiri mkubwa. Msimulizi anatueleza kwamba katika mojawapo ya kuta za nyumba ya Mzee Mwinyi kulikuwa na picha,

> *"Ilikuwa picha ya mwanamke mwenye sura nzuri aliyeketi juu ya jiwe kando ya kijito cha maji akiwa uchi huku akichana nywele na kutabasamu."* (Uk. 9)

Maelezo haya yanadhihirisha wazi kwamba Mzee huyu alikuwa mkware. Ukware ni tamaa ya kupenda kufanya tendo la kujamiiana kila wakati. Yamkini tabia hii ndiyo ilichangia pakubwa mzee huyu kummezea mate Bahati alipofika nyumbani kwake siku moja akiwa na Idi. Hatimaye, anaishia kumwandama Bahati kimapenzi.

Idi anafanya juu chini kumwaminisha Mzee Mwinyi kwamba Bahati anampenda. Kwa hivyo, mzee huyu, hata bila simile, anachukua hundi ya shilingi elfu ishirini na kumkabidhi Idi ampelekee Bahati kama zawadi. Wakati Idi akiipokea hundi ile wote wawili, yaani Mzee Mwinyi na Idi wapo nyumbani kwake Mzee Mwinyi mwenyewe (Uk. 40).

Kwa kufanya mambo kwa pupa kiasi hiki bila kufikiria, ni ishara kwamba Mzee Mwinyi alikuwa mwenye pupa. Matukio ya awali, Bahati alipoenda kwake, yalikuwa ishara dhahiri kwamba Bahati hakuwa anampenda. Aliona jinsi Bahati alivyoshtuka kumwona. Alivyokataa usuhuba wake. Lakini kwa kukubali kudanganywa na Idi, alitoa hundi haraka na kumkabidhi Idi ampelekee Bahati eti kwa sababu Idi kamwambia kuwa mapenzi kati yake na Bahati yamenoga.

> *"Ati watu husema mapenzi hayakutani, mbona yako na Bahati yamekutana?* (uk. 5)

Pupa ni nia ya kutaka kumaliza au kufikia mwisho wa jambo kwa haraka bila ya umakini. Haya ndiyo Mzee Mwinyi alikuwa akifanya kufuatia kusakamwa na kiu ya mapenzi.

**4.2.2.2 Idi.**

Idi alikuwa dereva wa Mwinyi kwa muda mrefu. Hatimaye, anaishia kumwoa Bahati. Alikuwa akiishi katika Mtaa wa Vibyongoni. Idi ni mhusika mjanja; ujanja wake unadhihirika wakati anapomfanya tajiri wake, Mzee Mwinyi, kuamini kwamba alikuwa akipendwa na msichana kwa jina Bahati. Hata hivyo, lengo lake kuu lilikuwa kumlaghai mzee huyu mali yake.

Baada ya kumshawishi Bahati kumzuzua Mzee Mwinyi kwa mapenzi ya uongo, ipo siku anaenda kwake na kumhadaa kwamba Bahati anahitaji zawadi. Mzee Mwinyi anatoa hundi ya shilingi elfu ishirini na kumkabidhi ili apelekee Bahati. Ingawa anapotoka hapo anamkabidhi Bahati hizo pesa, hii ilikuwa mojawapo ya njama zake za kumlaghai Mzee Mwinyi mali yake kupitia kwa Bahati. Kwa hivyo, mandhari haya yanachimuza sifa za Idi kama Mjanja. Ujanja ni hali ya mtu kuwa na hila au udanganyifu ili ajinufaishe binafsi. Imethibitika jinsi alivyofika kwa Mwinyi na kumdanganya,

> *"Unakumbuka uliniambia nimtafutie Bahati nyumba?"Idi alikumbusha.*
> *"Ee! Ndiyo;je umepata?*
> *"Nimepata moja nzuri kiasi."*
> *"Barabara!" Mwinyi akajibu.*
> *"Thamani yake shilingi elfu ishirini tu." Idi akaongezea.*
> *"Nitolee kitabu changu cha benki."* (uk. 40)

Hatimaye, Mzee Mwinyi anamkabidhi Idi hundi ya shilingi elfu ishirini. Hata hivyo, nyumba yenyewe hainunuliwi.

Baada ya ndoa kati ya Bahati na Idi wanahamia mtaa wa Buraha. Hapa ndipo wanapoishi. Inapotimia miaka mitano katika ndoa, vituko vya Idi vinaanza. Alikuwa akiajiri wafanyikazi na kuwafuta kiholela. Siku moja, akitaka kumfuta kazi mmoja kati ya wafanyikazi hao, anasikika akisema,

> *"Nimetaabika miaka mingi;sitakubali kutaabishwa na paka kama wewe!"* (Uk. 97)

Kwa kuwaajiri na kuwafuta wafanyikazi wake kiholela, Idi anadhihirika kuwa ni mwenye pupa, asiye na shukrani wala subira. Kuwa na pupa ni tabia ya kufanya mambo kwa haraka pasipo makini.

Msimulizi anasema kwamba ipo siku Bahati alimsikiliza mumewe akiimba usiku. Alipoamka na kuchungulia kupitia kwa dirisha, alimwona amekaa juu ya mdomo wa gari ameegemea kioo na chupa moja tupu ilikuwa chini juu ya mchanga chupa nyingine yenye kinywaji; pombe hasa, ilikuwa juu ya mdomo wa gari kati ya mapaja yake (uk. 114). Haya maelezo ya mandhari yanahihirisha kwamba Idi alikuwa mlevi.

Siku zilipita na Bahati akaunda njama na Mwajuma, mmoja kati ya wafanyikazi wao, kwamba angemwambia Idi kwamba anaenda kwao ili aweze kubaini yale ambayo aliwahi kuambiwa na Mwajuma kuhusu mumewe wakati ambapo hakuwa nyumbani. Mpango ukapangika akatoka kuelekea Selea. Ulipofika wakati mwafaka alichukuwa teksi na kurudi kwake Buraha. Alisubiri ishara za Mwajuma kwa vile walikubaliana kwamba Mwajuma angemwashiria wakati mwafaka wa kuingia nyumbani. Ishara ikatolewa. Msimulizi anaeleza kwamba,

> *"Bahati akajitoma uani akampata mumewe na mwanamke mwingine mwembamba, mwenye nywele za shungi utosini. Mumewe alikuwa ameganda kwenye kiuno chake kwa mkono mmoja na mwingine unamimina mvinyo katika bilauri mbili."* (Uk. 147)

Kwa mujibu wa maelezo ya mandhari haya, inathibitika kwamba Idi alikuwa mlevi na mpenda anasa. Ulevi ni hali ya kupotewa na fahamu kwa sababu ya kutumia pombe au dawa za kulevya ilhali anasa ni mambo au hali ya starehe na raha nyingi.

**4.2.2.3 Bahati.**

Bahati ni mkewe Idi na mwanao Cheusi na Jaku. Bahati ndiye anyetumiwa na mumewe Idi kumlaghai Mzee Mwinyi mali yake kabla waoane.

Msichana huyu alilelewa na mamake Cheusi baada ya babake, Jaku, kupotelea Kongo.

Msimulizi anaeleza kwamba, kwa kina Bahati kulikuwa Mtaa wa Selea, ambapo

walikuwa wanaishi katika nyumba ambayo ilikuwa imezeeka sana. Nyumba yenyewe inaelezwa kuwa,

> *"Si kuta, si milango, si paa, vyote vilionekana mfano wa kizee anayeomba mauti ... palikuwa na vibaraza viwili kimoja cha kushoto kimebomoka."* (uk. 18)

Mandhari yanayosawiriwa hapa yanaasharia umaskini ambao wanafamilia hii walikuwa wanapitia. Kwa hivyo, ni vyema kusema kwamba Bahati alikuwa maskini, umasikini ni hali ya kukosa mali na mahitaji muhimu.

Bahati anarejelea kipindi cha miaka mitano anapomhadithia Mwajuma masaibu aliyopitia katika ndoa yake na Idi. Anamwambia kuwa,

> "*Miaka mitano ikapita ... na miaka mitano si wakati mfupi kwa mwanadamu ambaye kila nukta ya uhai wake umejaa vituko vya namna kwa namna."* (Kur. 94-95)

Haya maelezo ya mandhari yanapoangaziwa yanatuonyesha kwamba Bahati na Idi walioana miaka mitano iliyopita na maisha yao kama wanandoa yalijaa masaibu mengi. Idi alibadilika na kuingilia ulevi, anasa, uasherati na fujo. Ndoa yao ilikosa amani. Kwa hivyo, masimulizi haya yanachimuza sifa ya mhusika Bahati kama mvumilivu. Anavumilia mateso katika ndoa yake na Idi.

Msimulizi anaeleza kwamba Bahati alifululiza moja kwa moja mpaka mtaa wa Vibyongoni ambapo Idi alikuwa akiishi. Hii ilikuwa baada ya wao kukutana awali na kutokubaliana kuhusu nia ya Idi kwamba Bahati "ampende" Mzee Mwinyi ili wanufaike na utajiri wake. Idi alikuwa akitaka njia bora ya kumlaghai Mzee Mwinyi mali yake kupitia kwa Bahati. Lakini Bahati alikataa, kisa hiki kilimuudhi sana Idi na kumrejesha Bahati kwao akiwa na hasira nyingi; jambo ambalo halikufurahisha Bahati kwa vile alimpenda sana Idi. Safari hii anayoichukuwa ya kwenda Vibyongoni kwake Idi ni kwa sababu ameamua liwe liwalo hawezi akampoteza Idi wake. Atamsaidia kwa njia zozote zile hata kama ni kukubali kumlaghai Mzee Mwinyi mali yake.

Bahati anapofika nyumbani kwa Idi, Idi anamnong'onezea kwamba anajua amekuja kuomba msamaha na kukubali kushirikiana naye kwa hali na mali. Bahati anatikisa kichwa kama ishara ya kukubaliana naye. Inasimuliwa kwamba,

> "*Ndipo Idi alimshika na kumtupa kitandani na kisha wakafanya mahaba kimya kwa kitambo"* (uk. 33)

Mandhari ya nyumba ya Idi yamewapa mazingira ya siri. Mahali pa kuzini bila kuonekana wala yeyote kujua na hivyo kuikuza sifa hasi ya Bahati kama mwanamke mzinifu. Uzinifu kwa mujibu wa TUKI (2019) ni ukware au tamaa ya kufanya tendo la kujamiiana.

Msimulizi pia anatudokezea kwamba,

> *"Siku ya tatu, mnamo saa nne za asubuhi, Bahati alishikwa na hamu ya kutaka kumwona Idi. Akaingia chumbani mwake (kule kwao Selea) na kutoa picha ya Idi aliyokuwa nayo kisha akakaa kitandani kuitazama. Sura yake Idi ikamwingia moyoni."* (uk. 30)

Kwa mujibu wa maelezo haya tunaweza kusema kwamba mandhari haya ya kiwakati na kimaeneo yamechangia pakubwa katika kutubainishia kwamba Bahati alikuwa akimpenda Idi na kwamba alikuwa hata na picha yake kwao ili kuitazama kila anapompeza. Kwa hivyo, alikuwa mwenye mapenzi ya dhati.

#### 4.2.2.4 Cheusi.

Cheusi ni mamake Bahati na mkewe Jaku. Anaishi Selea na mwanawe Bahati baada ya mumewe Jaku kupotelea Kongo. Inasimuliwa kwamba waliishi katika nyumba duni ambayo ilikuwa imezeeka; milango yenye kelele ikifunguliwa. Ndani ya nyumba yenyewe mlikuwa na mtungi wa maji unaovuja na kata yake ya kifuu cha nazi. Ndani hapakuwa na kiti cha kukalia ila mbuzi ya kukunia nazi. Chai iliyopikwa siku moja asubuhi ilikuwa ya mkandaa. Ilinywewa na mhogo wa

kutokosa (uk. 23). Maelezo haya ya mandhari ya nyumba na chumba hiki yanachimuza sifa ya Cheusi kama maskini.

**4.2.2.5 Bi. Mvita.**

Bi. Mvita ni shoga mkubwa wa Cheusi, mamake Bahati. Msimulizi anaeleza kwamba Bi. Mvita alipenda kuendeleza shughuli za arusi kwa mila za kizamani za Kiswahili na kwamba hakuna vile harusi ya mwanawe ingeendeshwa bila uwepo wa shoga yake, Bi. Mvita. Punde tu anapofika Selea, Bi. Mvita anaanza ukaguzi wa kila eneo ambalo harusi ingefanyika. Pindi anapomaliza na kuridhika amefanya ya kutosha, ujumbe kutoka kwake unafikishwa kwa Bahati kwamba angefikishwa unyago. Inasimuliwa,

> "*Jioni unyago ulianza. Wapigaji walikuwa uani na wachezaji waliojifunga vibwebwe, wanawake, vijana waliwazunguka wapigaji ... mirindimo ya msondo ikavuma hata kuta za kijumba kile zikavuma na kuwa sehemu ya ngoma."* (Kur. 82-83)

Kisha Bahati alibebwa mgongoni mwa Bi. Mvita na kupelekwa nje ya nyumba yao halafu Idi akafika na kulakiwa kwa shangwe. Baadaye, akaja Shehe Baraka akawafunganisha ndoa kwa itikadi za dini.

Matukio ambayo yaliendelea hapa katika nyumba ya kina Bahati, chini ya uelekezi wa Bi. Mvita ni dhihirisho kwamba alikuwa mtamaduni. Alifuatilia mila na desturi ya Waswahili ya kufanya unyago kabla ya ndoa ya Bahati. Mandhari ya kwa kina Bahati siku ya arusi, inayoyofafanuliwa inatumika vizuri kutufahamisha weledi wa Bi. Mvita kuhusu masuala ya utamaduni.

Kwa ujumla, imethibitika kwamba mandhari yana michango kabambe katika kukuza sifa za wahusika mbalimbali. Kupitia jinsi mandhari yalivyosawiriwa na watunzi hawa, kuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya sifa za wahusika wanaowasilishwa kwenye mazingira yanayohusika.



Mount Kenya University

Mandhari yaliyosukwa kitajiri yanafichua wahusika matajiri, yaliyosheheni umaskini yanafichua wahusika maskini, yaliyo na taswira ya kilevi, kisherati, utamaduni na kadhalika vivyo hivyo yanachimuza wahusika wenye mienendo na hulka kama hizo.

### 4.3 Mandhari Yanavyochangia Ukuzaji wa Ploti.

Ploti ni matukio yajengayo masimulizi (Wamitila, 2003). Kwa hivyo, ploti ni kule kufuatana kwa visa kimantiki katika kazi ya fasihi. Wamitila (2002) anasema kuwa msuko huu ni mfuatano wa matukio jinsi yanavyojiri kwenye tungo za kifasihi kwa mujibu wa kisababishi na uhusiano wao. Sehemu zifuatazo zinachanganua na kujadili nafasi ya mandhari katika ukuzaji wa msuko wa matukio katika riwaya teule – *Kidagaa Kimemwozea* pamoja na *Kiu*.

#### 4.3.1 Mandhari Yanavyochangia Ukuzaji wa Ploti ya *Kidagaa Kimemwozea.*

Ploti au msuko wa matukio ni mfuatano wa matukio jinsi yanavyojiri kwenye tungo za kifasihi kwa mujibu wa kisababishi na uhusiano wao (Wamitila, 2002). Msuko wa matukio yanayosimuliwa katika riwaya hii umekuzwa na kuchangiwa kwa viwango mbalimbali na mandhari kama vile: Mto Kibarenge, Sokomoko, kibanda cha Amani, kwa kina Fao, uwanja wa Nasaba Bora, miongoni mwa mengine. Matokeo ya uchunguzi na uchambuzi wa michango ya mandhari hayo yanawasilishwa na kujadiliwa kwenye vijisehemu vifuatavyo:

##### 4.3.1.1 Mto Kiberenge.

Mandhari aghalabu hutoa maelezo yanayoweza kuangazia matukio zaidi katika masimulizi na yakawa kielekezi cha hadithi yenyewe (Wamitila, 2002). Amani na Imani baada ya kutembea kwa siku kadhaa walikabwa na kiu. Walipofika kando ya Mto Kiberenge, Imani aliona kwamba walipata suluhisho la kiu walichokuwa nacho. Hawakujua kwamba mto huo ulikuwa na mwiko

kuhusu unywaji wa maji yake. Imani alipochota maji yale na kupiga funda moja baada ya jingine. Wale vijana waliokuwa wakiogelea walitoka majini kwa haraka ili kushuhudia na mmoja, kwa jina DJ, kumwonya kwamba,

*"Mazee usinywe maji hayo jo ... ni haramu*." (Uk. 6.)

Masimulizi ambayo yanafafanua kuhusu chanzo cha maji hayo kutonywewa na hata nyimbo kubuniwa kwa lengo la kuonya watu yamepenyezwa na mtunzi ili kusaidia kuendeleza ploti ya hadithi hii. Masimulizi hayo yanaendeleza ploti kwa kufanya msomaji kujua kiini cha maji ya mto Kiberenge kutonywewa pamoja na umbali mwiko huo ulienea. Kwa mujibu wa msimulizi wimbo ulibuniwa kuonya watu na kufanya mwiko huo kusambaa mpaka ikafikia ng'ambo zote mbili zilizopakana na Mto Kiberenge.

Masimulizi mengine yanatolewa kuhusu mwanamume mmoja mgonjwa wa kifafa aliyeenda kwenye mandhari ya Mto Kiberenge kuoga na baada ya kuvua nguo zake zote ghafla akaanza kufafaruka akateleza na kutumbukia majini na kuzama. Maiti yake, msimulizi anasema kwamba, ilisakwa bila mafanikio hii ikafasiriwa kama ishara kwamba miungu haikutaka maji ya mto huo kunywewa na binadamu. Masimulizi ya mandhari haya bado tu yalitumiwa na mwandishi kwa lengo la kuendeleza ploti yake ya hadithi ili msomaji wake aendelee kupata ufahamu zaidi wa chanzo cha mwiko uliozingira mto Kiberenge.

Isitoshe, mtunzi wa kazi hii ametoa masimulizi mengine kuhusiana na mandhari ya mto huu. Masimulizi yanahusu mandhari ya kihistoria, yaani enzi za harakati za ukombozi kutoka kwa ukoloni ambapo maiti ya Waafrika waliouawa na Wazungu walitupwa kwenye mto huu. Damu zao iligeuza maji haya mekundu lakini hata baada ya maji yale kutengenea baadaye. Taswira ya rangi nyekundu pamoja na maiti za watu ilisalia kwenye kumbukizi zao na hivyo kuchangia katika

kuhalalisha mwiko huu wa kutokunywa maji ya Mto Kiberenge. Maji hayo yakasalia ya kuogelea na kunywesha mifugo tu. Vilevile, masimulizi ya mandhari haya yamepenyezwa hapa kwa lengo la kuendeleza ploti ya hadithi hii, kuhusu baadhi ya vyanzo vya mwiko wa Mto Kiberenge.

Masimulizi ya DJ kwa Amani na Imani ukingoni mwa Mto Kiberenge kuhusu maisha yake; kwamba alikuwa mtoto wa mjane na mamake alikuwa akiuza pombe haramu mtaani Madongoporomoka mjini Songoa na kwamba alikawia sana bila kuwaona mamake na ndugu zake wengine watatu baada ya kusingiziwa kuiba na kufungwa jela ya watoto na kisha akawa mtoro wa jela ni masimulizi ambayo mtunzi ametumia kuendeleza ploti ya hadithi hii ili ipige hatua na kufanya msomaji aelewe asili ya huyu kijana machachari kwa jina DJ na madhila yaliyomfika hapo awali.

#### 4.3.1.2 Sokomoko.

Mtunzi ametueleza jinsi mandhari ya eneo hili yalivyokuwa hapo awali. Anasema kuwa ni eneo ambalo lilikuwa wakiishi wazungu peke na ardhi walizonyakua walitumia kupandia mimea kama michia, mikonge na kadhalika, pamoja na kufuga wanyama kama vile farasi, nyumbu, tausi, ng'ombe, punda na wengineo (uk. 18). Baadhi ya Wazungu walioishi hapa pia walitajwa kwa majina kama vile Ford, Bartholomew, Magdeline na Major Noon. Hata hivyo, masimulizi ya ziada yanatolewa kuhusu Major Noon ambaye wenyeji walikuwa wanamwita Majununi kutokana na kuboronga jina lake. Masimulizi mapevu yanatolewa kumhusu Mzungu huyu kama yafutavyo:

> *Majununi alikuwa mlowezi kutoka Uingereza, alipotua Sokomkoko alinyakua ardhi kubwa ya kujengea makazi yake*,msimulizi anaeleza kwamba *alikuwa kesha subuhiana na msichana mmoja Mfaransa kwa jina Mitchelle. Makazi yake ya kwanza yalikuwa ni hema ambayo alimwarifu mpenziwe aje aone kutoka Ufaransa, hata hivyo alipowasili aliudhika na makazi hayo," Monsieur Mjor Noon,"alisema Mitchelle. "Nasikitika sana sitakanyaga chini wayo wa mguu wangu. Jenga nyumba wacha ujuba.*" (Uk. 17)



Mount Kenya University

Majununi aliendelea na kujenga nyumba yenye vyumba vinne kisha akamwarifu Mitchelle aje aone. Punde alipowasili alikataa kutoka kwenye ndege na kusema,

*"Monsieur Major Noon,wacha ujuba wewe ile si nyumba.*" (Uk. 17).

Hatimaye, Majununi alijenga kasri ambalo kwa sasa lilikuwa linamilikiwa na Mtemi Nasaba Bora. Alipomwandikia Mitchelle barua tena wakati huu alishuka chini kuona jumba lile lakini hakupendezwa na idadi ya vyumba na rangi nyekundu kwenye sakafu. Kwa hivyo, alirudi kwao Ufaransa na kumjulisha Majununi kwamba aoe mwanamke kufu yake. Majununi akaishia kuchukia wanawake wote maishani na hakuwahi oa milele,akageukia kilimo na ufugaji wa wanyama. Kisa hiki kirefu kuhusu Majununi miongoni mwa Wazungu wengi waliokuja Sokomoko ni ishara kwamba mtunzi amekitumia kuendeleza ploti ya hadithi yake la sivyo angetaja Majununi jinsi alivyofanyia wale wazungu wengine. Kwa kumkuza huyu mhusika kwa kina hivi pia imetuwezesha kujua mengi kuhusu masaibu yaliyompata na jinsi alivyoishi baada ya usumbufu huu wote aliopitia mikononi mwa Mitchelle.

### 4.3.1.3 Kibanda cha Amani.

Msimulizi anaeleza kwamba Amani alipata ajira ya kushughulikia ng'ombe katika boma lake Mtemi Nasaba Bora. Siku moja alipokuwa kibandani kwake alianza kufikiria kuhusu nasaba yake. Katika safari hii ya kumbukizi tunajulishwa kama wasomaji kuhusu aila ya Amani, kwamba babu yake Amani aliitwa Chichiri Hamadi na kwamba aliuliwa na mtu mwenye uwezo mkubwa kwa sababu ya shamba lake alilokuwa nalo huku Sokomoko. Vilevile, kupitia kumbukizi hii tunaarifiwa kwamba aliyepanga mauaji yale (Mtemi Nasaba Bora) aliyapanga na baadaye kusingizia amu yake, Yusufu, kuwa ndiye alikuwa muuaji na kufungwa jela maisha.

Kupitia kumbukizi hii inabainikia msomaji kwamba Amani ndiye aliyekuwa mtoto wa pekee wa mamake ambaye alikuwa mjane walipokuwa wanaishi kule Ulitima. Maisha yao hayakuwa ya kimaskini sana wala ya kitajiri. Hii ina maana walikuwa wanaishi maisha ya kadri. Msimulizi kupitia kumbukizi hii anaeleza kwamba hatimaye mamake Amani aliaga dunia kupitia ajali ya barabarani. Matukio haya yote yanapenyezwa na mtunzi kupitia kwa Amani kwenye kumbukizi yake pale kwenye mandhari ya kibanda chake kwa lengo la kuendeleza ploti ya hadithi yake na kutusaidia kama wasomaji kujua mahali ambapo mgogoro kati ya Amani na Mtemi Nasaba Bora ulipoanzia na sababu zilizomfanya kuamua kuenda Sokomoko na zaidi kutaka ajira katika boma hili licha ya kwamba lilikuwa na historia ya wafanyikazi kuajiriwa na kufutwa kila uchao.

Baaada ya kulazimishiwa kitoto kile Uhuru na Mtemi Nasaba Bora, Amani aliamua kumtafuta Imani kwa kumtuma DJ ili aje amuauni majukumu ya ulezi. Imani alikubali mwito huo akaja kuishi na Amani pamoja na kitoto kile kwenye kibanda cha Amani. Siku zikapita kadhaa na kwa sababu Imani alikuwa na nia ya kumjua Amani zaidi aliamua kumfichulia siri zake akitumai kwamba Amani angefanya vivyo hivyo. Akaanza kusimulia jinsi walivyokutana pale ziwa Mawewa,

> *"Nilipokukuta pale ukingoni mwa Ziwa Mawewa nilikuwa nimeamua kujitosa majini na nifilie mbali kama nisingekupata hapo kando ya Ziwa Mawewa ningekuwa sasa marehemu. Najua ni vigumu kwako kusadiki maneno haya mtu kughairi nia ya kutaka kujiua ati kwa sababu ya kumkuta mwingine mahali alipotaka kufia ... kwa kweli kukuona pale ukingoni wasoma kwa sauti kuliniathiri sana. Sijui kwa nini?*" (Uk. 54)

Imani aliendelea kumweleza Amani historia yake,alimweleza kwamba babake ndiye aliyekuwa dereva wa lile gofu la tingatinga lililokuwa hapo kwake Mtemi Nasaba Bora. Tingatinga ambalo kwa sasa lilikuwa limebaki gofu na kumezwa na nyasi. Alimweleza kwamba alikuwa na ndugu ambaye alikuwa mwanasoka hodari kwa jina Chwechwe Makweche, Oscar Kambona, nduguye mmoja aliyeaga dunia kwa sababu ya mapuuza ya madaktari na mama yake. Alimweleza jinsi

babake alivyokufa katika harakati za kupambana na mkoloni ili nchi yao ipate uhuru. Alieleza jinsi ambavyo askari walifika kwao na kuwapiga yeye mamake na nduguye Oscar Kambona. Mamake akaaga dunia kutokana na kichapo cha wale askari. Nduguye Oscar Kambona akaondoka bila kumwaga akabaki peke yake. Wale askari wakarudi tena na nusura ateketezwe ndani ya nyumba yao. Hapa ndipo safari yake Imani ilianza ya kutaka kujitosa majini afilie mbali.

Kwa hivyo, katika safari ya kutaka kujiua alitembea na kufika ziwa Mawewa alipokutana na Amani kisadfa katika ukingo wa ziwa hilo. Masimulizi haya ya Imani kwake Amani yametumiwa na mtunzi kwa lengo la kuendeleza ploti ya hadithi hii. Hii ni kwa sababu mandhari ya Kibanda cha Amani kilimpa Imani fursa mwafaka ya kuwa pamoja na Amani na kukumbuka masaibu yaliyomkumba kwao Baraka. Zaidi ya hayo, masaibu ambayo kile kitoto kilikuwa kinapitia mikononi mwao pale chumbani kama kukosa mlo, mavazi na mazingira mazuri ya kukua pamoja na jukumu zito alilotwikwa Amani la ulezi huenda lilimfanya kufikiria kutaka kumjua zaidi.

Baada ya kukutana na kuwa marafiki, Amani na Madhubuti wanaonana mara kwa mara. Madhubuti alikuwa akimpa vitabu vyake asome. Madhubuti alikisia kwamba huenda Amani alikuwa msomi. Siku moja baada ya Madhubuti kusaili Amani kwa kitambo kuhusu kiwango chake cha elimu Amani anamjibu hivi,

> *"Kusema kweli niliwahi kuwa chuo kikuu mjini Songoa. Wapo walionionea gere kwa ufanifu wangu masomoni wakaniponza, kila mtihani nilioufanya tangu shule ya msingi hadi chuo kikuu niliongoza taifa zima. Basi ingawa sikupenda siasa, wanafunzi hao walificha karatasi za uchochezi chumbani mwangu na kuniitia askari. Nilifungwa jela miaka mitano ... kufungwa kulinikosesha maziko ya mamangu mzazi ...*" (Uk. 117)

Amani anasimulia kwamba alitaka kukutana na mjombake ambaye alimweleza kaifa ya kupokwa mali yao na ya nasaba yao. Masimulizi haya yote yametumiwa na mtunzi wa riwaya hii kwa lengo la kuendeleza ploti ya hadithi hii na ndiyo maana imetupa mwanya wa kujua yaliyokuwa moyoni

mwa Amani. Mandhari yanayosawiriwa hapa yanaedeleza ploti. Uwepo wa Madhubuti hapa unamfanya Amani kufunguka roho na kumweleza mambo yasiyojulikana kumhusu. Hata Imani hakuyajua licha ya kwamba walisafiri naye kwa muda kutoka Ziwa Mawewa mpaka Mto Kiberenge na hatimaye Sokomoko.

#### 4.3.1.4 Kwa Kina Fao.

Matukio muhimu yajengayo masimulizi ndiyo huijenga ploti ya kazi ya fasihi (Wamitila, 2003). Matukio haya hutendeka kwenye mandhari fulani ambayo huyapa uhai na uhalisi. Baada ya Amani kukilaza kikalala kitandani kile kitoto alichokiokota mlangoni pake, kumbukizi zake zilimwelekeza kwa kina Fao. Fao na Amani walikuwa wakisomea shule moja kule Ulitima. Wazazi wa Fao walikuwa tajiri. Babake Fao alikuwa meneja wa Benki mjini Ulitima na mamake alikuwa mwalimu wa Historia katika shule ya upili. Walikuwa na mali ndani na nje ya Ulitima. Amani anakumbuka kwamba alipotoka gerezani alimtembelea Fao kwao na kumkosa kwa sababu alikuwa ameenda Ulaya kusoma. Alimpata dadake Fao, ambaye kwa wakati huo alikuwa keshajifungua pasi na kuolewa. Vilevile, kulikuwa na kitoto kingine cha miaka mitano au sita hivi ambacho dadake alimwarifu kilikuwa chake Fao. Mtoto huyu alizaliwa baada ya Fao kumringa mwanafunzi aliyekuwa akimfunza kisha wazazi wa msichana huyo kwa ghadhabu wakakileta kikiwa na mwezi mmoja baada ya kuzaliwa. Masimulizi haya yametumiwa na mtunzi kuendeleza ploti ya hadithi yake na kumfanya msomaji kupata welewa kuhusu mhusika Fao, aila yake na matendo yake ya awali.

#### 4.3.1.5 Zahanati ya Nasaba Bora.

Riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* inasimulia mengi kuhusu mandhari ya Zahanati ya Nasaba Bora. Kuanzia jinsi ilivyopewa jina, utepetevu wa Wauguzi wake na hali ya Amani na DJ walipolazwa

humo pamoja na kutoroka kwa DJ zahanatini humo bila yeyote kujua. Hata hivyo, yapo maelezo ambayo mtunzi anayachimuza kuihusu zahanati hii. Inasimuliwa,

> *"Zahanati ya Nasaba Bora ilijengwa kwa auni ya fedha kutoka kwa serikali ya Uingereza. Fedha hizo zilipoletwa serikali ya Uingereza ilitumahi kuwa zingetumiwa kujenga hospitali kuu. Zilipoingia mkononi mwa Waafrika, zilipata matumizi mengine muhimu. Akali ndogo sana ilitumika kujenga zahanati ndogo ... akali kubwa ikaingia mifukoni mwa wasimamizi hao."* (Uk. 144)

Maelezo haya ya kina kuhusu mandhari na ujenzi wa Zahanati ya Nasaba Bora yametumiwa na mtunzi kuendeleza ploti ya hadithi yake na kutufahamisha kuhusu mahali pesa za ujenzi zilipotoka na jinsi zilivyoporwa na wasimamizi, akiwemo Mtemi Nasaba bora. Kwa hali hiyo, inabainika ni kwa nini Wanasokomoko walipata zahanati badala ya hospitali kuu.

#### 4.3.1.6 Uwanja wa Nasaba Bora.

Punde baada ya Mtemi Nasaba Bora kupotea na kupatikana msituni akiwa amejitia kitanzi, uongozi wake unafikia tamati. Kwa hivyo, inabidi nafasi yake ichukuliwe na kiongozi mwingine. Mtunzi anatumia mandhari haya ya msituni kuendeleza ploti ya hadithi yake. Anasimulia kuwa serikali kuu ilileta kaimu wa Mtemi kushikilia wadhifa huo. Kaimu Mtemi aliitisha mkutano wa hadhara katika uwanja wa Nasaba Bora. Wakaazi wa Sokomoko wakaja kwa wingi kumlaki. Inasimuliwa kwamba,

> "*Hawakujua kama ilihalisi au haikuhalisi kumpinga kaimu wa Mtemi, mtu ambaye hawakujua kaibukia wapi. Amani, Imani na Madhubuti pia walihudhuria hafla hiyo.*" (Uk. 157)

Masimulizi haya yanachangia kudhihirishia msomaji kwamba, japo Mtemi Nasaba Bora aliaga dunia, utawala uliendelea. Taarifa yenyewe inafahamika kupitia kuendelezwa kwa ploti ya hadithi hii na usimulizi wake pamoja na kufika kwa kaimu Mtemi katika Uwanja wa Nasaba Bora.

#### 4.3.1.7 Mandhari Kiwakati.

Akidhihirisha mandhari kwa kurejelea kipindi cha Enzi ya Ukoloni, msimulizi anaeleza kwamba,

> "*Wakati wa harakati za ukombozi dhidi ya ukoloni maiti za Waafrika waliouawa na Wazungu zilitupwa katika Mto Kiberenge*." (Uk. 4)

Ufafanuzi huu unaashiria kwamba upo wakati ambapo Wakoloni walikuwa katika nchi ya Tomoko. Ulipotimia muda fulani, vita vya ukombozi vilizuka ili Waafrika wajinasue kutoka katika minyororo ya ukoloni. Vita vyenyewe vilizuka baina ya Wakoloni na wapiganaji Waafrika ambao walijitolea mhanga kukomboa nchi yao. Baadhi yao waliuawa na miili yao kutupwa katika Mto Kiberenge. Ufafanuzi huu wa mandhari kihistoria umetumika kwa lengo la kuendeleza ploti na mtunzi. Japo ni tukio ambalo lilitendeka kitambo kwa mujibu wa hadithi inayosimuliwa, kuibuliwa kwalo kunamsaidia msomaji kujua chanzo cha mwiko unaozingira Mto Kiberenge.

### 4.3.2 Mandhari Yanavyochangia Ukuzaji wa Ploti ya *Kiu.*

Ploti imeelezwa kuwa ni mfuatano wa matukio katika tungo za fasihi (Wamitila, 2002). Kwa mantiki hiyo, uchunguzi na uchanganuzi wa mandhari mbalimbali yanayosawiriwa katika riwaya ya *Kiu* umefanikisha ubainishaji wa mchango wake katika ukuzaji wa ploti. Sawia na *Kidagaa Kimemwozea*, mandhari mbalimbali yametumika kuendeleza ploti katika riwaya hii. Mandhari muhimu yanayotumika kufanikisha mjadala ni pamoja na: chumba cha Mzee Mwinyi, chumba cha kina Bahati, Vibyongoni, hospitali, pamoja na bahari.

#### 4.3.2.1 Chumba cha Mzee Mwinyi.

Mtunzi aghalabu hueleza mandhari kwa njia inayochangia ujenzi wa ploti ya kazi yake. Sifa hii huchukuwa nafasi muhimu katika riwaya ya kiuhalisia (Wamitila, 2002). Idi anapoenda

kumtembelea Mzee Mwinyi kwake Ukele, anakaribishwa na Mwajuma, mfanyikazi wa nyumbani. Mandhari ya chumba hiki yalidhihirisha utajiri mkubwa ajabu.

Ukutani pembe mbili za faru, pambo zuri la thamani, ngozi ya chui pamoja na kichwa chake, bunduki mbili za kiasili zenye vitako vya mpingo na msumari ya dhahabu. Upande mwingine wa ukuta ulitundikwa upinde na mshale na picha mbili kubwa. Picha ya kwanza, ilikuwa ya mwanamke mwenye sura nzuri aliyeketi juu ya jiwe kando ya kijito akiwa uchi huku akichana nywele na kutabasamu. Picha ya pili ilikuwa ya Mzee Mwinyi mwenyewe, sura yake alipokuwa na miaka thelathini.

Msimulizi anasema kwamba punde Mwinyi alipoingia ukumbini hata kabla ya kuamkiana na Idi anasema,

> *"Picha hiyo* [ya msichana aliyekuwa uchi] *nilipewa na rafiki yangu wa kifaransa nilipokwenda Paris kabla ya Vita vya Kwanza vya Dunia*." (Uk. 9)

Baada ya maelezo haya wanaingilia masuala ya Bahati. Jambo hili ni ithibati kwamba ufafanuzi huu wa mandhari unatumiwa na mtunzi kuendeleza ploti ya hadithi yake kwa madhumuni ya kutufahamisha kwamba Mzee Mwinyi alikuwa na utajiri mkubwa pamoja na chimbuko la picha ile ya msichana aliyekuwa uchi.

#### 4.3.2.2 Chumbani kwa Kina Bahati.

Tunaelezwa na msimulizi kwamba Bahati alilemewa na hisia za huzuni baada ya mgogoro kuzuka kati yake na mpenziwe, Idi. Chanzo cha mgogoro huu ni pendekezo la Idi kwamba Bahati amdanganye Mzee Mwinyi kwa mapenzi ya uongo ili wamlaghai mali yake. Pendekezo ambalo Bahati analikataa na hivyo kusababisha mtafaruku baina yake na Idi. Kikafikia kiwango cha Idi kumrejesha kwao wakiwa hawaongei mle garini. Tukio hili lilimhuzunisha Bahati sana akawa

amejifungia mle chumbani mwake akilia. Mamake alimsaili lakini alikataa kumweleza yaliyojiri. Japo alishuku kuna jambo. Masimulizi haya kuhusu jinsi Bahati alivyolemewa na huzuni na kulia usiku kucha baada ya kuachana na Idi yametumika kuendeleza ploti ya hadithi hii ya mtunzi ili kutuwezesha kung'amua jinsi ambavyo Bahati alikuwa na mapenzi ya dhati kwake Idi.

Vilevile, msimulizi ameeleza kwa mapana jinsi chumba cha kina Bahati kilivyokuwa, msala ambao sakafuni ulikuwa umechakaa, kiti cha henzirani asilia ambacho marehemu nyanyake Bahati aliwahi kukikalia na kumpakatia mamake Bahati na kumnyonyesha (uk. 28). Masimulizi kuhusu babake Bahati, Jaku, ambaye inasemekana alielekea upande wa Kongo miaka sita iliyopita na kumwachia Cheusi malezi ya Bahati peke yake. Haya yote yanadhihirika kwenye mandhari ya chumba cha kina Bahati baada ya yeye kuona kwamba amepoteza bahati ya kumtoa mamake kwenye umaskini uliowazonga kwa kukataa kushirikiana na Idi. Lengo la mtunzi hapa bado likiwa kuendeleza ploti ya hadithi yake kwa kutujuza sisi wasomaji mengi kuhusu babake Bahati, familia ya mamake na umaskini wao.

Hatimaye, Bahati na Idi wanaoana na harusi yao inapangwa nyumbani kwa kina Bahati Mtaa wa Selea. Msimulizi anasema kwamba Cheusi, mamake Bahati, aliwaalika mashoga zake wengi kama vile Hadija na Biti Jaku wamsaidie katika maandalizi. Hata hivyo, kati ya mashoga hawa kuna mmoja, Bi. Mvita, anayetumiwa na mtunzi kuikuza zaidi ploti ya hadithi inayosimuliwa. Inasimuliwa kwamba harusi hiyo haingepangwa bila Bi. Mvita kuwepo. Inasemekana,

> "*... alipenda kuendesha arusi kwa mila za kizamani za Kiswahili ambazo zilihitaji mambo mengi ya kufanya. Chini ya uongozi wake, Bahati hakuwa na hiari ila kufuata maagizo yake.*" (Uk. 82)

Mtunzi anampa mhusika huyu nafasi kubwa katika harusi hii ili kumsaidia kuendeleza ploti ya hadithi na kumwezesha kufafanua umuhimu wa utamaduni katika jamii hii.

Baada ya ndoa ya Bahati na Idi kuingia doa na wakaachana alirudi kwao Selea. Ikawa kwamba siku moja Mwajuma alimshauri kumwandikia Idi barua ya kutaka mgao wake wa mali. Akafanya hivyo na kumpa Mwajuma barua yenyewe kumpelekea. Wasiwasi ukamwingia mbona kafanya hivyo. Ili kujipumbaza aliende alipokuwa mamake kisha masimulizi kuhusu babake yakachimuza,

> *"Juzi akaja bwana mmoja hapa, anavyosema mwenyewe kuwa anatokea Kongo, kaniambia kuwa walikuwa njia moja na baba yako, lakini bahati mbaya baba yako kakamatwa na vipusa walipokuwa njiani ... na kufungwa miaka sita. Anavyosema yeye kuwa miaka sita tangu hapo alipokamatwa kiasi imeshatimia. Sijui kweli ama uongo, lakini ikiwa kweli basi baba yako yu hai na kifungo chake kimekwisha."* (uk. 156)

Masimulizi haya yametumiwa na mtunzi kuendeleza ploti ya hadithi hii kwa kutueleza kuhusu alipopotelea Jaku kule Kongo. Kwamba kupotea kwake kulikuwa kwa sababu ya kushikwa na kufungwa kwa vile alijihisisha na uwindaji haramu kule Kongo. Mandhari haya ya nyumbani kwa Cheusi yanawaweka pamoja Bahati na mamake ili aweze kuelezwa kuhusu ripoti zilizochipuka kuhusu babake mzazi na tuhuma za kukamatwa kwake; masuala ambayo Bahati hakuwa na habari nayo.

#### 4.3.2.3 Vibyongoni.

Imebainika kwamba Selea kwa kina Bahati ilikuwa kwenye mabonde. Kwa hivyo, ilibidi yeyote aendaye Vibyongoni kupitia milima. Vibyongoni ulikuwa mtaa mzuri wenye nyumba za chini zilizopangwa (uk. 31). Njia za kuelekea huko zilikuwa safi, nyumba zake zimeezekwa bati, zimepangika na kusakafiwa vyema. Msimulizi anaongeza kwamba mtaa huu ulipewa jina hili wakaazi wake walivyofanya vibyongo kwa kupanda mlima huo. Masimulizi haya ya ziada yamepenyezwa hapa kwa minajili ya kuendeleza ploti ya hadithi ili kumfanya msomaji aweze kung'amua jinsi ambavyo eneo hili lilipata jina lake. Ikumbukwe kwamba kuna mitaa mingi

ambayo imetajwa hapa lakini asili ya majina hayo haijatolewa jinsi ilivyofanywa katika mtaa wa Vibyongoni.

### 4.3.2.4 Hospitalini.

Bahati alilazwa hospitalini baada ya mguu wake kuumia alipokuwa akimsaidia Idi kupanda viduta vya nyumba yao. Tukio hili lilifanyika baada ya Idi kurudi nyumbani siku moja akiwa amelewa. Bahati alipomwahi ili kumsaidia kupanda viduta alimlemea kwa uzani wake wakaanguka chini. Ni katika harakati hizi ndipo aliumiza mguu wake. Akiwa hospitalini, msimulizi anaeleza kwamba alianza kuomba,

> *"Ewe Mungu wangu, mwenye kuumba na kuumbua, mwenye kutaka likawa, mwenye kuombwa ukatoa, Mfalme wa viumbe vyote - mhidi mume wangu, mtie huruma na mapenzi, mfunue macho, utusamahe makosa yetu! ...*" (Uk. 119)

Maombi haya yafanyikayo kwenye mandhari ya hospitalini yametumiwa na mtunzi kwa minajili ya kuendeliza ploti ya hadithi hii. Bahati anamwombea mumewe kwa sababu ya kutekwa na ulevi na anasa. Mandhari haya ya hospitali yamechangia pakubwa pia katika kutuwezesha kufahamu kwamba matatizo ya kindoa yanapokuwa mengi basi wahusika hugeukia Mwenyezi Mungu kwa msaada.

### 4.3.2.5 Bahari.

Katika eneo hili twapata Bahati na Mwajuma wakibarizi huku akimweleza jinsi alivyomjua Mwajuma alipokuwa akija kwa Mzee Mwinyi. Anamweleza jinsi safari yake ya mapenzi na Idi ilivyokuwa na hata jinsi walivyomlaghai Mzee Mwinyi mali yake kupitia kwa njama za Idi na hatimaye kuoana na kuhamia Buraha. Bahati anamweleza kuwa,

> *"Basi ndugu yangu nikueleze nini! Ilikuwa raha ya siku mbili au tatu. Alianza kuchomoka na ulevi, si ulevi huo, mimi nikatupiliwa mbali, nikatafuta roho*

*yangu pa kuiweka. Tangu akishinda nje. Hata akilala nje, hata sasa hukaa nje wiki nzima sijamshuhudia. Na kila siku yanazidi. Na wewe unayaona. Miaka mitano yote nimeishi katika hali kama hii - mpaka leo.*" (Uk. 141)

Haya masimulizi yametumika kwa nia ya kuendeleza ploti ya hadithi hii ambapo msomaji anapata kujua motifu ya safari ya maisha na changamoto za maisha ya Bahati katika ndoa yake na Idi.

Hivyo basi, inahalisi kusema kwamba mandhari, kwa mujibu wa data zilizochanganuliwa katika vijisehemu hivi, yana michango mikubwa katika uendelezaji wa ploti za hadithi kwenye riwaya hizi mbili. Hii ni kwa sababu kupitia kwayo imethibitika kwamba mandhari yanachangia katika kuelezea motifu ya safari ya wahusika, vyanzo vya masaibu ya wahusika, kujuza kuhusu masuala ambayo wasomaji na wahusika wengine hawayafahamu kumhusu mhusika fulani, jinsi wahusika wanavyopambana na masaibu yao na hata kujua hisia zao wakiwa katika mandhari fulani. Akiishadidia hali hii, Wamitila (2002) anasema kwamba mandhari yanaweza kutumiwa na mtunzi kutoa maelezo fulani kuhusu matokeo kwa azma ya kuyapa masimulizi yake mwelekeo fulani. Haya maelezo yanaweza kuangazia matukio zaidi katika masimulizi hayo na yakawa kielekezo cha hadithi yenyewe.

## 4.4 Hitimisho.

Sura hii imejishughulisha na aina kuu mbili za mandhari - mandhari ya wakati na mandhari ya mahali. Imefafanua jinsi mandhari yanavyochangia ukuzaji wa maudhui mbalimbali, sifa za wahusika na uendelezaji wa ploti katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* (Walibora, 2012) na *Kiu* (Mohamed, 1972). Uchanganuzi wa data iliyokusanywa umechangia kuyajibu maswali ya utafiti. Matokeo ya uchunguzi yanathibitisha kwamba mandhari huchangia uwasilishaji wa ujumbe, ujenzi wa sifa za wahusika pamoja na ukuzaji wa ploti kwenye tungo za kiriwaya. Sura ya tano inayofuata inawasilisha muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

## SURA YA TANO

## MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

### 5.0 Utangulizi.

Hii sura inajishulisha na muhtasari wa matokeo, hitimisho na mapendekezo ya utafiti huu. sehemu ya kwanza inaieleza tasnifu nzima kwa kifupi kabla ya kuwasilisha matokeo ya utafiti kwa muhtasari. Sehemu ya tatu inawasilisha hitimisho la utafiti ilhali sehemu ya mwisho inajadili mapendekezo ya utafiti uliokamilika pamoja na mapendekezo kuhusu tafati za baadaye.

### 5.1 Muhtasari wa Tasnifu.

Tasnifu hii imeundwa kwa sura tano. Kila sura inatekeleza jukumu lake teule kama inavyodhihirika katika sehemu hii. Sura ya kwanza inaangazia msingi wa utafiti ambapo masuala yafuatayo yameshughulikiwa: usuli wa utafiti, suala la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, misingi ya uteuzi wa mada, upeo na mipaka ya utafiti pamoja na umuhimu wa utafiti.

Kila sehemu kwenye sura hii kinajishughulisha na dhima mahsusi. Usuli wa utafiti unaangazia masuala muhimu yaliyotumiwa kuujengea utafiti huu msingi dhabiti kwa kuvifafanua vigeu vyake. Suala la utafiti linaibuliwa na hivyo kuufanikisha uchunguzi wenyewe; malengo ya utafiti yalikuwa matatu. Nayo ni: kubainisha aina za mandhari yanayotumiwa kuwasilisha ujumbe katika riwaya ya *Kiu* na *Kidagaa Kimemwozea*, kutathmini mchango wa mandhari katika kujenga sifa za wahusika kwenye riwaya hizi na kueleza mandhari yanavyochangia ujenzi wa sifa za wahsusika kwenye riwaya hizi mbili. Maswali ya utafiti yalitungwa na kuwa kielelezo muhimu yaliyoongoza huu utafiti, misingi ya uteuzi wa mada ya utafiti imeelezwa na upeo na mipaka ikaafikiwa kwamba

ni riwaya mbili tu zilizochunguzwa - *Kidagaaa Kimemwozea* na *Kiu*. Kisha, umuhimu wa kuufanya utafiti huu umefafanuliwa.

Katika sura ya pili, mwauo wa maandishi umefanikishwa. Masuala kadhaa yameshughulikiwa kama yalivyochunguzwa na wataalamu wengine awali, yakiwemo: uanishaji wa mandhari, dhima ya mandhari katika ujenzi wa wahusika, mchango wa mandhari katika ukuzaji wa ploti na misingi ya kinadharia. Nadharia zilizoongoza huu utafiti zikiwa ni mbili ile ya Uhalisia na ya Umuundo.

Sura ya tatu ikachangia mbinu zilizotumiwa katika kufanya utafiti huu. Katika sura yenyewe baadhi ya masuala yaliyoangaziwa ni pamoja na: muundo wa utafiti, eneo la utafiti, idadi lengwa, sampuli na usampulishaji, njia ya kukusanyia data, uchanganuzi wa data, uwasilishaji wa matokeo na maadili ya utafiti.

Sura ya nne inachanganua data na kuwasilisha matokeo ya utafiti. Kila lengo limeangaziwa kwa mujibu wa mandhari mbalimbali yaliyopatikana kwenye riwaya zilizochambuliwa. Hatimaye, sura ya tano inajishughulisha na muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti.

Azma kuu ya utafiti huu ilikuwa kuchunguza usawiri wa mandhari kwenye riwaya ya *Kiu* na *Kidagaa Kimemwozea* ili kubainisha uhusiano uliopo kati ya mandhari na sifa za wahusika, mandhari na uwasilishaji wa ujumbe na mwisho uhusiano uliopo kati ya mandhari na uendelezaji wa ploti. Azma hii imeafikiwa kwa mwongozo wa malengo mahsusi matatu ambayo yalikuwa ni kubainisha aina za mandhari yanayotumiwa kuwasilisha ujumbe katika riwaya ya *Kiu* na *Kidagaa Kimemwozea*; kutathmini mchango wa mandhari kujenga sifa za wahusika katika riwaya ya *Kiu* na *Kidagaa Kimemwozea* na kueleza mandhari yanavyochangia ukuzaji wa ploti kwenye riwaya hizi.

Mandhari mbalimbali yalichunguzwa kutoka kwenye riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* (2012) na *Kiu* (1972). Ken Walibora na Mohamed. S. Mohamed wamesawiri mandhari yao kwa namna tofauti tofauti na hivyo kuufanikisha utafiti huu. Katika *Kidagaa Kimemwozea* mandhari takriban kumi na nane yamechangia katika kuafiki lengo la kwanza la utafiti, huku kwenye *Kiu*, yakiwa ni mandhari kumi yaliyoafiki lengo la utafiti. Katika lengo la pili mandhari kumi na manne na kumi mtawalia yaliafiki lengo kisha katika lengo la tatu mandhari manane na manne yalichangia katika kuafiki lengo hili.

### 5.2.1 Mandhari Yatumiwavyo Kuwasilisha Maudhui ya Riwaya.

Huu utafiti ulibaini kwamba katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* na *Kiu* mandhari yafuatayo yalichangia katika kukuza maudhui. Mandhari ya Mto Kiberenge ambayo yalichangia kuchimuza maudhui ya utamaduni, wakaazi wengi hapa ni watamaduni hawanywi maji ya mto huu kwa sababu ya kikwazo cha utamaduni, Mandhari ya Sokomoko yalichimuza maudhui ya ufisadi na kazi; mhusika Mtemi Nasaba Bora akiwa mstari wa mbele katika kuendeleza ufisadi Sokomoko, mandhari ya nyumbani kwa Mwalimu Majisifu yalichimuza maudhui ya utepetevu kazini, utu, wizi wa kitaaluma pamoja na ulevi. Mandhari ya kibanda cha Amani yalidhihirisha maudhui ya mapuuza, ukatili, uongozi mbaya na mabadiliko. Mandhari ya shuleni ulitima yalichimuza maudhui ya ufisadi, mandhari ya kasri la mtemi Nasaba Bora yalichimuza maudhui ya unyanyasaji, ufisadi, kifo na uozo. Mandhari ya uwanja wa Nasaba Bora yalidhihirisha moja kwa moja maudhui ya utabaka na ukoloni nayo mandhari ya barabara yalichimuza maudhui ya kifo na utepetevu kazini, chumba cha kulala kwa Mtemi Nasaba Bora kilidhihirisha maudhui ya ukatili, mapenzi na uashereti. Mandhari ya seli au choo yalichimuza maudhui ya ukatili na dhuluma dhidi ya wafungwa.

Mandhari chuoni Mkokotoni yalidhihirisha maudhui ya wizi wa kitaaluma, mwandishi wa *Kidagaa Kimemwozea* vilevile aliswiri mandhari yake ya Zahanati ya Nasaba Bora kama eneo la kuendelezea maudhui ya ufisadi na utepetevu kazini, mandhari ya msitu yalidhihirisha maudhui ya kifo, mandhari ya kiwakati kama vile enzi za ukoloni na Vita Vikuu Vya Dunia vilitumika kudhihirisha maudhui ya ukoloni na siasa mtawalia.

Katika riwaya ya *Kiu* (1972) mwandishi alitumia mandhari mbalimbali kudhihirisha maudhui tofauti tofauti kama vile: Mandhari ya chumba cha Mwinyi yalidhihirisha maudhui ya utajiri, mandhari ya Benzi yalidhihirisha maudhui ya mapenzi nayo mandhari ya Makonde yalichimuza maudhui ya uchafuzi wa mazingira. Kuna mandhari mengine kama vile mandhari ya Selea kwa kina mhusika Bahati ambayo yalichimuza maudhui ya malezi, ndoa, utamaduni na umaskini. Mandhari ya Vibyongoni ambapo aliishi mhusika Idi, yalidhihirisha maudhui ya uozo na uasherati, mandhari ya Benki yalidhihirisha maudhui ya kazi. Ukele ni mandhari mengine ambayo yalichimuza maudhui ya ulevi. Maudhui ya wakati, miaka mitano ilidhihirisha maudhui ya ndoa, ulevi, anasa na uasherati.

### 5.2.2 Mandhari Yachangiavyo Ujenzi wa Sifa za Wahusika katika Riwaya.

Katika lengo la pili la utafiti huu jumla ya mandhari kumi na manne kwenye *Kidagaa Kimemwozea* (2012) na tisa kwenye *Kiu* (1972) yaliliafiki, Mandhari ya Mto Kiberenge yalifichua sifa za wahusika kadhaa kama watamaduni na jasiri,mandhari ya nyumbani kwa Mtemi Nasaba Bora kulidhihirisha sifa za wahusika kama vile wenye mapuuza,wenye huruma na wakali,maegeshoni kwa gari yanadhihirisha sifa ya mwenye dharau na mapuuza. Nyumbani kwa Mwalimu Majisifu sifa zifuatazo zilijitokeza:mwenye utu,mwenye wivu,mpyaro na mkali.Mandhari ya kibanda cha Amani yalichimuza sifa ya mwenye hasira, msiri na mkweli. Uwanja wa Nasaba Bora ulidhihirisha

sifa ya mhusika Mtemi Nasaba Bora kama dhalimu na katili. Zahanati ya Nasaba Bora ilidhihirisha sifa za wahusika wengine kama wafisadi, wabadhirifu wa mali,wenye dharau ,mapuuza na utepetevu kazini. Mandhari ya seli yalidhihirisha sifa ya wahusika kama katili na wenye hasira. Mandhari ya chumba cha Mtemi cha kulala ilichimuza sifa ya mtiifu na katili, Barabarani tunapata sifa za wahusika kama walipiza kisasi, mwoga, mshawishi na mpenda amani. Mandhari ya wakati ya enzi za kikoloni ilidhihirisha Waafrika kama wazalendo.

Katika *Kiu* mandhari kadhaa yalidhihirisha sifa za wahusika kama vile mandhari ya barabarani yalifichua sifa ya Mwinyi kama mvumilivu na mwenye mapenzi ilhali dereva wake kama laghai,mandhari ya Ukele ilichimuza sifa ya mhusiska Idi kama mlevi, mandhari ya Selea ilifichua sifa za Bahati kama vile mwenye mapenzi ya dhati naye Bi. Mvita kama mtamaduni. Vibyongoni tunapata sifa za Bahati na Idi kama washerati na walaghai. Mandhari ya chumbani kwa Kidawa ilidhihirisha sifa ya mumewe kama mwenye wivu na mkali. Buraha ilifichua sifa za Idi kama mlevi, mpenda anasa, mpyaro na mkali. Mandhari ya wakati kama vile miaka sita ilifichua kwamba Jaku, baba yake Bahati alikuwa mwenye mapuuza.

### 5.2.3 Mandhari Yachangiavyo Ukuzaji wa Ploti ya Riwaya.

Tukiangazia lengo la tatu, tunapata mandhari tofauti tofauti ambayo yalichangia katika kukuza ploti ya hadithi katika riwaya hizi mandhari haya kwenye *Kidagaa Kimemwozea* (2012) ni kama vile mandhari ya Mto Kiberenge, ya Sokomoko, Kibanda cha Amani, kwa kina Fao, Zahanati ya Nasaba Bora, Uwanja wa Nasaba Bora na Enzi za kikoloni kama mandhari ya wakati, ilhali kwenye *Kiu* (1972) tulipata mandhari kama vile chumba cha Mwinyi, Selea, Vibyongoni, hospitalini na bahari.

Mandhari mbalimbali yalichangia katika msuko kwa kutufanya kujua jinsi wahusika walikuwa wakitoka katika mandhari moja mpaka nyingine na shughuli zilizowafanya kusonga songa kutoka sehemu moja mpaka nyingine.Kwa kufanya hivi mfuatano wa vitushi katika hadithi riwayani ulitiririka na kujengana kuanzia mwanzo mpaka mwisho wa hadithi na kutufanya kuelewa motifu ya safari ya kila mhusika pamoja na jinsi ususi wa misuko ilivyotiririka hadithini.Tulibaini hisia zao,jinsi walivyopambana na masaibu yao na mengi tuliyoyajua kuwahusu kupitia ploti yalichangiwa na mandhari ambamo walikuwemo.

## 5.3 Hitimisho.

Huu utafiti ulichunguza usawiri wa mandhari na uhusiano uliopo baina yake na sifa za wahusika,jumbe (maudhui) na ploti za hadithi kwenye riwaya hizi mbili.Uchunguzi ambao ulidhihirisha wazi kwamba mandhari yana michango mikubwa katika vitengo hivi vitatu kama ilivyojitokeza kwenya uchanganuzi wa data, ilibainika kuwa aina mbalimbali za mandhari;ya kijiografia na kihistoria yalikuza sifa za wahusika,jumbe na ploti za hadithi kikamilifu.Hivyo basi ni vyema kusema kwamba mandhari katika utungo wowote wa kifasihi ni kiungo muhimu kwa mwandishi yeyote ambaye anapania kutunga kazi yenye mnato na ustadi wa uandishi.

## 5.4 Mapendekezo.

Huu utafiti uliongozwa na nadharia mbili mseto ya umuundo na uhalisia ambazo zilitumika kuchunguza usawiri wa mandhari na michango yao katika kukuza jumbe,ploti na sifa za wahusika kwenye riwaya zilizotajwa awali kwa hivyo mapendekezo yetu ni pamoja na yafuatayo:

### 5.4.1 Mapendekezo ya Utafiti.

Utafiti huu utumike na wahakiki na watunzi wa kazi za fasihi kuainisha aina mbalimbali za mandhari na jinsi yanavyochangia katika ukuzaji wa ploti,maudhui na sifa za wahusika.

Wakuza mitaala pia waweze kutumia matokeo ya utafiti huu kuweka mandhari kama kigezo muhimu cha utunzi katika baadhi ya vitabu vinavyochapishwa vya fasihi katika taasisi za elimu nchini.

### 5.4.2 Mapendekezo ya Tafiti za Baadaye.

Tafiti za baadaye zishughulikie masuala kama vile:

i) Mandhari yanavyokuza vipengele mbalimbali vya fani katika riwaya hizi au nyinginezo.

ii) Mandhari yanavyokuza ploti, wahusika na maudhui katika tanzu nyinginezo kama ushairi, tamthilia na hadithi fupi kwa kutumia nadharia tofauti.

Mount Kenya University

## MAREJELEO


Adam, E. (2014). *The comparative grammaticality of the English comparative*. (Not published): Straford University.

Amana, B. (2008). *Njiapanda*. Nairobi: Oxford University Press, East Africa Limited

Bakize, L. (2014). *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es Salaam: Moccony Printing Press.

Buliba na wenzie. (2014). Relative Effects of Cooperative Learning Approach on Secondary School Students' Attitude in Kiswahili Language Comprehension in Kisii Central Sub County. *International Journal of Humanities, Social Sciences and Education, 4(3)*, 2349-2381.

Burhan, Z. (1987). *Mwisho wa kosa.* Nairobi: Longman Publishers.

Curran, R. na Perecman, E. (2006). *A Handbook for Social Science Field Research*. London: Sage Publications.

Dawson, D. (2002). *Practical Research Methods: A User-Friendly Guide to Mastering Research Techniques and Projects*. Oxford: How to Books.

Elmeel, S. na Elmeel, D. (2007). *Educator's Companion to Children Literature: Folklore Contemporary Realistic Fiction, Fantasy, Biographies and Tales from here and there Volume 2*. London: Green wood Publishing Group.

Erickson, N. (2018). The Importance of Setting in Your Story. https://blog.bookbaby.com/2018/02/Importance-of-Setting-in-Your-Story/.27/4/2021


Mount Kenya University

Fang, Z. (1996). Illustrations, Text, and the Child Reader: What are Pictures in Children's Story books for? *Reading Horizons: A Journal of Literacy and Language Arts, 23(1)*, 2-3.

Ferdinand, S. (1959). *Course in General Linguisics*. New York: Philosophical Library.

Fides, C. (2017). *Kutathmini Matumizi ya Lugha na Dhamira katika Tamthilia za Kinjekitile na Nyerere na safari ya Kanaani: Utafiti Linganishi*. Tasnifu ya Umahiri. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Fisher, D. na Frey, N. (2014). Student and Teacher Perspectives on Close Reading Protocol. *Literacy Research and Instruction 53(1)*, 25-49.

Fisher, D. na Frey, N. (2015). Improve Reading with Complex Texts. *Phil Delta Kappan 96(5)*, 56-61.

Gatakaa, G. (2012). *Uhakiki wa maudhui katika Utenzi wa Mikidadi na Mayasa*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Gromov, M. (2022). Depiction of the Younger Generation in Kenyan Swahili Women's Prose in the Twenty First Century. *The Nairobi Journal of Literature, 10 (Special Issue)*, 81-98.

Habwe, J. (2008). *Cheche za Moto*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Heidegger, M.S. (1982). *The Basic Problems of Phenomenology*. Trans. Albert Hofstadter. Bloomington: Indiana University Press.

Hinchman, K. na Moore, D. (2013). Close reading: A Cautionary Interpratation. *Journal of Adolescent and Adult Literacy, 56(6)*, 441-450.

Mount Kenya University

Hunt, P. (2006). Introduction: The Expanding World of Children's Studies. Katika, *Understanding Children's Literature*. New York: Routledge. Kur. 11-24.

Iser, W. (1977). *The Act of Reading: A Theory of Aesthetic Response.* Michigan: John Hopkins University Press.

Izadi, G. (2017). Heroic Legends and Epic. *Journal of History Culture and Art Research 6(1),* 602-616.

Jesse, M. (2017). *Itikadi katika Riwaya za Said Ahmed Mohamed*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Joyce, M. (2011). *Uhakiki wa Fani katika Utendi wa Mwananinga: Nadharia ya Umuundo*. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Kombo, D. na Tromp, D. (2006). *Proposal and Thesis Writing.* Nairobi: Pauliness Publications.

Kothari, C. (2008). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International Publishers.

Lucaks, G. (1963). *The meaning of contemporary realism*. London: Merlin Press.

Magare, F. (2002). *Uhakiki wa Tamthilia ya Amezidi kama kazi ya kibwege*. Tasnifu ya Umahiri (haijachapishwa). Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Massoud, S. (2013). *Maudhui na Fani katika Tamthilia za Kiswahili: Utafiti Linganishi wa Tamthilia ya Mashetani na Kivuli Kinaishi.* Tasnifu ya Uzamivu katika Kiswahili. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Matei, A. (2012). *Fani ya Fasihi Simulizi kwa Shule za Upili*. Nairobi: Oxford University Press.

Matei, A. (2017). *Chozi la Heri*. Nairobi: One Planet Publishing & Media Services.

Mbatia, M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and Publishing.

Mbithi, C. (2021). *Usawiri wa mandhari katika Embe Tamu, Siku ya Wajinga na Njia Panda*. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa). Nairobi: Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Mligo, E. (2012). *Jifunze Utafiti: Mwongozo Kuhusu Utafiti na Uandishi wa Ripoti yenye Mantiki*. Dar es Salaam: Ecumenical Gathering.

Mohamed, S. (1972). *Kiu*. Nairobi: Longman Publishers.

Mohamed, S. (1980). *Utengano*. Nairobi: Longman Publishers.

Momanyi, C. (2005). *Siku ya Wajinga*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Momanyi, C. (2021). *Nguu za Jadi*. Nairobi: Queenex Publishers.

Mpalanzi, L. (2020). Makutano kati ya Dini ya kijadi na kigeni: Mifano kutoka Riwaya Teule za Kiswahili. *Kioo cha Lugha, 17(1)*, 114-131.

Msacky, E. (2015). *Kuchunguza Dhamira za Kijamii na Kisiasa katika Riwaya ya Siri za Maisha*. Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa). Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Msokile, M. (1993). *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Mugenda, O. na Mugenda, A. (1999). *Research Methods: Quantitative and Qualitative Approaches*. Nairobi: Acts Press.

Mount Kenya University

Munyao, R. (2017). *Mwingiliano wa Fasihi na Historia katika Utenzi wa Nchuu Cwavo Yapo Tini Mwa Irara (Mtu ni kwa japo Chini mwa Irara).* Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Murray, P. (1978). *Literary Criticism: A Glossary of Major Terms*. New York: Longman.

Mwangi, D. (2005). *Uhakiki wa Fani katika Tamthilia za K.W. Wamitila*. Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Njogu, K. (2003). *Embe Tamu*. Nairobi: Oxford University Press.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Ntarangwi, M. (2004). *Uhakiki wa Kazi za Fasihi*. Illinois: Augustana College, Rock Island.

Ntiba, G. (2011). *Nyimbo kama Mkakati wa Kuimarisha Mshikamano Barani Afrika*: *Uchanganuzi wa Nyimbo za Kampeni za Wachuka.* Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Thika: Chuo Kikuu cha Mount Kenya.

Omondi, O. (2017). *Urudiaji na Uwasilishaji wa Maana katika Ushairi wa Kisasa*. Tasnifu ya Uzamifu (Haijachapishwa). Nairobi: Chuo Kikuu cha Nairobi.

Oyoo, M. (2003). *Theory of Children's Literature: A Module*. Nairobi: The Catholic University of Eastern Africa, Literature Department.

Perrine, L. (1959). *Brownings dramatic monologue: The strategy of the double mask*. London: Cambridge University Press.

Mount Kenya University

Ponera, S. (2019). *Misingi ya Utafiti wa Kitaamuli na Uandishi wa Tasnifu*. Dodoma: Central Tanganyika Press.

Rief, S. (2012). How to Reach and Teach Children with ADD/ADHD: Practical Techniques, Strategies and interventions, 2nd edition. San Frasisco: Jossey-Bass Publishers.

Rowe, T. (1939). *Write that Play*. New York: Funk and Wagnalls Publishers.

Sengo, T. (2009). *Sengo na Fasihi za Kinchi*. Dar es Salaam: Aera Kiswahili Researched Products.

Senkoro, F. (1988). *Ushairi: Nadharia na Tahakiki*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Senkoro, F. (2011). *Fasihi*. Dar es Salam: KAUTTU.

Shanahan, T. (2014). This is not close reading (but we'll tell you what it is). *Instructor 123(1),* 28-30.

Smith, D. (2013). *Phenomenology: The Stanford Encyclopedia of philosophy of Mind The Metaphysics Research lab, center for the study of language and information*. New York: Stanford University Press.

Sweetlands, R. (2017). Elements of Story or Fiction - character, setting, plot, point of view, style, tone, theme. www.homeofbob.com/literature/genre/fiction/ficElements.html

Syambo, B. na Mazrui, A. (1992). *Uchambuzi wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational Publishers.

TUKI. (2013) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la 3.* Nairobi: Oxford University Press.

Mount Kenya University

Walibora, K. (1996). *Siku Njema*. Nairobi: Longhorn Publishers.

Walibora, K. (2003). *Kufa Kuzikana*. Nairobi: Longman Publishers.

Walibora, K. (2006). *Ndoto ya Almasi*. Nairobi: Moran Publishers.

Walibora, K. (2012). *Kidagaa Kimemwozea*. Nairobi: Target Publications.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa fasihi: Msingi na vipengele vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Nadharia na Istilahi*. Nairobi: Focus Publications.

Wamitila, K. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: Focus Publishers.

Wamitila, K. (2008). *Kanzi ya fasihi I: Uchanganuzi wa fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.

Mount Kenya University

# VIAMBATISHO

## KIAMBATISHO A: BARUA YA UTAMBULISHO

**Mount Kenya University**

MKU

Unlocking Infinite Possibilities

**DIRECTORATE OF GRADUATE STUDIES**

**MAKI/2022/51252**

**25th April, 2024**

***National Commission for Science Technology & Innovation (NACOSTI)***
***Off Waiyaki Way, Upper Kabete,***
***P.O Box 30623- 00100***
***NAIROBI, KENYA***

Dear Sir/Madam,

**RE: WYCKLIFFE COLLINS JAOKO- REGISTRATION NO. MAKI/2022/51252**

The purpose of this letter is to introduce the above named student who is pursuing **Master of Arts in Kiswahili** in the Department of **Psychology, Languages and Humanities** in the School **of Social Sciences.**

The title of the research is" **Usawiri wa Mandhari Katika Riwaya ya Kiswahili: Mfano wa Kiu (Mohamed, 1972) Na Kidagaa Kimemwozea (Walibora 2012."** It has been cleared by the University's Ethics Review Committee (Certificate attached) and now has to proceed to the field to collect data between **May, 2024 and July, 2024.**

Any assistance accorded to the student will be highly appreciated.

Thank you.

Mount Kenya University
P. O. Box 342 - 01000.THIKA
Office of the Director,
Graduate Studies

**Dr. Samuel M. Karenga, Ph.D**
**Director, Graduate Studies**
Enc.

Main Campus, General Kago Road, P.O. Box 342-01000 Thika.
Cell: +254 709 153 000 | +254 709 153 200
Email: info@mku.ac.ke, Web: www.mku.ac.ke
**Chartered and ISO 9001 : 2015 Certified Institution.**
**Unlocking Infinite Possibilities**

## KIAMBATISHO B: CHETI CHA IDHINI

**Mount Kenya University**

REF: **MKU/ISERC/3644** Date: 25 April 2024

TO: **WYCKLIFFE COLLINS JAOKO**

REG: **MAKI/2022/51252**

Dear Sir/Madam,

**RE: USAWIRI WA MANDHARI KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI: MFANO WA KIU (MOHAMED, 1972) NA KIDAGAA KIMEMWOZEA (WALIBORA, 2012)**

This is to inform you that **Mount Kenya University** has reviewed and approved your above research proposal. Your application approval number is **2688.** The approval period is **25/04/2024 - 24/04/2025.**

This approval is subject to compliance with the following requirements;

i. Only approved documents including informed consents, study instruments, MTA will be used

ii. All changes including amendments, deviations and violations are submitted for review and approval by **Mount Kenya University**

iii. Death and life threatening problems and serious adverse events or unexpected adverse events whether related or unrelated to the study must be reported to **Mount Kenya University** within 72 hours of notification

iv. Any changes, anticipated or otherwise that may increase the risks or affect the safety or welfare of study participants and others or affect the integrity of the research must be reported to **Mount Kenya University** within 72 hours

v. Clearance for export of biological specimens must be obtained from relevant institutions

vi. Submission of a request for renewal of approval at least 60 days prior to expiry of the approval period. Attach a comprehensive progress report to support the renewal

vii. Submission of an executive summary report within 90 days upon completion of the study to **Mount Kenya University**

Yours sincerely,

The Chairman
Mount Kenya University
Ethics Review Committee
P. O. Box 342 - 0100, Thika

**Dr. Alfred Owino, PhD**
**Chairman, Mount Kenya University ISERC**

Main Campus, General Kago Road, P.O. Box 342-01000 Thika.
Cell: +254 709 153 000 | +254 709 153 200
Email: info@mku.ac.ke, Web: www.mku.ac.ke
Chartered and ISO 9001 : 2015 Certified Institution.
Unlocking Infinite Possibilities

## KIAMBATISHO C: IDHINI YA NACOSTI

REPUBLIC OF KENYA

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Ref No: **322722**

Date of Issue: **14/May/2024**

### RESEARCH LICENSE



**This is to Certify that Mr.. WYCKLIFFE COLLINS JAOKO of Mount Kenya University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Kisumu on the topic: USAWIRI WA MANDHARI KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI: MFANO WA KIU (MOHAMED, 1972) NA KIDAGAA KIMEMWOZEA (WALIBORA, 2012) for the period ending : 14/May/2025.**

License No: **NACOSTI/P/24/35366**

**322722**

Applicant Identification Number

Director General

NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**See overleaf for conditions**

National Commision for Science, Technology and Innovation -

**THE SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION ACT, 2013 (Rev. 2014)**

Legal Notice No. 108: The Science, Technology and Innovation (Research Licensing) Regulations, 2014

**The National Commission for Science, Technology and Innovation**, hereafter referred to as the Commission, was the established under the Science, Technology and Innovation Act 2013 (Revised 2014) herein after referred to as the Act. The objective of the Commission shall be to regulate and assure quality in the science, technology and innovation sector and advise the Government in matters related thereto.

**CONDITIONS OF THE RESEARCH LICENSE**

1. The License is granted subject to provisions of the Constitution of Kenya, the Science, Technology and Innovation Act, and other relevant laws, policies and regulations. Accordingly, the licensee shall adhere to such procedures, standards, code of ethics and guidelines as may be prescribed by regulations made under the Act, or prescribed by provisions of International treaties of which Kenya is a signatory to
2. The research and its related activities as well as outcomes shall be beneficial to the country and shall not in any way;
    i. Endanger national security
    ii. Adversely affect the lives of Kenyans
    iii. Be in contravention of Kenya's international obligations including Biological Weapons Convention (BWC), Comprehensive Nuclear-Test-Ban Treaty Organization (CTBTO), Chemical, Biological, Radiological and Nuclear (CBRN).
    iv. Result in exploitation of intellectual property rights of communities in Kenya
    v. Adversely affect the environment
    vi. Adversely affect the rights of communities
    vii. Endanger public safety and national cohesion
    viii. Plagiarize someone else's work
3. The License is valid for the proposed research, location and specified period.
4. The license any rights thereunder are non-transferable
5. The Commission reserves the right to cancel the research at any time during the research period if in the opinion of the Commission the research is not implemented in conformity with the provisions of the Act or any other written law.
6. The Licensee shall inform the relevant County Director of Education, County Commissioner and County Governor before commencement of the research.
7. Excavation, filming, movement, and collection of specimens are subject to further necessary clearance from relevant Government Agencies.
8. The License does not give authority to transfer research materials.
9. The Commission may monitor and evaluate the licensed research project for the purpose of assessing and evaluating compliance with the conditions of the License.
10. The Licensee shall submit one hard copy, and upload a soft copy of their final report (thesis) onto a platform designated by the Commission within one year of completion of the research.
11. The Commission reserves the right to modify the conditions of the License including cancellation without prior notice.
12. Research, findings and information regarding research systems shall be stored or disseminated, utilized or applied in such a manner as may be prescribed by the Commission from time to time.
13. The Licensee shall disclose to the Commission, the relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee, and the relevant national agencies any inventions and discoveries that are of National strategic importance.
14. The Commission shall have powers to acquire from any person the right in, or to, any scientific innovation, invention or patent of strategic importance to the country.
15. Relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee shall monitor and evaluate the research periodically, and make a report of its findings to the Commission for necessary action.

National Commission for Science, Technology and Innovation(NACOSTI),
Off Waiyaki Way, Upper Kabete,
P. O. Box 30623 - 00100 Nairobi, KENYA
Telephone: 020 4007000, 0713788787, 0735404245
E-mail: dg@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke

## KIAMBATISHO D:KIZIO CHA MFANANO MATINI

USAWIRI WA MANDHARI KATIKA RIWAYA YA KISWAHILI: MFANO WA KIU NA KIDAGAA KIMEMWOZEA

ORIGINALITY REPORT

| 11% | 11% | 2% | 6% |
|---|---|---|---|
| SIMILARITY INDEX | INTERNET SOURCES | PUBLICATIONS | STUDENT PAPERS |

PRIMARY SOURCES

| | | |
|---|---|---|
| 1 | erepository.uonbi.ac.ke<br>Internet Source | 2% |
| 2 | repository.out.ac.tz<br>Internet Source | 1% |
| 3 | ir-library.ku.ac.ke<br>Internet Source | 1% |
| 4 | repository.suza.ac.tz:8080<br>Internet Source | 1% |
| 5 | www.coursehero.com<br>Internet Source | 1% |
| 6 | Submitted to University Der Es Salaam<br>Student Paper | 1% |
| 7 | ir.mu.ac.ke:8080<br>Internet Source | 1% |
| 8 | Submitted to Kenyatta University<br>Student Paper | <1% |
| 9 | teacher.co.ke<br>Internet Source | <1% |

| | | |
|---|---|---|
| 10 | Submitted to Eiffel Corporation<br>Student Paper | <1% |
| 11 | core.ac.uk<br>Internet Source | <1% |
| 12 | ir-library.mmust.ac.ke:8080<br>Internet Source | <1% |
| 13 | Submitted to Kisii University<br>Student Paper | <1% |
| 14 | journals.eanso.org<br>Internet Source | <1% |
| 15 | taifaleo.nation.co.ke<br>Internet Source | <1% |
| 16 | Submitted to University of Rwanda<br>Student Paper | <1% |
| 17 | repository.rongovarsity.ac.ke<br>Internet Source | <1% |
| 18 | Submitted to Eastern University<br>Student Paper | <1% |
| 19 | Submitted to University of Brighton<br>Student Paper | <1% |
| 20 | www.jamiiforums.com<br>Internet Source | <1% |
| 21 | ir-library.mmarau.ac.ke:8080<br>Internet Source | <1% |

| | | |
|---|---|---|
| 22 | ir.kabarak.ac.ke<br>Internet Source | <1 % |
| 23 | repository.seku.ac.ke<br>Internet Source | <1 % |
| 24 | cujos.cumhuriyet.edu.tr<br>Internet Source | <1 % |
| 25 | www.journals.eanso.org<br>Internet Source | <1 % |
| 26 | Submitted to Masinde Muliro University of Science and Technology<br>Student Paper | <1 % |
| 27 | kcpe-kcse.com<br>Internet Source | <1 % |
| 28 | eastafricans.org<br>Internet Source | <1 % |
| 29 | repository.embuni.ac.ke<br>Internet Source | <1 % |
| 30 | Submitted to UNICAF<br>Student Paper | <1 % |
| 31 | journals.uonbi.ac.ke<br>Internet Source | <1 % |
| 32 | Submitted to American College of Education<br>Student Paper | <1 % |
| | Submitted to St Mary's School, Nairobi | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 33 | Student Paper | | <1 % |
| 34 | escholarship.org<br>Internet Source | | <1 % |
| 35 | mwalimuwakiswahili.co.tz<br>Internet Source | | <1 % |
| 36 | www.qucosa.de<br>Internet Source | | <1 % |
| 37 | www.rucu.ac.tz<br>Internet Source | | <1 % |
| 38 | ir.mksu.ac.ke<br>Internet Source | | <1 % |
| 39 | zenodo.org<br>Internet Source | | <1 % |
| 40 | erepository.uonbi.ac.ke:8080<br>Internet Source | | <1 % |
| 41 | www.tie.go.tz<br>Internet Source | | <1 % |
| 42 | repository.maseno.ac.ke<br>Internet Source | | <1 % |
| 43 | Submitted to Pwani University<br>Student Paper | | <1 % |
| 44 | Submitted to The University of Dodoma<br>Student Paper | | <1 % |

| | | |
|---|---|---|
| 45 | erepository.kibu.ac.ke<br>Internet Source | <1 % |
| 46 | rucu.ac.tz<br>Internet Source | <1 % |
| 47 | afrika.univie.ac.at<br>Internet Source | <1 % |
| 48 | jwmr.sanru.ac.ir<br>Internet Source | <1 % |
| 49 | researchspace.ukzn.ac.za<br>Internet Source | <1 % |
| 50 | Saade Said Mbarouk. " Uchambuzi wa Riwaya ya Kwa Kutumia Nadharia ya Saikolojia Changanuzi ", Eastern African Literary and Cultural Studies, 2019<br>Publication | <1 % |
| 51 | erepository.kafu.ac.ke<br>Internet Source | <1 % |
| 52 | ijojournals.com<br>Internet Source | <1 % |
| 53 | dos.chuka.ac.ke<br>Internet Source | <1 % |
| 54 | elibrary.pu.ac.ke<br>Internet Source | <1 % |
| 55 | etd.lib.metu.edu.tr<br>Internet Source | |

<1 %

| | | |
|---|---|---|
| 56 | iajournals.org<br>Internet Source | <1 % |
| 57 | docplayer.fi<br>Internet Source | <1 % |
| 58 | fr.m.wikipedia.org<br>Internet Source | <1 % |
| 59 | saspublishers.com<br>Internet Source | <1 % |
| 60 | Masola, Isaac Sello. "Towards a Methodological Model for the Teaching of Northern Sotho Poetry at Colleges of Education", University of Johannesburg (South Africa), 2021<br>Publication | <1 % |
| 61 | Given. The SAGE Encyclopedia of Qualitative Research Methods<br>Publication | <1 % |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Exclude quotes | Off | Exclude matches | Off |
| Exclude bibliography | Off | | |